Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 6 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**SPIKA:** Waheshimiwa wabunge, kabla sijamwita Naibu Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, natumaini mmekuwa na *weekend* nzuri na yenye utulivu kama aliyokuwa nayo Spika na kwa hiyo niwatakie kazi njema kwa juma hili pamoja sikukuu njema ya SABA SABA hapo kesho. (*Makofi*)

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi ka Kujenga Taifa kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwafahamisha kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo Dar es Salaam kwa shughuli maalum za kikazi na kama kawaida amemwacha Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Masuala ya Muungano mambo yote ya kuendesha shughuli za Serikali humu ndani ya Bunge ataendelea Mheshimiwa Khatibu hadi hapo Waziri Mkuu atakaporejea.

Naomba upande huu wa pili nadhani Mheshimiwa Masoud ataendeleza shughuli za Kambi ya Upinzani hadi hapo wenyewe watakaporejea. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, Swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Anne K. Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki.

Na. 162

**Adhabu ya Kuhamisha Watendaji wa Kata/Vijiji**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, imekuwa ni jambo la kawaida sana kwamba, Ofisa Mtendaji wa Kata au Kijiji akiharibu kazi katika Kata au Kijij kimoja hupewa adhabu ya kuhamishwa kwenda kata au kijiji kingine.

Je, Serikali inaona mfumo huo ni sahihi ?

**SPIKA:** Pole sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi naelewa umetoka kwenye msiba wa wifi yako, tunakupa pole sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika utumishi wa Umma kuna uhamisho wa aina kuu mbili. Kwanza, ni uhamisho wa mtumishi mwenye kuomba kuhamishwa kutokana na sababu zake binafsi. Pili, ni uhamisho wa kawaida ambao Mwajiri na Mamlaka yauhamisho huhamisha watumishi kwa nia ya kuboresha utendaji kazi kwani uzoefu umeonyesha kwamba mtumishi anapokaa kituo kimoja kwa muda mrefu ufanisi wake wa kazi hushuka kutokana na kuzoea mazingira na hivyo kufanya kazi kwa mazoea bila ubunifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8/2002 Kifungu 107 Mamlaka ya kufanya uhamisho wa watumishi wa Umma ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hata hivyo, kwa sasa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma amekasimu mamlaka ya uhamisho kwa watumishi wa Serikali za Mitaa kutoka Mkoa moja kwenda Mkoa mwingine kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Uhamisho kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine ndani ya Mkoa, Mamlaka yamekasimiwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika. Aidha, ndani ya Halmashauri ni Halmashauri yenyewe ambapo Mtendaji Mkuu ni Mkurugenzi wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu katika Ofisi yangu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Watendaji wa Kata na Vijiji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same waliohamishwa ni pamoja na Watendaji wa Kata 12 na Watendaji wa Vijiji 21. Uhamisho huo ulifanyika kwa sababu ya kuboresha utendaji kwa watendaji wote wa Kata. Kwa watendaji wa Vijiji uhamisho wa kuomba ulikuwa ni watumishi watano na uhamishi wa sababa ya kuboresha utendaji walikuwa ni watumishi kumi na sita.

Vilevile, watendaji kumi na tano wamechukuliwa hatua za kinidhamu na kati hayo saba ni watendaji wa Kata nane ni Watendaji wa vijiji. Watumishi hao wamechukuliwa hatua za nidhamu kutokana na kukiuka Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8/2002.

Mheshimiwa Spika, uhamishi siyo adhabu inapothibitika Watendaji wana utendaji mbovu huchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8/2002 na siyo vinginevyo. Kwa upande mwingine Watendaji wa Kata au Vijiji wanaoharibu kazi hawastahili kuhamishwa badala yake Halmashauri kama Mamlaka ya Nidhamu inapaswa kuchukuliwa hatua za nidhamu. Hivyo Serikali haina mfumo wa kutoa adhabu ya kuhamisha watendaji wa Kata na Vijiji wanapokuwa na makosa.

Aidha, kama mtendaji atakuwa amehamishwa ndani ya Halmashauri bado Halmashauri kama mamlaka ya nidhamu inaweza kuendelea na mchakato wa kuchukua hatua za kinidhamu.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, niseme sijaridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa wananchi wa Tanzania wa majimbo yote wanajitahidi sana kujiletea maendeleo wenyewe, lakini kama kuna kikwazo kikubwa cha wananchi ni hawa Watendaji wa vijiji, inapofika kwamba wananchi wetu wanatoa michango yao na hawapati mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hawa waliohamishwa Same wamehamishwa lakini wote wamehamishwa baada ya matakwa ya wananchi kwa hiyo bado Serikali haijajibu. Je ni lini Serikali itakuwa inawahamisha wale ambao wananchi wakiwalalamikia wanawachukulia hatua badala ya kuwahamisha kuwatoa Same Mashariki na kuwapeleka Same Magharibi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne K. Malecela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba Mamlaka ya Nidhamu ni Halmashauri husika, kwa Watendaji wa Kata hadi Wakuu wa Idara, Mamlaka ya Nidhamu ni Halmashauri husika. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inamshughulikia Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya tu ambaye atakuwa amekosa nidhamu.

Lakini hata hivyo, kwa wale Watendaji wa Vijiji na Kata ambao wamekosa nidhamu, Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni Waheshimiwa Madiwani katika Mamlaka husika mimi ninachoomba wachukuliwe hatua za kinidhamu palepale walipo na si vinginevyo hakuna sehemu inayotaka mtumishi mbovu. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba si vema kumhamisha mtumishi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Kwa hiyo, nitoe tu rai kwamba Mamlaka ya Nidhamu ni Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kwa kuwatoa watumishi wabovu na si vinginevyo. (Makofi)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu swali la msingi amesema kwamba si vizuri watumishi wakae kituo kimoja muda mrefu kwa sababu wanaweza wakafanya kazi kwa mazoea. Lakini ukweli unabaki palepale kwamba

watumishi wengi wanakaa kituo kimoja zaidi ya miaka kumi au kumi na tano na pale ambapo Halmashauri zinaomba wahamishwe tatizo huwa fedha.

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa pesa za uhamisho kwa watumishi kwa watumishi ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu ili waweze kwenda maeneo mengine kwa maana ya kwamba waepuke pia kufanya kazi kwa mazoea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godfrey Zambi, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna watumishi wengi sana wa Serikali za Mitaa ambao wamekaa sehemu moja zaidi ya miaka kumi na tano.

Mheshimiwa Spika, rai hii ilitolewa na Wabunge wengi katika Bunge lako la mwaka 2006 na kuanzia mwaka 2006 hadi sasa hivi tumehamisha watumishi wapatao 1500 kwa ajili tu ya kuboresha ufanisi wa kazi kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Lakini niseme tu kwamba huwezi ukawahamisha watumishi wote kwenye Halmashauri kwa wakati mmoja ndiyo maana tunafanya kwa awamu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zambi kama anaona kwamba kwenye Halmashauri yake kuna watumishi ambao wamekaa muda mrefu naomba tuwasiliane ili tuwahamishe kwa nidhamu si vema kuwatoa watumishi wote kwa wakati mmoja na kuweka watumishi wapya bali tunawatoa kwa awamu kulingana na shida iliyopo, uwezekano wa kubadilishana watumishi na upatikanaji wa watumishi kutoka katika sekta husika.

Na. 163

**Ubinafishaji wa Shirika la Reli Tanzania**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na mtatizo mengi baada ya Shirika la Reli Tanzania kuingia ubia na Wawekezaji binafsi:-

(a) Je, Serikali inasemaji juu ya uwezo wa kifedha wa wawekezaji hao ?

(b) Je, tangu kubinafsishwa kwake, ni faida gani au hasara gani imepatikana ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu majibu tafadhali! Hawa jamaa sijui wanakutafuta nini hawakuachii hata baada ya Makadirio kupita. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kwamba, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* halikuingia ubia na wawekezaji binafsi, bali ni Serikali ya Tanzania ndiyo iliyoingia ubia na *RITES* ya India na kuunda kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* kwa mgawanyo wa hisa 51% za *RITES* na 49% za Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokuwa inaingia mkataba na wawekezaji hawa ilikwishafanya tathmini na kuridhika na kuwa wanao uwezo wa wastani wa fedha kuwawezesha kuendesha shughuli za Shirika la Reli na hasa kwa kuzingatia kwamba makampuni yenye uwezo mkubwa hayakujitokeza kushiriki kuomba uendeshaji wa Shirika la Reli.

Kwa kutambua uwezo huo wa wastani tokea mwanzo ndiyo maana Serikali ya Tanzania kama mwanahisa wa Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* ilikubali kudhamini mkopo wa fedha *USD 44* milioni kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IFC)* ili kuwezesha Kampuni hiyo kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya ukodishwaji wa shirika la Reli, *TRL* kama mwekezaji ameweza kufanya yafuatayo:-

(i)Kuwekeza kiasi cha dola za kimarekeni milioni 10.2 Kama mtaji wa kuanzisha kampuni.

(ii)Kulipa Mishahara yote ya Menejimenti ya Juu ya Kampuni pamoja na sehemu ya mishaahara ya watumishi wengine.

(iii)Kukodisha vichwa 25 vya treni na mabehewa 23 kutoka kampuni ya *RITES* ya India.

(b)Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ya kiutendaji yanayolikabili Shirika la Reli ambayo Serikali inaendelea kuyashughulikia, faida zifuatavyo zimepatikana.

(i)Huduma ya usafiri imeweza kurejeshwa kuanzia Dar es Salaam badala ya Dodoma ambapo kuanzia mwaka 2004, TRC walihanishia karibu huduma zote kutoka Dar es Salaam na kuzipeleka Dodoma umbali wa kilomita 465. Hali hii imesaidia kuwapunguzia adha ya usafiri wananchi, kupunguza gharama ya wajasiria mali na kuokoa fedha za matengenezo ya mara kwa mara ya barabara ambayo ilikuwa inapitisha magari yenye uzito mkubwa kwenda Dodoma.

(ii)Imerejesha huduma za uchukuzi wa mizigo kwa Reli ya Dar es Salaam, Tanga, Korogwe, Moshi hadi Arusha. Usafirishaji wa mizigo kutoka Tanga hasa saruji

umesaidia kwa kiwango kikubwa viwanda vya Tanga kupunguza gharama za usafirishaji japokuwa treni huenda tupu kutoka Dar es Salaam.

(iii)*TRL* imeendeleza kutoa huduma za treni ya abiria na mizigo kwa reli za Manyoni- Singida na Kaliua – Mpanda.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana pamoja na Mheshimiwa Waziri kuacha kutaja hasara ambazo zimetokea baada ya kubinafsishwa Shirika hili. Mimi nadhani hasara ni nyingi zaidi kuliko faida ambazo amezitaja na pengine angeliambia Bunge lako hili kwamba hivi tatizo la kurekebisha mkataba ni tatizo la kitu gani hasa? Kwa nini mkataba haurekebishwi? Hivi huu ni Msahafu ambao haurekebishwi au kuguswa kabisa?

Pamoja na kutaja kwamba kuna gharama ambazo zimeingiwa na Shirika la *RITES* la kukodisha mabehewa na injini. Mabehewa na injini zilizokodishwa kwanza ni za gharama kubwa sana yaani za bei ya juu. Lakini vilevile ni za kizamani za miaka ya 1960 zikaachwa za kwetu za miaka ya 1990. Haoni nayo hii ni kubebesha mzigo wa bure kwa shirika na ingewezekana tukanunua mabehewa yetu na injini zetu sisi wenyewe kwa sababu pesa tulikuwa nazo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Selelii kama ifuatavyo. Mkataba huu siyo kitabu kitakatifu yaani si *Quran* wala si Biblia na wala Serikali haina kigugumizi chochote katika kuujadili na kuurekebisha mkataba huu kwa manufaa ya Watanzania. Serikali imeanza kufanya kazi hiyo na majadiliano ni majadiliano ya pande mbili siyo kitu ambacho kufumba na kufumbua unaweza ukajadili kitu ukakimaliza papo kwa papo, hili ni jambo la mchakato lazima lichukue muda, lazima waitwe Wataalam wa pande mbili waangalie kwa umakini pale ambapo jambo limekosewa liweze kurekebishwa kwa ridhaa za pande mbili. Sasa hivi Serikali imeunda vikundi kazi viwili, kimoja kinaangalia mpango wa biashara wa kampuni na kikundi kazi cha pili kinafanya mapitia mikataba yote mitatu *Concessions Agreement Shareholder Agreement* pamoja na *MEMATS* mabazo zimeunda *TRL* ili kuhakikisha kwamba maslahi ya Mtanzania yamelindwa na tunapata reli ambayo itakuwa na maslahi na manufaa kwa wananchi wa Tanzania.

Swali la pili, mabehewa na injini ambazo zimekodishwa ni mabehewa na injini zile ambazo kampuni yetu inasimia mali za Serikali imeridhia yakodiwe, kwa mfano vichwa. Ilivyokuwa *TRC* ilikodi vichwa *73 R-class* kutoka *RITES* kabla *TRC* haijabinafsishwa au miundombinu yake haijakodishwa kwa *TRL*.

Wakati TRL inachukua miundombinu kumi 73Class na imeendelea kukodi vichwa aina hiyohiyo baada ya kuingiza katika ukodishaji wa miundimbonu hii siyo vichwa vya mwaka 60 ni vichwa ambavyo sisi tulishakuwa tunavikodi na mpaka hapo miundimbinu yetu itakapoweza kuchukua vichwa vya aina nyingine Serikali haitasita kukodisha vichwa ambavyo vinaendana na mahitaji ya reli yetu.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na pia nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ilitangaza mpango maalum wa kuwapeleka Watanzania katika kombe la dunia kwa kupitia reli ya *TAZARA*. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Bunge hili Serikali imejipangaje ili kuhakikisha Watanzania hawa wanakwenda na kurudi salama bila kuwakama njiani na kuona kombe hili la dunia?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hili ni swali jipya, Mheshimiwa Hafidh akipenda basi alilete rasmi ili liweze kujibiwa.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, swali linaulizwa na Mheshimiwa George Lubeleje wa Mpwapwa.

Na. 164

**Taasisi ya Taifa ya Utafiti Mpwapwa Kupatiwa Vitendea Kazi**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Taasisi ya Taifa ya utafiti wa Mifugo *(NLRI)* Mpwapwa ina upungufu mkubwa wa vitendea kazi na kwamba, vile vilivyopo vimechakaa sana, na kwa kuwa, hali hiyo husuia ufanisi wa kituo hicho katika kuhudumia maeneo ya vijijini.

Je, serikali ina mpango gani wa kutoa vitendea kazi kwa Taasisi hiyo kama vile magari mapya, matrekta na mashine mbalimbali zinazotumika kituoni hapo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Taasisi ya Taifa ya utafiti wa Mifugo ya Mpwapwa ina upungufu wa vitendea kazi yakiwemo magari, matrekta, mashine za kukamulia maziwa na vifaa vya maabara ambavyo ni muhumu katika kazi zake za utafiti.

Ili kuimarisha utendajikazi katika Taasisi hiyo, Wizara yangu imekuwa ikinunua viaa na vitendea kazi mbalimbali kwa awamu kulingana na uwezo wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2007/2009 Wizara yangu iliinunulia Taasisi hiyo gari moja jipya aina ya *Toyota Land cruiser Station Wagon*. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 Wizara imenunulia Taasisi hiyo magari mapya mawili aina ya *Toyota Double Cabin*, *Computer* 3 na *Printer 2.*

Aidha, katika kuimarisha Taasisi hiyo na vituo vingine vilivyopo ndani ya eneo hilo, katika mwaka 2008/2009, kituo cha Uchunguzi wa Mgonjwa ya Vifugo *(VIC)* kilinunuliwa kompyuta moja na pia kuunganishwa kwenye mtandao wa *Internet*.

Aidha, Chuo cha Mafunzo ya Mifugo cha Mpwapwa nacho kilinunuliwa kompyuta saba na kuunganishwa kwenye mtandao wa *internet* na kununuliwa vifaa vya mabara ikiwa ni pamoja na *Autoclave*, *Surgical Trolley* moja, *Centrifuge* moja, *Sterilizer* moja, *Microscopes* tatu, *Cool Box* moja, *Instrument Trays* tatu na *Straining Racks* kumi na tano.

Katika bajeti ya mwaka 2009/2010 Wizara yangu imetenga fedha kwa ajili ya kununua trekta moja na zana zake ikiwa ni pamoja na mashine moja ya kukata na kufunga nyasi, (*bailer*). Aidha, wizara itanunua mashine moja ya kukamulia maziwa na nyingine moja ya kutotolewa vifaranga watakaotokana na mayai ya kuku wa asili.

Vilevile Wizara yangu itaagiza vifaa mbalimbali vya maabara vya kutathmini ubora wa vyakula vya mifugo, ambavyo ni pamoja na *Proximate Analyser*, mashine ya kusaga vyakula (*Grinding machine*) na mashine ya kuchuja mvuke (*distiller*).

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa vitendea kazi hivi utaboresha shughuli za utafitikatika taasisi hiyo muhimu ya utafiti wa mifugo kwa ujumla hapa nchini. Wizara itaendelea na jitihada hizo hadi hapo Taasisi itakapoweza kujitosheleza katika vitendea kazi vitakavyohitajika.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawil ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

La kwanza, kwa kuwa, Taasisi ya utafiti wa mifugo ya Mpwapwa haijatambulika kisheria na kwa kuwa Serikali inaandaa Muswada, ni lini Muswada huu utaletwa Bungeni ili Taasisi hii iweze kutambulika kisheria?

La pili, kwa kuwa hivi sasa watafiti wanahama na kwenda kwenye Taasisi nyingine kwa sababu ya maslahi duni. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuongeza maslahi ya watafiti ili wasihame?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifutavyo.

Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Lubeleje anavyofuatilia mwenendo wa Taasisi hii. Mwaka 2007/2008 wakati Kamati inajadili Mheshimiwa Lubeleje alikuja na kutueleza namna hali ilivyo na mwaka huu vilevile alikuja wakati huo alitoka akicheka kwa sababu kwa kweli tumempa hela nyingi yaani

Taasisi hiyo imepewa hela nyingi.  Vilevile amewahi kunialika mimi kutembelea ile Taasisi tukaenda tukaandangalia na ile safari ilisaidia sana mambo mengi katika Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Taasisi hiyo ya Mpwapwa miaka ya 80 ilikuwa katika kituo kikuu cha Tanzania Live *Stock Research Instute,* lakini mwaka 1988 taasisi hii ilirudishwa kuwa Idara ya Serikali na kwa kufanya hivyo imefanya mafao ya wafanyakazi ukilinganisha na wale waliopo Chuo Kikuu Taasisi ya *TAFIR* ambayo  iko chini ya Wizara yetu wale wanapata mishahara mikubwa lakini hawa kwa sababu ni Idara ya Serikali wanapata mishahara midogo sana.

Sasa tumelitambua hilo na tunaandaa Muswada ambao utawasilishwa hapa Bungeni  umeshapita kwenye *cabinet secretariat,* utapitia kwa Makatibu Wakuu Baraza la Makatibu Wakuu halafu ukishapita utakwenda kwenye Baraza la Mawaziri, nia yetu ni kuanzisha Taasisi hiyo ili hawa ili hawa wafanyakazi waweze kupata mafao mazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba wafanyakazi wanahama kwa sababu mishahara ni midogo, nimekwenda pale Uyole nikangalia hali mbaya sana, nimekwenda Mpwapwa pia hali ni ngumu sana. Sasa nia yatu ni kuifanya hii Taasisi tukishaanzisha tukaifanya Taasisi mishahara yao itakuwa ni sawasawa na ile ya Chuo Kikuu na Taasisi nyingine za Serikali ambayo mishahara kwa sasa wanapata ni mizuri sana. Kwa hiyo, tutaharakisha kuleta huo Muswada ili kuboresha mafao ya hawa wafanyakazi ili wasihame kwenda sehemu nyingine.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika,nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mifugo mingi iko vijijini na Wilayani hakuna vifaa vya kupimia magonjwa aya mifugo, kwa hiyo Wataalamu wa mifogo w anabuni tu kwamba huyu ng’ombe inawezekana ana ugonjwa fulani. Ni lini Serikali itapeleka vifaa vya kupima mifugo wilayani ili wananchi waweze kujua magonjwa yanayowakabili mifugo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA MAENDELEO YA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Ni kweli magonjwa hutokea huko vijijini lakini sisi tunayo **system** pale pale Wilayani yule *Livestock Officer*  huwa anakusanya taarifa yoyote ambayo imetokea kwa magonjwa na tuna vituo vyetu *Vetnary Information Investigation Centre* ambavyo vile huchukua zile sample, yaani wanachukua sample ya mfugo huo na kutuma katika *laboratory* yetu iliyopo Temeke kwa hiyo hiyo ndiyo inafanya *analysis* na kujua kwamba ni ugonjwa gani na kuchukua hatua.

Kwa hiyo, *sample* hizo zinakusanywa kila wakati tunafanya *severance collection* na kubaini kama kuna magonjwa yanashughulikiwa.

Kwa hiyo, kule wilayani wata *collect* tu *information data* na kupitisha *Vetnary Information Centre* na kutuletea na *laboratory* yetu kwa mwaka huu imeimarishwa sana ni bahati nzuri sana kwamba mwaka jana ilipata milioni kama 400 na mwaka huu.

Na. 165

**Mpango wa Upatikanaji wa Pembejeo za Salfa**

**MHE. JUMA A.NJWAYO (K.n.y. MHE. RAYMOND MROPE)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna mpango mzuri wa mfuko wa pembejeo Wilayani ambapo wananchi wengi wamejiunga ilikupata huduma nzuri kwa mazao ya biashara na chakula, na kwakuwa zao la korosho linategemea sana upatikanaji na mapema na upuliziaji wa Salfa *( surphur)*.

(a)Je, kuna mpango gani kitaifa wa kupata salfa kwa Mikoa inayolima korosho nchini?

(b)Je, kwanini Serikali huchelewa kutoa fedha za ruzuku kiasi kwamba salfa inafika baada ya mwezi mei wakati ambapo wakulima wengi wanahaha kwa kukosa pembejeo hiyo muhimu?

(c)Je, Serikali inafahamu kuwa inaleta ukiritimba kwa kuchagua wakala mmoja kuleta salfa Mkoani Mtwara na hivyo wakulima wanakosa huduma hiyo kwa wakati, kufedheheshwa na kukosa imani na Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:**Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Jimbo la Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a)Tangu Serikali ilipoanza kutoa ruzuku ya madawa ya korosho mwaka wa 2004/2005, mahitaji ya madawa yamekuwa yakiainishwa na Wilaya za Mikoa inayolima zao la korosho kabla ya mwezi wa februari kila mwaka.

Baada ya kupata mahitaji hayo, Bodi ya korosho Tanzania *(CBT)* kwa niaba ya Wizara huwasiliana na makampuni yanayoingiza madawa hayo ikiwemo salfa na kuingia nayo mikataba ya usambazaji wa kusimamia ulipaji wa ruzuku ya bei baada ya wakulima kulipa sehemu ya bei iliyopangwa na Serikali. Lengo ni kuhakikisha kwamba pembejeo hiyo inamfikia mkulima kwa wakati na kwa bei nafuu kwa madhumuni ya kuongeza tija katika zao la korosho.

(b) Fedha za ruzuku kwa zao la korosho zinatokana na vyanzo vikuu viwili ambavyo ni mgao wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na ushuru wa korosho zinazouzwa nje ya nchi zikiwa ghafi.

Mgao wa Bajeti kutoka katika Wizara umekuwa ukipelekwa *CBT* katika miezi ya machi au Aprili ya kila mwaka kwa mfano fedha za ruzuku ya madawa kwa msimu wa 2007/2008 ziliandaliwa na kutolewa mwezi Aprili, 2008, fedha za ushuru wa korosho ambazo zilikusanywa na mamlaka ya mapato Tanzania *(TRA)* katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Tanga na Dar es Salaam zimekuwa zikipelekwa *CBT* kila mwezi wa Sita au wa Saba wa kila mwaka.

Katika vipindi hivyo, yaani Machi hadi Julai, wasambazaji wa madawa huwa hawajaanza kudai malipo yao kwa kuwa matumizi ya madawa hayo huwa bado yanaendelea.Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba fedha za ruzuku zinatolewa mapema iwezekanavyo kuwawezesha wakulima kupata salfa kwa wakati naofaa.

(c) Serikali haichagui wakala wa kupeleka salfa mkoani Mtwara. Inachofanya ni kuingia mkataba na wasambazaji wa madawa ya Korosho wote wenye madawa yaliyofanyiwa uchunguzi na majaribio na vituo vya Serikali vyenye majukumu hayo vya *TPRI* na *ARI* Naliendele na kuwaorodhesha wasambazaji hao. Katika msimu wa 2008/2009 makampuni matano yalisajiliwa kusambaza salfa ili kumpa mkulima fursa ya kutosha ya kuchagua dawa itakayomfaa mara anapohitaji. Makampuni hayo ni:-

(i) *Abbasi Export*
Aina ya dawa: *Palm Brand Sulfur Dust*

(ii) *Suba Agro Trading & Engineering Co. Ltd.*
Aina ya dawa: *Kumulus DF.*

(iii) *Export Trading Co. Ltd.*
Aina ya dawa: *Falcon Sulfur Dust*

(iv) *MRAITF*
Aina ya dawa: *Palm Brand Sulfur Dust.*

(v) *Tanzania Fertilizer Co. Ltd.*
Aina ya dawa: Salfa ya Unga.

**MHE. JUMA A. NJWAYO**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyogeza.Kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba fedha za ruzuku zinapelekwa kwenye *CBT* mwezi wa sita na wa saba, jambo hili limekuwa linasababisha kuchelewa sana kufika kwa madawa kwenye maeneo ya korosho na ninao mfano msimu wa mwaka jana zilifika mwezi Desemba na *January.* Je ili kurekebisha hali hiyo wanaweza sasa wakaanza kupeleka pesa kuanzia mwezi wa tatu au wa nne tuwahi msimu na tuwasaidie wakulima mapema?

(b) Kituo cha Naliendele kimekuwa kikichangia ufanisi sana wa maendeleo ya zao la korosho, karanga, ufuta na mazao mengine. Lakini liko tatizo kwamba Bajeti wanayotengewa ni ndogo na hii si kwa AliNaliendele tu pamoja na vituo vingine vya utafiti vya kilimo vilivyopo nchini, tukumbuke kwamba mwaka huu tumepitia azimio kwamba kilimo kwanza. Je, uko mpango wa Serikali wa kusaidia vituo hivi vya Utafiti ili viweze ku-*perform* kama inavyotarajiwa kwa kuwasaidia wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi nimesema Serikali inaendelea kufanya utaratibu kwa kuhakikisha kwamba pembejeo zote sio salfa tu zinawafikia wakulima kwa wakati. Na kwa hivyo yanapotokea matatizo haya ya kuchelewachelewa basi kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunajitahidi tunayarekebisa kama mlivyoona hata kwenye mbolea, tatizo hili lipo lakini tunachokifanya ni kwamba tatizo hili tunalikabili kwa kuharakisha pembejeo zimfikie mkulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwisha chukua hatua mbalimbali ikiwemo hatua ya kuhakikisha kwamba fedha zinatengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maeneo yale yote yanayolima korosho wanazipata kabla ya msimu.

Kwa mfano mwaka jana ilikuwa kwamba Halmashauri zingeshiriki au zingefanya zenyewe kuagiza lakini ikwa kwa bahati nzuri *CBT* tayari walikwisha jipanga kuagiza. Ikabidi waache lakini kwa mwaka huu 2009/2010 Serikali yenyewe tayari imekwisha tenga shilingi bilioni 1.6 kwa ajili hiyo hasa kwa ajili ya kuongeza ruzuku kwa madawa ya korosho kwa hizi fedha zitakwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Naliendele, Bajeti ni ndogo ni kweli na mimi nakiri kwamba mara nyingi tunapata matatizo hayo ni kutokana na ile fedha yenyewe ambayo Serikali inayo kwa wakati huo.

Lakini nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka juzi nakumbuka nikiwa Wizara ya Kilimo Serikali ilichukua hatua kubwa sana kuhakikisha kwamba zile fedha zote za michangomichango ambazo zilikuwa zinapeleka kwa wadau mbalimbali kwa mfano za *research* Serikali inazichukua yenyewe ili kupunguza mzigo ambao wananchi wangepata kawa hiyo hizo fedha sasa zinatolewa na Serikali kwa ajili ya vituo kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli Bajeti ni ndogo lakini tunaendelea kuchukua hatua kuongezea vituo hivi ili viweze kutoa mchango wake.

**MHE. SULEIMANI O.KUMCHAYA:** suala hili siyo mara ya kwanza kufika katika Bunge hili kuhusu ukiritimba wa kampuni moja kuuza salfa katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Na kila tunapojibiwa tunaambiwa kwamba tuna makampuni kadhaa kama

Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu, lakini ukienda kule unaikuta kampuni hiyo hiyo tu. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kujiridhisha kama kweli hizi kampuni ambazo zinatajawa zinafanya kazi hii ya kugawa salfa ama kuna jambo jingine ambalo halifahamiki linalosababisha wakulima wa korosho wapate taabu katika kupata salfa ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA):** Mimi nataka kwanza nimhakikishie nilikuwa Wizara hiyo ya Kilimo miaka michache iliyopita. *CBT* kwanza yenyewe kama *CBT* haifanyi kazi hiyo ya kuagiza ni makampuni haya ndio ambayo tumeyapa kazi ya kuagiza salfa hiyo, Serikali iko tayari kabisa na mara nyingi tuna kaa pamoja na wadau wote wanaolima korosho kuhakikisha kwamba tunapata muafaka ni nini kifanyike na hata sasa nataka nikubaliane naye kwamba bado utaratibu huu uko wazi wadau wa korosho mnayo nafasi kubwa kabisa kukaa na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kuangalia ni wapi kuna *blind spots* ili tuweze kurekebisha

Mheshimiwa Spika, sidhani kama tatizo kubwa labda ambalo Serikali inang'ag'ania kwamba huyu apeleke salfa na huyu asipeleke. Kama anazo sifa na kama kwa kupeleka salfa ile wale wadau wote au yale makampuni ambao waagizaji na watumiaji wanaona kwamba inafaa basi wakiletwa pale sidhani kama Serikali itakataa, tutaangalia ni wapi mradi tu salfa ile iwafikie wananchi wale kwa wakati naomba hili uendelee kulileta tu huo mjadala tuuzungumze mradi tufanye kabla ya msimu kuanza.

**SPIKA:** Kwa upendeleo swali fupi,unajua ni vigumu sana kumuona Mheshimiwa Vita Kawawa hata akisimama.kwa hiyo bahati mbaya sikumuona tu, swali la nyongeza .

**MHE. VITA R . KAWAWA**: Mheshimiwa Spika ahsante kwa kuniona na ufupi wangu, Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimwulize swali moja tu la nyongeza kwa kuwa katika Wilaya yetu ya Namtumbo tunalima pia korosho katika Tarafa ya Sasawala lakini huwa tunapata soko la korosho na pembejeo zake za salfa kupitia Wilaya ya Tunduru.

Tunashukuru lakini unasababisha sana ucheleweweshaji wa kupata hizo salafa na soko la korosho.

Je, Serikali inaweza kututambua na kutuweka katika utaratibu wa upatikanaji wa salfa hiyo ili salfa iwe inapitishwa katika Chama chetu cha Ushirika cha Sonamku?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA):** Sipendi kumwambia moja kwa moja kwamba sasa tayari nimekubali waagize moja kwa moja lakini ninachotaka kumhakikishia ni kwamba hatua yoyote ambayo inalenga kuboresha usambazaji wa pembejeo mazungumzo yanakubalika.

Mimi nafikiri ni juu ya Wilaya ya Namtumbo kama nilivyomjibu Mheshimiwa Kumchaya, kuhakikisha kwamba ina simama kidete kutuonyesha kwamba chama chao

cha Ushirika kinao Uwezo huo na kinaweza kufanya kazi hiyo ikasambaza salfa kwa wakulima wake. Hilo naomba niseme kwa niaba ya Serikali kwamba linaweza kuzungumzika tulipatie ufumbuzi

Na. 166

**Kuwezesha Kilimo – Mkoa wa Tabora**

**MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora una mabonde mengi mazuri ya Kilimo yenye rutuba na yanayojaa vipindi vyote vya mvua; na kawa kuwa mabonde hayo hayalimwi kutokana na na uwezo mdogo wa wananchi hivyo maji hayo hupotea bure tu; na kawa kuwa, kila mwaka Mkoa wa Tabora hukumbwa na balaa la njaa:-

Je, Serikali ina mpango gani maalum wa kuwezesha kilimo katika Mkoa huo kwa kuupatia zana za kilimo, pembejeo za kutosha na huduma za ugani ili mabonde hayo yenye rutuba yaweze kulimwa na kuzalisha chakula cha kutosha na ziada kwa ajili ya kulinda uchumi wa Mkoa huo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** ) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa Mkoa wa Tabora katika uzalishaji wa mazao ya chakula, hususani mahindi na mpunga, kwa kujumuisha baadhi ya Wilaya Mkoani humo katika mpango wa ruzuku ya pembejeo. Mwaka 2008/2009, Wilaya ya Sikonge ilinufaika kwa Ruzuku ya pembejeo za kilimo zikiwemo mbolea na mbegu bora za mahindi kwa utaratibu wa *vocha.*

Mheshimiwa Spika, Aidha mwaka 2009/2010 Wilaya ya urambo itaongezwa katika mpango wa ruzuku kwa kupewa vocha kwa ajili ya mbegu bora za mpunga. Kuhusu kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa huo, skim 21 zenye jumla ya hekta 5,145 zimekamilika na katika msimu wa 2008/2009 zimezalisha tani 22,908 za mpunga. Katika mwaka wa 2009/2010 skim saba mpya zitajengwa na *skim 3* zitafanyiwa ukarabati; *skim* hizo zina jumla ya hekta 2,214 na zinatarajia kuchangia uzalishaji wa mpunga kiasi cha tani 28,125. Kutokana na uwekezaji huo, Mkoa wa Tabora mwaka 2008/2009, umeweza kuzalisha tani 600,380 za chakula na kuweza kutosheleza mahitaji ya chakula ya Mkoa ambayo tani 531,681 kwa mwaka, kwa hiyo kuwa na ziada ya tani 68,699.

Kuhusu kuendeleza matumizi ya matrekta madogo ya mkono yaani *power tillers*, tayari Halmashauri za Wilaya Mkoani humo zimeona umuhimu wa kuongeza matumizi ya zana hizo na zimepanga kununua *power tillers* 36 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika inaendelea kutekeleza mpango wa kuimarisha huduma za ugani . Kupitia mpango huo watafundishwa na kuajiriwa wataalamu wa Kilimo 11, 703 ifikapo mwaka 2012/13. Mwaka 2008/2009 wataalam 3,078 wameendelea kupatiwa mafunzo katika vyuo vya kilimo vya Wizara.

Baada ya kuhitimu wataajiriwa na kupelekwa katika Halmashauri za Wilaya nchini na Mkoa wa Tabora utapewa kipaumbele katika mgao huo.Aidha katika Mwaka 2008/2009 Mkoa wa Tabora umepokea wataalam 8 waliohitimu shahada ya kilimo na wamepangiwa vituo katika Wilaya za Sikonge, Nzega na Manispaa ya Tabora .

**MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA**: Kwa kuwa Mkoa wa Tabora bado uko nyuma kimaendeleo na kwasababu hiyo hata Wilaya zake, Halmashauri zake uwezo wake ni mdogo. Na mara kwa mara tumekuwa tunapanga tuweze kupata zana kwa kutegemea uwezo wa Halmashauri lakini inashindikana.

Je, Serikali kwa kuzingati mchango wa Mkoa wa Tabora katika pato la Taifa hasa kwa kupitia zao la tumbaku haioni umuhimu sasa angalau wa kununua trekta ishirini tu kwa Mkoa wa Tabora ili tuweze kuzalisha kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA**: Kwanza nataka nikubaliane na Mheshimiwa Sakaya kwamba Mkoa wa Tabora kwa kweli uko nyuma katika matumizi ya zana. Kama nina taarifa sahihi Mkoa mzima matrekta mazuri yanayofanya kazi kwa maana katika ule ni matatu.

Kwa kweli iko haja ya kuongeza nguvu hiyo, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Sakaya kwamba Serikali sasa imeongeza nguvu katika upatikanaji wa Pembejeo.

Mheshimiwa Spika, nitajibu tu kwa kifupi kwa mifano iliyopo kwamba mfuko wetu wa pembejeo ambao ndio unatoa mikopo ya kununua zana za kilimo zikiwemo hizo *power tillers* na matrekta makubwa.

Umeongezewa fedha mwaka huu na Waziri wa Kilimo atakaposoma Bajeti yake lazima mtasikia hilo lengo ni kuhakikisha wananchi wanaotumia mfuko huo kupata zana hizi, na mimi nataka niwashauri ndugu zangu wote kwa Mkoa wa Tabora zikiwemo Halmshauri nazo zisimame kidete kusaidia wananchi angalau hata kuwadhamini pale ambapo wanahitaji kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, kalini pia Mheshimiwa Rais alipokuwa akitutangazia pale Kilimani kama utakumbuka alizungumzia sana suala hili kwasasababu alisema katika zile mbinu za kujikomboa na mtikisiko huu wa fedha na uchumi Duniani.

Tunatarajia kutumia dola milioni 40, na fedha hizi zitaelekezwa katika Kilimo, katika mfuko wa pembejeo, katika kuagiza matrekta na tulifika mahali tukasema matrekta haya yataagizwa na katika kupunguza gharama tutatumia vikosi vyetu hata vya majeshi kama JKT na NYUMBU ku –*assemble* hizi *tractor* lengo ni kuhakikisha haya ma -*trector* yanapelekwa katika Mikoa ambayo haina na Tabora itakuwa mmoja wapo .

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumebanwa na muda naomba twende sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na 167

**Uhaba Wa Vitendea Kazi Katika Jeshi La Polisi**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (K.n.y. MOHAMED ALI SAID)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Bukombe hapo tarehe 30/4/09 katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge nilikiri kuwa jeshi letu la polisi lina uhaba wa vitendea kazi.

Je, ikiwa jeshi letu litashindwa kukabiliana na vitendo vya uhalifu , Serikali haioni kuwa usalama wa raia wake utakuwa hatarini hivyo ione umuhimu wa kuwapatia vitendea kazi bora vya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wakati nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Bukombe hapo tarehe 30 Aprili, 2009 nilieleza kuwa jeshi la polisi linakabiliwa na uhaba wa Vitendea kazi mbalimbali . Hata hivyo napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba uhaba huo hauwezi kusababisha jeshi kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kulinda Usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa uwezo wa Bajeti yetu ya Serikali, vipaumbele tulivyonavyo na changamoto zinazokabili Serikali katika kuwahudumia wananchi wake. Hivyo jeshi la Polisi litaendelea kupatiwa vitendea kazi vya kisasa na kuboresha hali ya maisha ya askari wetu kadri Bajeti ya Serikali itakavyoruhusu. Aidha kwa rasilimali chache zilizopo, Jeshi hilo litaendelea kujiimarisha kwa kutumia mbinu na mikakati

mbalimbali ya kipolisi, kiintelijensia na kupitia dhana ya polisi Jamii na Ulinzi shirikishi.

Mheshimiwa Spika, jukumu la ulinzi wa usalama wetu na mali zetu ni letu sote. Hivyo pamoja na changamoto tulizonazo tukishirikiana kwa dhati hakika tutafanikiwa kupambana na uhalifu hapa nchini

**MHE. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:** Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema pamoja na uhaba wa vitendea kazi analihakikishia Bunge lako Tukufu kwamaba halitoshindwa kulinda usalama wa Raia na mali zao. *(Makofi)*

Je, ni kwa nini basi kuna matukio mengi sana ambayo yameripotiwa na jeshi hilo limeshindwa kuwakamata wahalifu zaidi kuliko wale wanaopatikana pamoja na taarifa na msaada unaotolewa na wananchi?

(b)Kwa kuwa ujasiri wa kuwakamata wahalifu hautegemei vitendea kazi pekee inategemea pia ujasiri wa jeshi hilo pamoja na mafunzo ya kiupelelezi wanaoyapata wananchi. Na kwa kuwa mafunzo hayo wanayapata askari wa ngazi za juu tu.

Je, Mheshimiwa Waziri atalihakikishia Bunge lako Tukufu vipi kwamba sasa askari wa ngazi za chini ambao wanajumuika na wananchi watapata mafunzo ya kiupelelezi ili waweze kulisaidia Jeshi la polisi katika kuwakamata wahalifu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, maswali mawili aliyouliza Mheshimiwa Mnyaa, ningeomba asionekane kwamba ana uhakika na kile ambacho amekisema hapa Bungeni. Kwasasababu kwa mfano anavyosema kwamba yamekuwepo matukio mengi ambayo yameripotiwa lakini jeshi la polisi limeshindwa kuwakamata hata hao wahalifu, naomba nitamke hapa rasmi katika Bunge lako kwamba hiyo kauli si kweli na kama nilivyosema katika jibu langu la msingi suala la Ulinzi katika Taifa letu na Usalama wa raia na mali zao haliwezi likawa la vyombo peke yake linataka tushirikiane kati ya vyombo na wananchi husika.

Mheshimiwa Spika, na ndio maana tumekuja na hii dhana ambayo ni *philosophy* ya kusema kwamba lazima tuwe na polisi jamii na ulinzi shirikishi yaani wote kwa pamoja. Inatokea kweli pahala pengine tunakwama kwa sababu hatupati taarifa zilizokuwa sahihi na pahala pengine hatupati ushirikiano uliokuwa sahihi, na hii naisema na wananchi wanaona na kitu ambacho tumekuwa tunaomba na tunazidi kuomba katika kujibu suala lako Mheshimiwa Mnyaa kwa kweli tupate ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi na pale ambapo tunapata hakika jeshi la polisi limekuwa linafanya kazi yake hiyokwa usahihi na kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kuzungumzia juu ya ujasiri. Hakika tuna vikosi maalumu tumekwenda kila mahali ambapo kumetokea matatizo kuna vikosi ambavyo anaviongoza kamanda wetu Tosi, ambaye amepata heshima kubwa hapa Nchini. Na kwa kweli vitendo vya uhalifu watu wanavyozidi kuongezeka nchini, na mambo ya

utandawazi yanavyozidi kuongezeka nchini kweli siyo hapa Tanzania peke yake, ni katika nchi zote Duniani.

Kwa kweli zinakabiliwa na matatizo lakini kwa kweli jeshi letu la polisi na uhaba wa vitendea kazi tumekuwa kwa kweli mstari wa mbele katika kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, ningependa niongeze tu kuwa niwashukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama wamejitahidi sana na hilo wameliona. Na kwa kweli wamekuwa wanasema hata ngazi za juu kwamba jeshi la polisi liongezewe vitendea kazi.

Na. 168

**Ajali za Barabarani /Majini**

**MHE. MASOUD ABADALA SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, ajali za barabarani na baharini zimekuwa zikisababisha watu wengi kufariki dunia,wengine kujeruhiwa na kupoteza mali zao:-

Je,ni watu wangapi waliojeruhiwa kwenye ajali kuanzia Januari 2009 hadi Juni 2009 kwa kuonyesha mchanganuo wa ajali za barabarani na baharini katika kila mwezi kwa kipindi hicho.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abadallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu za majeruhi wa wa ajali za barabarani kwa kipindi cha Januari ,2009 mpaka tarehe 31 mei ,2009 ni kama ifuatavyo:-

| **MWEZI** | **WALIOJERUHIWA** |
|---|---|
| JANUARI, 2009 | I,530 |
| FEBRUARY, 2009 | 1,450 |
| MACHI 2009 | 1,786 |

| | |
|---|---|
| APRIL 2009 | 1,528 |
| MEI | 1,378 |
| **JUMLA YA MAJERUHI** | **7,672** |

Mheshimiwa Spika, majeruhi wa ajali za majini kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

| **MWEZI** | **WALIOJERUHIWA** |
|---|---|
| JANUARY 2009 | HAKUNA |
| FEBRUARI 2009 | 2 |
| MACHI 2009 | HAKUNA |
| APRILI 2009 | 5 |
| MEI 2009 | 28 |
| **JUMLA YA MAJERUHI** | **35** |

Mheshimiwa Spika, takwimu za mwezi Juni, 2009 hazijawa tayari kwa matumizi rasmi.

**MHE. MASOUD ABADALA SALIM**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nina maswali mawili ya nyongeza kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Katika kupunguza ajali, je Jeshi la Polisi ina mpango gani wa ziada kwa kushirikiana na *SUMATRA*, *TRA*, Shirika la Viwango, Wizara ya Miundombinu katika kuwabaini madereva ambao wanaendesha magari kwa mwendo wa kasi na wengine wakiwa wamelewa?

Mheshimiwa Spika, la pili, je, polisi ina mpango gani wa kutafuta boti nyingine kubwa za doria ili kukabiliana na ajali wakati imetokea ndani ya bahari au kwenye Maziwa?

**SPIKA:**Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA MAMBO YA NDANI YA NCHI** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwa kweli changamoto kubwa tuliyonayo upande wetu sisi kama polisi, hasa kikosi cha usalama barabarani. Ni

hili swala la madereva; zipo Sheria na tunajaribu kuwekea mkazo upande wa Sheria, lakini pia niseme kwamba tunahitaji ushirikiano mkubwa wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wapo watu wanagushi hizi leseni na jamii inajua. Wako watu katika mabasi haya wanakwenda kasi sana na watu wengine wanataka kweli waende kasi sana. Kwa hiyo, tutajitahidi kama nilivyosema katika maswala mengine. Upande wa ku-*enforce*, kusimamia zile Sheria lakini, tunataka ushirikiano mkubwa.

Kwa mfano gari linapokwenda vibaya, hapana mbaya abiria huweza kupiga simu polisi kusema tunakwenda tumo katika gari lakini hili gari, huyu dereva anaonekana anakwenda vibaya. Haya hayafanyiki.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengine tunasema kwamba jamii wenyewe wanajua kwamba watu wengine, hawana leseni, watu wengine wana leseni za kughushi, na kadhalika. Kwa hiyo, mimi ninachozungumzia hapa ningeomba tupate ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa wananchi ili tuweze kuhakikisha kwamba Sheria inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajali za majini. Kwa kweli nataka niseme, kwamba tunao uhaba wa vitendea kazi na hili linajulikana katika Kamati nilivyosema haya mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, wamelizungumzia, na Mheshimiwa Masoud aliye uliza swala hili, nashukuru kwamba ni mmoja wapo wa wajumbe wa Kamati hiyo na analifahamu vizuri na tunasema alikuwa analisemea vizuri; naomba uendelee kulisemea ili tupate vitendea kazi tuhakikishe kwamba doria katika bahari na katika Maziwa inatekelezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaelekea sasa Wizara ya Fedha na Uchumi. Muda wa maswali umefika, ukomo wa maswali, lakini kama mnavyokumbuka kulikuwa na taarifa nyingi sana za kuwasilishwa. Kwa hiyo, tutaibia dakika tano hivi au isiyozidi kumi ili tumalize haya ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi wa Musoma Mjini.

Na. 169

**Malipo ya Bima za Maisha**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Sheria za Nchi yetu, bima ya Mtu inapoiva (Bima ya Maisha) ndani ya miezi sita mwenye bima anapaswa kuwa amelipwa:-

(a) Je, zipo bima ngapi zilizoiva na hazijalipwa kwa kipindi kinachozidi miezi sita?

(b) Je, mteja akifariki kabla hajalipwa bima yake iliyoiva atalipwaje?

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE – NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, idadi ya bima zilizoiva na hazijalipwa kwa kipindi kinachozidi miezi sita kwa mujibu wa taarifa hadi kufikia tarehe 31/12/2008 ni 43,797.

(b) Mheshimiwa Spika, mteja wa bima iliyoiva kama atafariki kabla ya kulipwa bima yake, utaratibu uliopo ni kwa warithi wake ndiyo hulipwa bima hiyo na Kampuni ya Bima husika baada ya msimamizi wa mirathi kuwasilisha taarifa zifuatazo:-

(i) Hati halali ya usimamizi wa mirathi iliyotolewa na Mahakama;

(ii) Hati halisi ya bima aliyopewa mteja (Marehemu) wakati anakata bima yake;

(iii) Cheti cha kifo cha Marehemu;

(iv) Taarifa ya Daktari au Mwenyekiti wa kijiji au kitongoji, inayoelezea mazingira ya kifo cha Marehemu;

(v) Hati ya uthibitisho wa umri wa mteja alipofariki dunia; na

(vi) Taarifa binafsi ya msimamizi wa mirathi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba, idadi ya bima zilizoiva na ambazo hazijalipwa ni kubwa kufikia 43,797; je, ni fedha kiasi gani zinazotakiwa kulipwa kutokana na hizo bima zilizoiva?

(b) Kwa kuwa, mtu anategemea kwamba, bima yake ikishaiva ndani ya kipindi cha miezi sita tayari awe ameshalipwa, ili fedha hizo aweze kuzitumia kwa matumizi mengine, lakini kwa bahati mbaya sana muda mrefu unapita pasipo kulipwa, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kila baada ya miezi sita inapofika fedha hizo zinaweza kulipwa ili mteja huyo aweze kuendelea na shughuli zake?

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE – NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha ambacho zinapaswa kulipwa kwa bima zote zilizoiva ni shilingi bilioni tisa.

Mheshimiwa Spika, nadhani Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka katika Sheria ya Bima tuliyoipitisha mwezi wa April mwaka huu, sheria hii sasa inazungumzia wazi kwamba, bima ikiiva katika kipindi cha siku thelathini inatakiwa ilipwe, kwa hivyo hakuna tena ule mtiririko wa miezi sita.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, katika jawabu la Waziri amekiri kwamba, kuna kundi kubwa sana la watu ambalo halijalipwa bima ambazo tayari zimeiva na kwa kuwa, suala la bima ni mkataba na kwa kwa sababu kuna watu ambao wana miaka mingi hawajalipwa bima zao zilizoiva, je, Serikali sasa iko tayari kuwalipa watu hao pamoja na *interest* kwa sababu mmewacheleweshea pesa zao ambazo walitegemea kuzitumia. (*Makofi*)

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE – NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima ambayo tumeipitisha mwezi April mwaka huu na Bunge lako Tukufu kuiridhia, haina kifungu cha kulipa na riba. Kwa maana hiyo, sheria ndiyo itakayoongoza malipo hayo. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hakutakuwa na malipo na riba.

Na. 170

**Ushuru wa Mafuta na Geita Gold Mines**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, *Geita Gold Mines* inaingiza nchini mafuta zaidi ya lita milioni saba kwa mwaka:-

Je, ni ushuru kiasi gani *Geita Gold Mines* inatozwa kwa kiasi hicho kwa mafuta?

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE – NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Jimbo la Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) namba 99 la tarehe 11 April, 2005 ambalo limeelekeza kuwa, kampuni iliyopewa leseni ya kuchimba madini ya dhahabu nchini na ambayo imetiliana mkataba wa uchimbaji na Serikali *(Mining Development Agreement),* wakati inapoingiza mafuta nchini kwa matumizi yake ya

uchimbaji wa dhahabu, kampuni hiyo itatozwa ushuru wa barabara na mafuta *(the road and fuel tolls*) wa dola za Kimarekani laki mbili USD 200,000/= kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tangazo hilo, kampuni ya *Geita Gold Mines* ambayo ni miongoni mwaka makampuni hayo, tokea mwaka 2006 imelipa ushuru huo jumla ya shilingi 760,915,620/= ikiwa ni ushuru wa barabara na mafuta. Fedha hizo zimelipwa kwa mpango ufuatao:-

- Mwaka 2006 - Tsh. 258,016,620/=
- Mwaka 2007 - Tsh. 229,199,000/=
- Mwaka 2008 - Tsh. 273,700,000/=

Jumla ni Tsh 760,915,620/=

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu ya Waziri, nina maswali madogo mawili ya kumuuliza:-

(a) Kwa kuwa, kiwango cha ushuru wanachotozwa *Geita Gold Mines,* hakilingani na wingi wa mafuta wanayoingiza nchini, je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Serikali kutoza kiwango hicho kidogo cha ushuru?

(b) Kwa kuwa, imebainika leo kuwa ushuru unaotozwa *GGM* ni kidogo sana na hii ni kutokana na upungufu uliopo kwenye Sheria za Madini zilizopo sasa, je, ni lini Serikali itaileta Sheria ya Madini hapa Bungeni kufanyiwa marekebisho ili pamoja na mambo mengine tupate kuongeza kiwango cha ushuru?

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE – NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi ambayo Serikali ilitoa kiwango hicho ni kutokana na kwamba, ile kazi ya uchimbaji wa madini tuliiona hapo awali ina gharama kubwa na sisi kama Serikali hatukuwa na hisa katika kampuni hizo, kwa hiyo Serikali ikahisi kwamba, ni vema msaada wetu uwe kuweka kiwango kidogo cha ushuru wa mafuta ili wenzetu waweze kuchimba madini yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nataka nikiri kwamba, hali hiyo sasa hivi inaangaliwa kufuatia ripoti ya Jaji Bomani na hatimaye tunaweza tukafikia mahali pazuri zaidi na wenzetu hawa wachimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua ni lini Sheria ya Madini italetwa hapa Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho. Nataka nilieleze Bunge lako kwamba, lengo letu ilikuwa kuileta Sheria ya Madini kufanyiwa marekebisho lakini sisi sote ni mashahidi hiki kipindi cha bajeti *programme* iko *very tight.* Kwa maana hiyo, tunatarajia kama mipango itakwenda vizuri, katika Bunge lijalo tunatarajia kuileta ili tuweze kuifanyia marekebisho au kuiangalia upya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umeshapita, sasa ni matangazo. Kama kawaida yetu tunaanza na wageni wetu.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nitaanza na wanafamilia ingawa Waziri hakutaja wanamhusu vipi, lakini nitatangaza tu ni wanafamilia. Kwanza ni Ndugu Mariam Mwinyi, naomba asimame, Ndugu Jamila Mwinyi na Ndugu Tarik Mwinyi, karibuni sana kuja kumshuhudia nadhani Baba ninavyowaona ninyi. Yupo na mkewe pia asimame. Unajua unapokosea umri wa Mwanamke ukamfanya ni mdogo, yote inakuwa ni faraja ni furaha, ahsante sana na samahani. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo watendaji wakuu wa Wizara ambao ni Jenerali Davis Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, karibu sana Jenerali tunafurahi mara kwa mara tunapoweza kuwaona hapa. Wabunge wanalipenda sana Jeshi lao kama Watanzania wote wanavyolipenda. Lina historia iliyotukuka kabisa. Hakuna watu wowote katika mipaka inayotukaribia wenye Jeshi ambalo limekuwa na historia iliyotukuka kama letu, tunafurahi sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo ndugu Andrew Nyumayo, Katibu Mkuu wa Wizara, yupo pia Luteni Jenerali, Abrahamani Shimbo, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Meja Jenerali Samwel Kitundu, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kuwa wapo na wapiganaji wengine ambao sikuorodheshewa hapa, ningeomba waliopo *Speakers Gallery* wasimame tuweze kuwatambua, Makamanda wa vikosi mbalimbali karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kwa makofi hayo, mnashuhudia jinsi Wawakilishi wa wananchi wanavyolipenda Jeshi letu, kwa sababu ya rekodi yake. *(Makofi)*

Lakini naona mkono wangu wa kulia maana hawa jamaa zetu huwa wanakwenda kwa vyeo, sasa hawa nao waliopo kulia sijui ndiyo Mameja na Makapteni, basi vyovyote vile, naomba pia msimame. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawaona pia watendaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nashukuru sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Emmanuel Nchimbi, ambaye ni Alexander Nchimbi, Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Tanzania, ahsante sana. Tunajivunia muda mrefu umefanya shughuli za umoja wa vijana, nadhani unafuata nyayo za Kaka yako, kwa hiyo tunakutakia kheri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Mheshimiwa Harith Mwapachu, Mbunge wa Tanga Mjini, ambao ni Wanakwaya arobaini (40) wa kikundi cha Amani kutoka Kanisa la Anglikana, Mkoa wa Tanga. Kikundi kinaongozwa na Charles

Ndunguru. Naomba Wanakwaya wasimame. Ahsanteni sana. Nafurahi zaidi kuwatambulisha kwa sababu kwaya hii ipo hapa kuendeleza kampeni ya utunzaji wa mazingira na pia mapambano ya kupiga vita mauaji ya walemavu wa ngozi, ahsante sana. Tunajivunia kwaya zetu zinapokuwa zinaingia katika masuala muhimu ya kijamii na kuhamasisha kwamba, maovu haya yaweze kukomeshwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mbunge wa Muheza ambao ni viongozi wa Chama Tawala na Serikali za Vijiji. Wako kumi na tatu, tafadhali wasimame, ahsanteni sana. Mwaka jana walipokuja viongozi kutoka Muheza, niliweza kupata machungwa kutoka Muheza, natumaini safari hii pia utamaduni huo unaendelea Mheshimiwa Mtangi. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, ambao ni jumla ya Walimu 25 kutoka Shule ya St. Mary ya Moshi Mjini. Kwa taarifa yenu, Waheshimiwa Wabunge, shule hii katika mitihani ya Kidato cha Nne, wamekuwa na historia ya kuwa katika kumi bora tangu mwaka 2004 hadi sasa. Ahsante sana Walimu wa St. Mary, huo ni ushindi mzuri sana. Natumaini wajukuu wangu wananisikiliza ili baadaye niweze kuwapeleka katika shule nzuri kama hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, msanii maarufu wa nyimbo za Injili, Bi Hellen Juma Njama. Karibu sana, tunakutakia mema katika kazi yako yenye kheri kwa binadamu na baraka kwa Mungu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Clemence Lyamba ambao ni wanafunzi 64 na Walimu 8 kutoka Shule ya Msingi Kantui, iliyopo Kidatu. Sidhani kama wamepata nafasi, inawezekana wapo katika *basement*. Ahsanteni na huo ndiyo mwisho wa wageni.

Kuna tangazo moja tu la kazi zetu, Mheshimiwa Hassan Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, leo saa saba mchana, Wajumbe wote wa Kamati mkutane katika ukumbi namba 227.

Huo ndio mwisho wa matangazo, Katibu kwa hatua inayofuata.

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WAWILI WA TUME YA UTUMISHI WA BUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia awali, kutokana na mabadiliko ya Tume ya Utumishi wa Bunge, tulikuwa na nafasi tatu, moja kwa mujibu wa sheria ni kiongozi wa Kambi ya Upinzani, anaingia kwa wadhifa wake kwa hiyo nafasi hiyo haipigiwi kura, mbili ni Wabunge wanawake wawili, mmoja kutoka Kambi ya Upinzani na mmoja kutoka Chama Tawala.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea hapa jina moja moja tu kutoka sehemu zote mbili, kwenye Chama Tawala na Kambi ya Upinzani. Kwa mujibu wa utamaduni wetu, tunapopata jina moja moja, wajibu wangu ni kuwatangaza hao basi mambo yamekwisha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kutoka Chama Tawala, nafurahi kumtangaza Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe ameshinda, hongera sana, tunakukaribisha katika Tume. Hivi ni moja ya vikao muhimu sana vya Mheshimiwa Spika, kwa sababu ndiyo inasimamia namna ambavyo sura ya Bunge itakavyokuwa kwa miaka kadhaa ijayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kutoka Kambi ya Upinzani tumepokea jina la Mheshimiwa Magdalena Sakaya. (*Makofi*)

*(Hapa Mhe. Anna Maulidah Komu alisimama)*

**SPIKA:** Mbona umesimama, mimi ndilo jina nililopewa, sema umesimama kuhusu utaratibu au?

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba, hata mimi nilipeleka fomu yangu, nashangaa limekuja jina moja, jina langu limekwenda wapi?

**NDG. JOHN JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, tarehe 3/7/2009, nilileta taarifa Bungeni ya kuonyesha jinsi ambavyo nimepokea majina, moja hadi saa kumi jioni. Kwa hiyo, sikupata jina la Mheshimiwa Komu, kama ambavyo anasema.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mhehsimiwa Spika, siyo sawa kwa sababu nilipeleka fomu yangu siku saba ama kumi zilizopita, sasa nashangaa kuambiwa kwamba, hiyo fomu haijapokelewa. Nilimkabidhi Katibu wa Katibu, walikuwa wawili, mwanaume na mama kakaa huku na nikaikabidhi fomu yangu, sasa ninapoambiwa kwamba, fomu hiyo haijafika mikononi mwa Katibu, nashangaa sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni hivi, sasa naelewa tatizo lilivyotokea. Takribani kama siku chache tu, sisi kufika hapa, tulitoa tangazo, likawa ni fupi mno na tukapokea malalamiko kwamba, halikutenda haki. Mtakumbuka nilisimama hapa na *Hansard* zitaonyesha, tukatoa tarehe mpya ndiyo hiyo tarehe 3/7/2009. Kwa hiyo, kwa namna uchaguzi ulivyo, kama wagombea hawakufuata tarehe ambayo inahusika basi haiwezekani, kwa sababu *nomination day* ikibadilishwa ni lazima ifuatwe. *(Makofi)*

**MHE ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, siku uliposimama, siwezi kukubali...

**SPIKA:** Mheshimiwa sikiliza, mimi nikisimama wewe huruhusiwi kusimama, ndiyo Kanuni zinavyosema, kwa hiyo jambo hili limekwisha na matokeo ndiyo hayo. *(Makofi)*

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, hapana, huu ni uonevu kwa kweli, kwa sababu siku umetangaza hapa nimekwenda kuwauliza fomu yangu ipo, wakaniambia wanayo, sasa unaponiambia hivyo kwa kweli naona huzuni kubwa sana. Siku umetangaza mara ya pili, nimekwenda kuwauliza fomu yangu ipo wakasema fomu ipo sasa huu ni uonevu. Kwa kweli nitakubali tu kwa sababu ya kauli yako lakini nitaendelea kusononeka kwamba, mmenionea.

**SPIKA:** Katibu, ni nani alithibitisha kwamba, ameipokea na akasema ile ile ya zamani iendelee?

**NDG. JOHN JOEL - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, tangazo liko wazi, mwisho kabisa wa tangazo lilisomeka kwamba, Waheshimiwa Wabunge, waliochukua fomu za Tangazo la Awali, wanaombwa kuchukua upya fomu. Kwa hiyo, alitakiwa achukue fomu upya na hakuna aliyethibitisha kwamba, amechukua fomu.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, nitaendelea kuweka msimamo wangu pale pale kwamba, baada ya kwenda kuulizia kwamba, fomu yangu ipo? Niliambiwa ipo na sikuambiwa kwamba, nichukue fomu nyingine. Kwa hiyo, mimi siwezi kuwa Malaika kujua kwamba, kuna fomu nyingine inachukuliwa wakati niliwauliza wahusika wakasema fomu inaendelea ile ile.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nisipoheshimu *Returning Officer*, maana ndiyo utaratibu, ushahidi tunaupata kutoka kwa anayepokea fomu, hakuna lingine unaweza ukafanya katika uchaguzi. Ni kama mambo ya Tume ya Uchaguzi, Rais hawezi kuingilia Tume ya Uchaguzi ikishasema.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, sawa lakini nitaendelea kusoneneka kwamba, nimeonewa.

**SPIKA:** Pole sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge.

## HOJA ZA SERIKALI

### (Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 -Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, kwa kazi nzuri ya kuchambua mapendekezo na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali wakati wa

kupitia Randama ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mwaka 2009/2010. Napenda kueleza kwamba, Kamati hiyo imetoa mchango mkubwa katika kuboresha Makadirio haya ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumatano tarehe 29 Aprili, 2009 katika Kambi ya Jeshi la Wananchi ya Mbagala, Dar es Salaam, kulitokea ajali mbaya ya milipuko ya mabomu. Ajali hiyo, imesababisha vifo vya Watanzania wenzetu 27, watu zaidi ya 200 kujeruhiwa na nyumba za makazi zaidi 7,000 kubomolewa. Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Viongozi Wakuu wa Serikali na Jeshi, walitembelea eneo la ajali na pia hospitalini kuwafariji wahanga wa ajali hiyo. Aidha, Rais kwa niaba ya Serikali, alitoa tamko kuhusu ajali hiyo. Vile vile Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilitoa tamko na kutangaza hatua mbali mbali ambazo zilichukuliwa kufuatia ajali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Tume Maalum iliundwa na Serikali kufanya uchambuzi wa ajali ile ili kubaini chanzo chake, athari zilizopatikana na kushauri hatua za kuchukua. Tume hiyo imekwishamaliza kazi yake na kutoa taarifa yake, taratibu zinakamilishwa ili taarifa hiyo iweze kujadiliwa na Baraza la Mawaziri, na kufanyiwa maamuzi. Pamoja na hayo, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na kwa niaba yangu mwenyewe, kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa wahanga wa ajali hiyo, wakiwemo watu waliopoteza maisha, walioumia na waliopoteza mali zao. Tumesikitishwa sana kwa yote yaliyotokea na tunamwomba Mwenyezi Mungu Azilaze Mahali Pema Peponi Roho za Marehemu na awajalie uzima wa haraka, wote walioathirika kwa namna moja ama nyingine, kutokana na ajali hiyo. Amina.

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa vyombo vya ulinzi na usalama, mamlaka za kiraia hasa Idara ya Zima Moto, Hospitali ya Wilaya ya Temeke, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Shirika la Msalaba Mwekundu, kwa jinsi walivyokabiliana na kudhibiti hali ya mkanganyiko mkubwa uliotokea siku ya ajali na siku zilizofuata. Kazi waliyoifanya ilikuwa kubwa sana na kwa hakika iliweza kuepusha maafa makubwa zaidi kutokea. Napenda pia kuwashukuru viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na viongozi wa Wilaya ya Temeke na Serikali za Mitaa katika eneo la ajali, wahisani, wasamaria na wananchi wote kwa ujumla kwa misaada na ushirikiano walioutoa kwa wahanga kuanzia siku ya ajali hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Bunge lako Tukufu, lilipata misiba ya Marehemu Julius Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Faustin Kabuzi Rwilomba aliyekuwa Mbunge wa Busanda na Mbunge wa zamani wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, Marehemu Phares Kabuye. Napenda kutumia fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu hawa, sote tunawakumbuka marehemu hao kwa uhodari wao wa kazi na jinsi walivyokuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya wananchi walipokuwa hapa Bungeni na kwingineko. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu Mahali Pema Peponi. Amina

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa hotuba yake ya kina ambayo imeelezea mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2008/2009. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa hotuba zao walizokwishawasilisha na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Bunge lako lilipata Wabunge watatu wapya kufuatia kufanyika kwa chaguzi ndogo. Wabunge hao ni Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale Mbunge wa Mbeya Vijijini, na Mheshimiwa Lolensia J. M. Bukwimba, Mbunge wa Busanda. Wote nawapongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Nchi inayozungukwa na Nchi nyingine nane upande wa Kaskazini, Magharibi na Kusini na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki. Hivyo, mwenendo wa hali ya usalama katika nchi hizo na eneo hilo la bahari unatoa picha ya hali ya ulinzi na usalama katika mipaka ya nchi yetu. Mwenendo huo katika mwaka 2008/2009 uligubikwa na masuala makuu mawili ambayo ni baadhi ya nchi kuendelea kukabiliwa na migogoro na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, na baadhi ya nchi kutokuwa na uhusiano mzuri kutokana na kugombea umiliki wa maeneo ya ardhi, rasilimali na kushutumiana kwa kuhifadhi na wakati mwingine kusaidia vikundi vya waasi dhidi ya utawala/Serikali ya nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki watapata fursa ya kulielezea Bunge lako Tukufu kuhusu hali ilivyo katika nchi hizo na juhudi za Serikali ya Tanzania katika kusuluhisha migogoro na mapigano hayo. Lakini inatosha kueleza tu kwamba migogoro na mapigano hayo, hasa katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Somalia yamesababisha kuwepo wakimbizi, wahamiaji haramu, maharamia na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo, mambo ambayo yamekuwa yakihatarisha usalama wa mipaka ya nchi yetu na nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa hali hiyo, Jeshi la Wananchi limejizatiti ipasavyo kudhibiti ulinzi na usalama wa mipaka yetu na kwamba hali katika mipaka yote ya nchi kwa ujumla ni shwari. Matukio ya ujambazi wa kutumia silaha katika maeneo ya mipakani, hususan kwenye mpaka wetu na nchi ya Burundi yamepungua sana ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika miaka ya nyuma. Matukio machache yaliyotokea yameweza kudhibitiwa kwa ushirikiano wa Jeshi la Wananchi, Polisi na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama. Hali katika mpaka mmoja mmoja katika mwaka 2008/2009 ilikuwa ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka katika Bahari ya Hindi, hali kwa ujumla katika mpaka huu haijatengamaa kutokana na vitendo vya uharamia katika mwambao wa Bahari ya Hindi hususan kwenye Ghuba ya Aden na Pwani ya Afrika Mashariki vinavyofanywa na maharamia wa Kisomali. Katika kipindi cha mwaka huu hadi kufikia mwezi Mei, 2009 maharamia hao walishateka meli zipatazo 13.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuwepo ulinzi wa meli za Majeshi ya nchi za Ulaya kwenye eneo la Ghuba ya Aden, maharamia wamebadilisha mbinu sasa wanazifuata meli na kuziteka kwenye Bahari Kuu (kina kirefu) katika Bahari ya Hindi ambako meli za kivita hazipo. Meli za ulinzi zimeshindwa kudhibiti eneo lote la Bahari ya Hindi kutokana na ukubwa wa eneo la maji, hali inayotoa mwanya kwa maharamia kufanya vitendo vyao viovu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Jeshi la Wananchi, limeimarisha ulinzi kwa kufanya doria karibu na mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi pamoja na kusindikiza meli zinazoomba msaada huo. Aidha, ushirikiano na majeshi ya nchi za Afrika Kusini, Kenya na Msumbiji umesaidia kudhibiti hali katika mwambao huo. Changamoto iliyopo ni kuimarisha zaidi uwezo wa Kikosi cha Wanamaji cha Jeshi la Wananchi kufanya doria katika maji marefu ya Bahari ya Hindi ambako kwa sasa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, mpaka na nchi za Kenya na Uganda. Katika mpaka huu, hali kwa ujumla ni shwari isipokuwa suala la kuharibiwa kwa alama za mipaka (*beacons*) bado halijapatiwa ufumbuzi. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya na pia Serikali ya Uganda inaendelea na mazungumzo kulipatia ufumbuzi suala hili. Aidha, katika mipaka na nchi hizi lipo tatizo la ujenzi holela katika baadhi ya maeneo ya mipaka kwenye wilaya za Tarime na Maramba kwa upande wa mpaka na nchi ya Kenya na kwenye Wilaya ya Misenyi kwa upande wa mpaka na nchi ya Uganda.

Vile vile katika upande wa mpaka na nchi ya Kenya hali bado ni ya wasiwasi kutokana na kuwepo mapigano ya mara kwa mara kwa koo za Warenchoka, Wanchari na Wakira yanayosababishwa na kugombea ardhi na wizi wa mifugo kwa pande zote za mpaka. Hatua zinazochukuliwa kudhibiti hali hiyo ni pamoja na uongezaji wa idadi ya polisi, doria za Jeshi la Wananchi na uwezekano wa kuanzisha kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika eneo hilo ili kuweza kupunguza vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, mpaka na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*). Hali kwa upande wa mpaka na Rwanda ilikuwa shwari. Hata hivyo, kwa upande wa mpaka na Burundi, hali haikuwa salama sana kutokana na matukio ya ujambazi wa kutumia silaha yanayofanywa na raia wa Burundi kwa kushirikiana na raia wabaya wa Tanzania waishio mpakani. Hata hivyo, matukio ya ujambazi yamepungua ikilinganishwa na kipindi cha nyuma. Aidha, hali ya usalama wa mpaka kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni shwari licha ya kuwepo tahadhari mashariki mwa nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpaka na Nchi za Zambia, Malawi na Msumbiji. Hali ya usalama wa mpaka katika eneo hili ilikuwa shwari. Hakuna matukio ya uvunjifu wa amani yaliyoripotiwa ingawa kuna tatizo la ujenzi holela katika mji wa Tunduma kwenye mpaka na nchi ya Zambia.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 Kuhusu Ulinzi wa Nchi Kwa Mwaka 2008/2009. Dira ya Maendeleo ya

mwaka 2025 kuhusu ulinzi wa nchi inaelekeza kwamba amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao ni mazingira ya msingi na muhimu katika kujiletea maendeleo yetu. Kwa bahati nzuri Nchi yetu imekuwa na mazingira ya amani, utulivu na usalama toka tupate Uhuru mwaka 1961.

Hali hii imedumishwa na Serikali za awamu zote nne. Sifa hizi hapana budi zijengwe, zilelewe na ziendelezwe kama nguzo mojawapo muhimu za kujiondoa katika umaskini na kujiletea maendeleo endelevu. Changamoto kubwa mbele yetu ni kudumisha amani na utulivu uliojengwa kwa muda mrefu na kuboresha usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa msingi huo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imeilekeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na vyombo vingine vya dola kuimarisha ulinzi wa Nchi yetu dhidi ya adui kutoka nje kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuunda Jeshi dogo la Ulinzi wa nchi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa;

(b) Kulijengea Jeshi la Ulinzi mazingira mazuri ya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kutatua matatizo ya makazi na maslahi ya watumishi wake; na

(c) Kuendeleza ufufuaji wa mafunzo ya JKT kwa vijana wa Kitanzania ya kulinda na kujenga nchi, kuimarisha umoja wa kitaifa na kuwajenga vijana katika uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza maelekezo hayo ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 kwa kuyapa maeneo hayo kipaumbele katika bajeti za kila mwaka. Kutokana na hatua hiyo, Jeshi letu limeweza kuimarika kwa kupata zana, vifaa na vitendeakazi muhimu na hivyo kuliwezesha kutekeleza majukumu yake ya ulinzi wa mipaka yetu ipasavyo. Aidha, Wizara imefanikiwa kufufua mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa Kitanzania. Utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kila kipengele ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uundwaji wa Jeshi dogo la Ulinzi wa nchi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa. Katika mwaka 2008/2009 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelinunulia Jeshi la Wananchi vifaa na vitendeakazi ili kuliimarisha na kuliongezea uwezo katika kutekeleza majukumu yake, hususan kufanya doria za ulinzi wa mipaka na kusaidia kukabiliana na majanga na maafa pindi yanapojitokeza. Vifaa hivyo ni pamoja na magari na vipuri vyake ambayo yamepokelewa kama ilivyopangwa Baadhi ya vifaa hivyo vimepatikana kama misaada toka Serikali za nchi rafiki.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China chini ya ushirikiano wetu wa muda mrefu imelipatia Jeshi la Wananchi zana na vifaa mbalimbali vya kijeshi kuliongezea uwezo wake wa kiutendaji kivita. Serikali za Marekani na Uingereza zimelipatia Jeshi la Wananchi vifaa na vitendeakazi vingine kwa ajili ya kikundi

kitakachoshiriki operesheni ya Ulinzi wa Amani huko Darfur, Sudan. Naomba kuchukua fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi hizo kwa ushirikiano wao na jinsi wanavyoendelea kulisaidia Jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na ununuzi mpya wa vifaa, Jeshi limefanyia matengenezo zana na vifaa vyake vya zamani ili kuviongezea uwezo wa kutumika katika majukumu ya ulinzi wa nchi na majukumu mengine hapa nchini. Kila ilipowezekana, mashirika ya Wizara ya Mzinga na Nyumbu pamoja na karakana za Jeshi yametumika kutekeleza jukumu hili. Pamoja na ununuzi wa vifaa vipya vya kijeshi unaoendelea, Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa kuimarisha karakana za Jeshi kwa kuzifanyia ukarabati wa Karakana za Kanda pamoja na kutoa mafunzo kwa mafundi wake ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Utekelezaji wa mpango huo ni hatua muhimu kwa Jeshi la Wananchi kwa vile utapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa karakana za watu binafsi ambazo gharama zake ni kubwa sana. Karakana hizo zikiimarika, zitaweza kutoa huduma kwa magari na mitambo ya Wizara na Idara za Serikali na Mashirika ya Umma kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi kwa Wanajeshi. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeendelea na jukumu la kuwaendeleza na kuwajenga Wanajeshi katika taaluma zao, falsa ya ulinzi wa nchi, nidhamu, bidii ya kazi na uwajibikaji ili wawe na uwezo wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yao. Jeshi la Wananchi limewezeshwa kuwapatia Maafisa na Askari wake mafunzo yanayohusu taaluma zao katika Vyuo na Vikosi vya Jeshi hapa nchini. Aidha, Jeshi la Wananchi limewezeshwa kuboresha mazingira ya vyuo vyake ili viendane na wakati. Hii ikiwa ni pamoja na kuvipatia vifaa vya kisasa vya mafunzo, ukarabati wa majengo na miundombinu. Vile vile Serikali za nchi za Canada, India, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Ufaransa na Uingereza zimelipatia Jeshi la Wananchi nafasi za kozi mbalimbali za Kijeshi katika vyuo vyao vya kijeshi. Kwa mara nyingine tena, napenda kuzishukuru Serikali hizo kwa ushirikiano wao na misaada yao kwa Jeshi letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chini ya ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi wa Jumuiya za Kikanda za Nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jeshi la Wananchi pia limeshirikiana na majeshi ya jumuiya hizo katika maeneo ya mafunzo. Katika ushirikiano huo, Jeshi la Wananchi limepatiwa nafasi za mafunzo ya Ukamanda na Unadhimu katika vyuo vya kijeshi vya nchi hizo na Jeshi letu limetoa nafasi za mafunzo katika vyuo vyake kwa majeshi ya nchi hizo. Vile vile, chini ya ushirikiano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jeshi la Wananchi limetoa nafasi za mafunzo katika vyuo vyake vya "*Command and Staff College* na *Tanzania Military Academy* vilivyopo Monduli, Arusha kwa nchi za Afrika ya Kusini, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Botswana, Swaziland, Lesotho na Malawi. Aidha, Jeshi la Wananchi limepata nafasi za mafunzo ya Ukamanda na Unadhimu katika nchi za Afrika Kusini, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Jeshi la Wananchi pia limeendesha mazoezi kwa ajili ya Maafisa na Askari wake katika ngazi za Kombania, Vikosi na

*Brigade* ili kujinoa na kujiimarisha katika utayari wa kutekeleza majukumu ya kulinda nchi na majukumu mengine hapa nchini. Aidha, kwa lengo la kutekeleza majukumu ya kimataifa maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi wamefanya mazoezi ya Ulinzi wa Amani kujiandaa kushiriki katika operesheni mbali mbali katika nchi zenye migogoro duniani. Napenda kuchukua nafasi hii kuzishukuru Serikali za nchi za Canada, Marekani, Ufaransa na Uingereza kwa misaada inazotoa kwa jeshi letu ili liweze kutekeleza wajibu wake huo wa kimataifa. Napenda pia nichukue nafasi hii kuushukuru Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kwa kuwawezesha Wanajeshi wetu kushiriki kwa mafanikio katika operesheni za Ulinzi wa Amani huko *Comoro, Darfur, Ivory Coast, Lebanon* na Sudan ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika mwaka 2008/2009, Jeshi la Wananchi limeendelea kushirikiana katika mafunzo ya kijeshi na operesheni za pamoja na majeshi ya nchi za Jumuiya za Kikanda za Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Hivi sasa majeshi ya nchi za Ushirikiano wa Afrika Mashariki yanajiandaa kushiriki katika zoezi la medani linaloitwa "ZOEZI MLIMA KILIMANJARO" linalotarajiwa kufanyika nchini Tanzania katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Tanga mwezi Septemba, 2009. Zoezi hilo ni la kwanza na la aina yake kuandaliwa na kugharamiwa na majeshi ya nchi wanachama na litahusu ulinzi wa amani *(peace keeping operation)*, vita dhidi ya ugaidi *(counter terrorism)* na kukabiliana na maafa *(disaster management).*

Vile vile Majeshi hayo yanajiandaa kufanya zoezi la pamoja linaloitwa "*ZOEZI NATURAL FIRE*" kwa kushirikiana na Jeshi la Marekani litakalofanyika nchini Uganda mwezi Oktoba, 2009. Aidha, Jeshi la Wananchi na majeshi ya nchi nyingine za *SADC* yanajiandaa kushiriki katika zoezi la medani la *SADC* linalotarajiwa kufanyika nchini Afrika ya Kusini mwezi Septemba, 2009. Zoezi hilo limetanguliwa na mazoezi ya ramani *(MAP EXERCISES)* na vituo vya uamrishaji yaliyofanyika Angola na Msumbiji. Jeshi la Wananchi pia litashikiri katika ZOEZI GHOFINHO litakalofanyika mwezi Septemba 2009 ili kukamilisha uundaji wa Brigedi ya Kulinda Amani ya Nchi za *SADC*. Hali kadhalika Jeshi la Wananchi linajiandaa kupeleka Wakufunzi wa kijeshi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Mgambo kwa umma wa Watanzania. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Jeshi la Wananchi limetoa mafunzo ya ulinzi wa mgambo kuanzia mwezi Juni, 2008 hadi Novemba, 2008 katika mikoa mbalimbali nchini. Mafunzo hayo ya kuuandaa umma wa Watanzania katika mapambano dhidi ya adui yamefanyika katika ngazi za mafunzo ya awali, mafunzo ya kujikumbusha kwa wanamgambo na wakufunzi, kozi za uongozi mdogo wa mgambo na kuunda kombania za mgambo vijijini. Aidha, yamefanyika mazoezi ya kivita ya vikosi vya mgambo katika Kanda nne za ulinzi nchini chini ya usimamizi wa Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa teknolojia ya Kijeshi na Uendelezaji wake. Moja ya maeneo muhimu katika azma ya kujenga Jeshi dogo la Kisasa ni kuimarisha uwezo wetu wa utafiti wa teknolojia ya kijeshi kwa madhumuni ya kuliwezesha Jeshi kuzalisha bidhaa kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya ulinzi na usalama hapa nchini. Katika

mwaka 2008/2009, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuweka mkazo katika kutekeleza jukumu hili kwa kufadhili shughuli za utafiti na uzalishaji katika mashirika yake ya Mzinga na Nyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mzinga liliendelea na utekelezaji wa mradi wa kukarabati na kuboresha majengo na mitambo yake ili kuongeza uwezo katika shughuli za utafiti na uzalishaji. Baadhi ya miundombinu ya shirika ikiwemo barabara, mifereji na mabwawa ya maji machafu imekarabatiwa. Aidha, kwa kutumia wataalam wake katika kufufua na kukarabati baadhi ya vifaa vilivyokuwa vimeharibika kiwandani ili kuendelea kuvitumia katika uzalishaji. Vile vile, Shirika liliendelea na ukarabati wa vifaa vya kijeshi vilivyoharibika, kufanya utafiti na kubuni teknolojia kwa ajili ya matumizi ya kiraia kama vile kutengeneza mashine za kupasulia, kuranda na kukereza mbao; mashine za kupukuchulia, kukobolea na kusaga nafaka pamoja na mashine za kukamua mafuta na breki za gari moshi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumbu, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Shirika la Nyumbu limefanya yafuatayo;- kuboresha mfumo wa tekinohama, kutoa mafunzo kwa wafanyakazi, kukarabati wa mitambo, majengo na karakana, kuendeleza utafiti wa magari na mitambo, kutengeneza mashine za kufyatulia matofali ya "*hydraform*" kwa kutumia saruji na udongo wa mfinyanzi na trekta ndogo za *power tiller*, pamoja na kutengeneza vipuri vya magari na mitambo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Ujenzi wa mazingira nadhifu na salama ya kufanyia kazi na huduma ya makazi katika Makambi ya Jeshi pamoja na huduma, stahili na maslahi kwa Wanajeshi, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma ni maeneo ya vipaumbele kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa sasa. Katika mwaka 2008/2009 Wizara iliendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, huduma muhimu za maji, umeme, mwasiliano, tiba pamoja na kinga kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na huduma ya makazi katika Makambi. Hatua muhimu imefikiwa katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na huduma ya makazi katika Makambi kwa Wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa. Nilipokuwa nawasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2008/2009 hapa Bungeni nilieleza kwamba Wizara yetu kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba mpya 242 za kuishi Wanajeshi katika makambi yaliyoko katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Napenda kutoa taarifa kwamba ujenzi wa nyumba hizo umekamilika na zilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Januari, 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imedhamiria kuyaimarisha kwa kuendeleza ushirikiano na *NSSF* na mashirika mengine ya ndani na nje ya nchi yatakayopatikana kwa lengo la kupunguza

makali ya tatizo sugu la uhaba mkubwa wa nyumba za kuishi Wanajeshi katika makambi linalolikabili Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa nyumba hizo mpya umetekelezwa sambamba na utekelezaji wa mpango wa kukamilisha viporo vya ujenzi wa majengo mbali mbali, ukarabati wa majengo ya zamani zikiwemo nyumba za kuishi, ofisi na madarasa pamoja na miundombinu ya katika makambi. Katika mpango huo, kwa mwaka 2008/2009 miradi ifuatayo ya ujenzi imetekelezwa na kukamilika katika makambi ya Jeshi la Wananchi:- darasa la *simulator* – Pangawe (Morogoro), *sterilisation block* na choo - Hospitali Kuu ya Kijeshi Lugalo (Dar es Salaam) na jengo la walinzi na uzio Msangani (Kibaha). Pamoja na mafanikio hayo mikataba ya ujenzi ya miradi iliyokamilika ya ukarabati wa mfumo wa majitaka, Mirambo (Tabora), na ujenzi wa mahanga ya zana (Shinyanga), hanga la zana Kiluvya (Kibaha), maghala Kinonko (Morogoro), bwalo (Musoma) na hanga la ndege – Ukonga (Dar es Salaam) ililipiwa na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, vile vile miradi ya ukamilishaji wa viporo 44 vya nyumba za kuishi askari waliooa Makambako (Iringa), ukamilishaji wa viporo 36 vya nyumba za kuishi askari waliooa na bwalo (Pemba), ukarabati wa ofisi kikosi cha uhandisi wa medani – (Ngerengere), ujenzi wa hanga la zana – Welezo (Zanzibar), ujenzi wa nyumba za maafisa kapera Kigamboni, ujenzi wa ghala la silaha Changanyikeni, ujenzi wa "unit aid station", Mgulani, na ujenzi wa mabweni, Masaki (Dar es Salaam), ujenzi wa ofisi na mabweni (Shinyanga), ujenzi wa mtandao wa maji safi Njohu (Mtwara), ukarabati wa mfumo wa majitaka katika Shirika la Mzinga (Morogoro) na Navy (Kigamboni), ujenzi wa mtandao wa maji safi Msangani (Kibaha), ukamilishaji wa jengo la Wizara Upanga (Dar es Salaam) na ukarabati wa hospitali ya Bububu (Zanzibar) yote ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa shughuli zilizotekelezwa ni kukamilisha viporo vya ujenzi wa mabweni, zahanati, nyumba za kuishi askari wa kudumu, ujenzi wa mabafu, vyoo na miundombinu ya maji na umeme katika makambi ya Bulombora (Kigoma), Ruvu (Pwani), Oljoro (Arusha), Mgambo (Tanga), Chita (Morogoro), Mafinga (Iringa), Mlale (Ruvuma) na Makao Makuu ya JKT (Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma muhimu za maji, umeme, simu, mahitaji muhimu ya mafuta, vilainisho na vipuri. Katika mwaka 2008/2009 Serikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji, umeme, simu, mahitaji ya mafuta, vilainisho na vipuri vya magari, mitambo na vifaa mbalimbali kwa ajili ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ulipiaji kikamilifu wa huduma na mahitaji haya muhimu umekwazwa na uwezo mdogo kifedha ikilinganishwa na mahitaji halisi, hali iliyosababisha kulimbikiza madeni. Pamoja na kuwepo hali hiyo hatua mbali mbali zimechukuliwa kudhibiti matumizi ya huduma na mahitaji haya ili kuepukana na kulimbikiza madeni. Mojawapo ya hatua hizo ni kutenganisha kasma ya matumizi ya

mafuta na vilainisho katika sehemu mbili za mahitaji ya majukumu ya mafunzo, mazoezi kwa Wanajeshi na operesheni za kiulinzi na mahitaji ya majukumu mengine ya kiutawala. Lengo la hatua hiyo ni kuhakikisha kwamba mahitaji muhimu ya kiulinzi hayakwamishwi na mahitaji ya majukumu ya kiutawala.

Mheshimiwa Spika, huduma ya mawasiliano. Mazingira mazuri ya kufanyia kazi katika makambi, ni pamoja na uwepo wa huduma ya uhakika ya mawasiliano ndani ya makambi, baina ya makambi na nje ya makambi. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuuboresha mtandao wa Mawasiliano ya Pekee Jeshini *(Indepenedent Telecommunication Network - ITN)* ili uendane na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano ulimwenguni na hivyo kuimarisha huduma ya mawasiliano jeshini. Maboresho hayo ni pamoja na kufanya ukarabati wa minara na kufufua baadhi ya mitambo ya mtandao huo iliyoharibika, kutandaza nyaya (*cabling*) na kuweka vifaa vipya katika vituo vya mawasiliano vilivyoko Mafinga, Songea, Makambako, Mzinga, Pangawe, Potoa, Navy Kigamboni, Kisarawe, Tabora, Mwanza na Makao Makuu ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, maslahi kwa Wanajeshi. Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa Umma, katika mwaka 2008/2009 stahili za mishahara, posho, malimbikizo ya mishahara kwa waliopandishwa na waliobadilishiwa vyeo na huduma ya maziko kwa Wanajeshi, watumishi wa umma na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa zimetolewa kikamilifu na kwa wakati. Hata hivyo, baadhi ya stahili zikiwemo mavazi, vifaa vya malazi na likizo zilitolewa kwa kiwango cha wastani kutokana na mahitaji kuwa makubwa ikilinganishwa uwezo uliokuwepo kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya chakula kwa Wanajeshi. Kuanzia mwezi Machi, 2009 kiwango cha posho ya kumlisha Mwanajeshi mmoja kimeongezwa kutoka shilingi 2,500.00 hadi 3,500.00 kwa siku na baadae mwezi Aprili, 2009 kilipandishwa hadi shilingi 5,000.00. Japo ongezeko hilo kuwa la asilimia 100 bado halikidhi mahitaji halisi ya huduma ya chakula kwa Mwanajeshi mmoja kwa siku. Serikali bado inayo dhamira ya kuboresha zaidi kiwango hicho uwezo wa kifedha utakapoimarika.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha huduma ya tiba na kinga kwa Wanajeshi na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, Watumishi wa Umma na raia kwa ujumla. Katika mwaka 2008/2009 huduma za kinga na matibabu mbali mbali kwa Wanajeshi na watumishi wa umma na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutolewa kwa kutumia mtandao wa vituo vya tiba visivyopungua 70. Vituo hivi vimetoa huduma za tiba kama upasuaji, pua na koo na huduma za afya ya uzazi na watoto.

Aidha, kwenye baadhi ya vituo hivyo zimetolewa huduma za uchunguzi wa maradhi mbalimbali. Vtuo hivyo ni pamoja na Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Hospitali ya Jeshi-Mbeya, Hospitali ya Jeshi-Mwanza, TMA-Monduli, Mazao-Morogoro, Hospitali ya Bububu na JKT Mgulani zilizopanuliwa na kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa msaada wa kifedha na kiufundi kutoka Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani imetoa msaada wa kukarabati Hospitali ya Jeshi ya Kanda huko Nyumbu (Kibaha) na kwamba kazi hiyo tayari imeshaanza. Vile vile Serikali hiyo imekubali kujenga Hospitali ya Jeshi ya Kanda huko Tabora katika eneo la Nyuki na tayari imelipatia Jeshi la Wananchi msaada wa "mobile hospitals" mbili zikiwa na vifaa vyake vya tiba na magari.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inathamini sana misaada inayotolewa na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa Jeshi la Wananchi, hususan katika sekta ya tiba. Msaada tunaopatiwa ni mkubwa na wa kutegemewa siyo tu kwa Wanajeshi bali pamoja na Watanzania kwa ujumla. Hivyo, napaenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa msaada na ushirikiano wao unaoendelea kuimarika mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza pia kwamba tathmini imekwishafanywa kuboresha Hospitali za Songea, Ngerengere, Kigamboni, Pangawe, Bulombora na Nachingwea kwa lengo la kuimarisha huduma ya tiba katika Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, ufufuaji wa Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana wa Kitanzania. Katika mwaka 2008/2009, Jeshi la Kujenga Taifa limeendeleza kazi ya ufufuaji wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuchukua vijana wa kujitolea kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani na kuwapatia mafunzo ya kuwajenga katika uzalendo, ulinzi, usawa na umoja wa kitaifa, pia kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi stadi. Vijana waliopo katika makambi kwa sasa idadi yao ni 7,110. Vijana hawa wapo katika makundi mawili ya Operesheni Maisha Bora ambao idadi yao ni 2,819 wanaotarajiwa kumaliza mkataba wao wa miaka miwili tarehe 15 Julai, 2009 na Operesheni Uadilifu ambao idadi yao ni 4,219 watakaomaliza mkataba wao wa miaka miwili tarehe 30 Juni 2010. Mpaka sasa kuna makambi saba (7) yanayotoa mafunzo ya awali ya uzalendo, ulinzi, usawa na umoja wa kitaifa ambayo ni Makutupora (Dodoma), Mafinga (Iringa), Oljoro (Arusha), Mlale (Ruvuma), Ruvu (Pwani), Bulombora (Kigoma) na Mgambo (Tanga). Makambi haya yana uwezo wa kuchukua vijana 1,000 mpaka 1,500 kila moja.

Mheshimiwa Spika, yapo makambi mengine saba yanatumika kuendeshea mafunzo ya Stadi za Kazi, makambi hayo ni Rwamkoma (Mara), Mgulani (DSM), Chita (Morogoro), Maramba (Tanga), Itende (Mbeya, Nachingwea (Lindi) na Mbweni (DSM). Aidha, hatua kadhaa zimechukuliwa ili kuboresha malezi na mafunzo ya vijana kwa kuwaandaa wakufunzi ili kuimarisha kada ya ukufunzi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwapeleka kozi za ukufunzi zinazoendeshwa na Mamlaka ya Ufundi Stadi nchini (VETA);

(ii) Kuendesha semina kwa wakufunzi kama vile kilimo, ufugaji na kadhalika;

(iii) Kuwahimiza wakufunzi wenye viwango vya chini vya ujuzi kujiendeleza kimasomo ili waweze kumudu kazi ya kuwalea vijana; na

(iv) Kushiriki kozi za ujasiriamali (entrepreneurship) ili wakufunzi hao wawafundishe vijana jinsi ya kubuni na kuendesha miradi yao baada ya kuondoka JKT.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo katika ufufuaji wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kupanua uwezo wa makambi hayo ili kuweza kuchukua vijana 10,000 kwa wakati mmoja. Hii ni kwa kuzingatia utekelezaji wa uamuzi wa Serikali wa kuchukua vijana wa mujibu wa sheria ifikapo mwaka 2010/2011. Changamoto nyingine ni jinsi ya kuwatumia vijana wanaofuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa maana ya kuleta tija katika Taifa, hususan mageuzi ya kilimo nchini na kuimarisha ulinzi na uzalendo wa Taifa dhidi ya athari hasi za utandawazi, maendeleo ya teknolojia na mwingiliano mkubwa wa watu ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa kufunga mjadala kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2008/2009, ilitolewa hoja hapa Bungeni kwamba ifanyike tathmni ya kutosha ili kuanzisha makambi zaidi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika maeneo mengine ya nchi. Wizara iliahidi kuifanyia kazi hoja hii na naomba kuchukua fursa hii kuitolea maelezo. Kwanza nieleze kwamba katika kufanya uamuzi wa kuanzisha Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa yapo mambo ya msingi ya kuzingatiwa hususan ukubwa wa eneo, hali ya miundombinu, upatikanaji wa huduma muhimu na uwepo wa mazingira yanayoruhusu utekelezaji shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini iliyofanyika maeneo mapya matano kwa sasa yanakidhi mahitajio ya kuanzishwa makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, na maandalizi ya kupokea vijana yanaendelea. Maeneo hayo ni:- Msange (Tabora), Kanembwa (Kigoma), Tarime (Mara), Muleba na Missenyi (Kagera). Maeneo ya Msange na Kanembwa tayari yameshakabidhiwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kufufua makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ambao umelenga kuchukua vijana wanaotakiwa kujiunga na JKT kwa mujibu wa sheria ifikapo mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka, utawala bora. Kwa lengo la kuboresha huduma mbalimbali zitolewazo kwa wateja wa ndani na nje, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, chini ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma Awamu ya II, imeandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja *(Client Service Charter).* Mkataba huo utazinduliwa hivi karibuni, baada ya kuujadili kwa pamoja na wateja wetu na kuanza kutekelezwa mwezi Agosti, 2009.

Aidha, chini ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeandaa Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* wa Wizara unaoainisha malengo, majukumu, kazi na jinsi ya kugawanya rasilimali ili kutekeleza majukumu ipasavyo na kwa ufanisi zaidi. Chini ya

Programu hiyo watumishi wa kada za kutunza kumbukumbu na makatibu mahsusi wamehudhuria mafunzo ya utunzaji kumbukumbu yaliyoendeshwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni muhimu katika kutatua kero kubwa wanayopata watumishi kupata maslahi yao hususan wanapostaafu kutokana na kutokuwepo kumbukumbu muhimu katika majalada yao. Wizara pia imegharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake katika fani mbalimbali nje na ndani ya nchi ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeandaa mikutano ya Baraza la wafanyakazi. Aidha, Wizara imewawezesha wafanyakazi wake kushiriki kwenye sherehe za Mei Mosi, Siku ya Wanawake Duniani na Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2009 ambapo wananchi wamepata fursa ya kuelimishwa kuhusu majukumu na huduma mbalimbali zitolewazo na Wizara. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote waliotembelea mabanda ya Wizara na kutoa maoni yao. Aidha, nawaalika wananchi kujitokeza kwa wingi kutembelea mabanda yetu kila maonyesho haya yanapofanyika ili kujionea bidhaa mbalimbali zinazotegenezwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI. Juhudi za kupambana na UKIMWI katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa zimeendelea kwa kuwaelimisha Wanajeshi na watumishi wa umma kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI. Kamati mbalimbali za ushauri vikosini zimeundwa kuongeza jitihada za kukabiliana na ugonjwa huu. Waathirika hupata dawa za kurefusha maisha (ARVs) ambazo hutolewa bure kupitia Bohari Kuu ya madawa (MSD). Dawa hizo hutolewa kupitia vituo vya Jeshi vya *Care and Treatment Centres*. vilivyoko katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Hospitali za Jeshi za Mbeya, Mwanza, na Bububu (Zanzibar), pamoja na Hospitali za Kanda za Mazao (Morogoro), TMA (Arusha), Mirambo (Tabora), Luhuwiko (Ruvuma) na Nyumbu (Pwani). Ufadhili wa kuanzishwa vituo hivyo unatoka *Department of Defence* ya Serikali ya Marekani ikishirikiana na *Pharm Access International*.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa vituo hivi havitoi huduma kwa Wanajeshi, watumishi wa umma na familia zao tu bali pia kwa raia wanaoishi maeneo yaliyo karibu na hospitali hizo. Wafadhili wengine ambao wamekua wakitoa misaada ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi ni pamoja na *Global Fund* na Benki ya Dunia ambao wamekuwa wakielekeza misaada yao kwenye kuzuia maambukizi ikiwemo uhamasishaji wa Wanajeshi wa ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa. Rushwa ni adui mkubwa wa utawala bora. Kwa kutambua hilo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na mikakati ya kupambana na rushwa kwa kusisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa uwazi na uadilifu. Katika kutekeleza hili kila Idara na Vitengo hasa vinavyohusika na utoaji na usimamiaji wa huduma na zabuni zimetakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia

taratibu, kanuni na sheria zilizopo. Wizara pia inachukua hatua madhubuti ya kuimarisha mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma Jeshini ili kuzuia mianya ya rushwa na kusimamia kwa makini zaidi mikataba mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, imeunda Kamati ya Mazingira kuratibu utekelezaji wa sheria hiyo katika Wizara na Taasisi zake. Kamati hiyo inaundwa na wajumbe kutoka Makao Makuu ya Wizara, Jeshi la Wananchi, Jeshi la Kujenga Taifa, na Mashirika ya Mzinga na Nyumbu ambayo kila moja ina kamati yake ya utendaji kwa masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009, Wizara imendesha vikao vya kamati za mazingira, kufuatilia shughuli za mazingira katika taasisi zake, kujenga uelewa wa mazingira kwa watumishi, kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wanakamati, kupitia na kuboresha mtaala wa mafunzo ya vijana wa JKT kuhusu masuala ya mazingira na kuendesha mafunzo mafupi kwa wakufunzi wa vijana. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha Kikosi cha Jeshi 692 cha Tabora kimeshinda tuzo maalamu ya utunzaji wa msitu wa asili ulioko kikosini hapo.

Mheshimiwa Spika, michezo. Kwa kutambua kwamba, michezo kwa Wanajeshi na watumishi wa umma inasaidia kuimarisha afya, akili na ukakamavu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilishiriki katika mashindano ya Shirikisho la Michezo la Wizara (SHIMIWI) yaliyofanyika mjini Morogoro na mashindano ya mpira wa miguu na wa pete yaliyofanyika Musoma wakati wa maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi ambapo timu yetu ya mpira wa pete ilifanikiwa kuchukua kombe la mshindi wa kwanza wa mchezo huo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio muhimu ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2008/2009. Shabaha kuu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ni kuimarisha na kujenga uwezo wa kudhibiti ulinzi wa Taifa kwa kufanya mambo makuu yafuatayo:-

(a) Kujenga jeshi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa kwa ajili ya majukumu ya ulinzi wa nchi yafuatayo:-

(i) Kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya uvamizi wa adui;

(ii) Kushiriki katika majukumu ya kulinda amani duniani;

(iii) Kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na maafa ili kuokoa maisha na mali za wananchi; na

(iv) Kuandaa na kuongoza umma wa Watanzania katika jukumu la ulinzi wa Taifa dhidi ya adui.

(b) Kulijenga Jeshi la Kujenga Taifa ili liwe na uwezo wa hali ya juu wa: -

(i) Kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, ulinzi, usawa na umoja wa kitaifa na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi stadi;

(ii) Kuwa chimbuko la ajira kwa vyombo vya ulinzi na usalama hapa nchini; na

(iii) Kuwa chombo cha kuchangia uzalishaji mali nchini.

(c) Kuendeleza utafiti na kujenga uwezo katika teknolojia ya kijeshi; na

(d) Kujenga na kudumisha amani na utulivu na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia shabaha hizo, mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2008/2009 kwa ujumla yameweza kuonekana katika uimarishaji wa uwezo wa Jeshi la Wananchi katika kudhibiti ulinzi na usalama wa mipaka yetu. Uhusiano wetu na nchi nyingine duniani katika nyanja za kiulinzi. umeendelea kuimarika na hivyo kudumisha mazingira ya amani na utulivu kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani hasa majirani zetu. Kutokana na mafanikio hayo hakukuwa na adui yeyote kutoka nje aliyeathiri usalama, amani na utulivu wa nchi yetu. Nchi imeendelea kuwa imara na salama na wananchi wameendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi limeendelea kutoa msaada wa kukabiliana na maafa na majanga yalipojitokeza na kudhibiti wavamizi wanaopora rasilimali za Taifa kama vile uvuvi usiozingatia sheria katika maeneo yetu ya Bahari ya Hindi. Aidha, zoezi la kufufua JKT linaendelea kwa mafanikio makubwa Idadi ya vijana waliochukuliwa katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya mafunzo ya uzalendo, ukakamavu na umoja wa kitaifa ilifikia 7,110 ikilinganishwa na vijana 6,677 katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio muhimu katika kuhakikisha usalama wa nchi yetu. Hata hivyo, kwa kuzingatia mwenendo wa kiusalama katika ukanda wetu wa Afrika na duniani kwa ujumla, bado tunayo kazi ya kuimarisha zaidi ulinzi wa nchi yetu. Hili ni jukumu la gharama kubwa na haliwezi kufanikishwa katika kipindi kifupi kutokana na uwezo mdogo wa uchumi wa Taifa. Serikali inalitambua jukumu lake hili la msingi na inalishughulikia hatua kwa hatua kadri uwezo wake kifedha unavyoimarika.

Mheshimiwa Spika, malengo ya bajeti ya mwaka 2009/2010. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2009/2010, imelenga kuimarisha uwezo wa Jeshi kulinda usalama na uhuru wa nchi pamoja na kudumisha amani na utulivu baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, Fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2009/2010 ni kwa ajili ya utekelezaji wa mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Kulipia gharama za matumizi ya huduma na mahitaji muhimu kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kiulinzi na usalama;

(b) Kuwapatia Wanajeshi, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa umma huduma na stahili mbali mbali ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(c) Kuendeleza teknolojia na uzalishaji katika vituo vya utafiti na viwanda vya kijeshi;

(d) Kuendeleza ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na ulinzi kupitia ushirikiano kati ya nchi na nchi, ushirikiano wa kikanda na kimataifa;

(e) Kuendeleza mafunzo ya kuwajenga vijana wa Kitanzania katika ukakamavu, uzalendo na umoja wa Kitaifa, na kuwandaa katika uzaliashaji mali kwa kuwapatia elimu ya awali ya ufundi stadi, kilimo, ufugaji, uvuvi, ujasiriamali na taaluma nyinginezo katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa;

(f) Kuimarisha ofisi za Waambata Jeshi huko Washington DC, New York, Rwanda na Afrika Kusini;

(g) Ukamilishaji wa baadhi ya viporo vya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika makambi ya Jeshi la Wananchi huko Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Bukoba, Tabora, Makambako, Mtwara, Kibaha, Dodoma, Shinyanga, Morogoro, Zanzibar na Mtwara;

(h) Ujenzi mpya wa majengo ya ofisi na makazi katika makambi ya Jeshi la Wananchi huko Biharamulo, Kigoma, Kibaha, Tanga, Arusha, Dar es Salaam, Zanzibar, Tabora, Mbeya, Dodoma na Morogoro;

(i) Ukarabati wa majengo na miundombinu katika makambi mbalimbali ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa;

(j) Utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Utumishi wa Umma Awamu ya Pili kwa kumalizia ufungaji wa mtandao wa mawasiliano na kuanzisha mkakati wa elimu, mawasiliano na habari; na

(k) Uboreshaji wa mazingira katika maeneo ya makambi ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kufanikisha na kutekeleza jukumu la kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango iliyosaidia kufanikisha maandalizi ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyonayo juu yangu ya kuendelea kunikabidhi madaraka ya kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yenye dhamana nzito ya kuhakikisha ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitatumia uwezo na ujuzi wangu wote ili kufanikisha matarajio aliyonayo juu yangu katika utekelezaji wa majukumu aliyonikabidhi. Vile vile, kwa niaba ya Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kulijali Jeshi la Wananchi kihuduma na kivifaa ili liweze kutimiza wajibu wake wa kulinda uhuru na usalama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) na Mawaziri wote kwa msaada na ushirikiano walionipatia katika kutekeleza majukumu yangu katika mwaka 2008/2009. Pia kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi (Mb.) na wajumbe wa Kamati hiyo kwa msaada na ushirikiano walioutoa kwangu na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi (Mb.), Katibu Mkuu, Bwana Andrew S. Nyumayo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis A Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Abdulrahaman A Shimbo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali SN Kitundu, Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma. Wote nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa walionipa na kwa ushauri wao ulio makini na wenye uaminifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa ushirikiano wao walionipa katika mwaka 2008/2009. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, naomba pia kutoa shukrani zangu kwa Serikali za nchi mbalimbali kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda pia kumshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali na Watumishi waliopo chini yake kwa kuichapa na kuikamilisha Hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2009/2010, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama ilivyoelezwa katika hotuba hii,

kwa mwaka 2009/2010, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 443,340,823,000.00 ambapo kati yake Shilingi 395,179,305,000.00 zitatumika kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 48,161,518,000.00 ni Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, Shilingi 47,860,118,000.00 ni fedha za Ndani na Shilingi 301,400,000.0 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zimegawanywa katika mafungu kama ifuatavyo:-

**(a) Fungu 38: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania**

(i) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida – shilingi 312,707,205,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo –shilingi 20,000,000,000.00 ambazo zote ni fedha za ndani.

(b) Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa

(i) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida – Shilingi 69,077,870,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo–Shilingi 13,500,000,000.00 ambazo zote ni fedha za ndani.

(c) Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

(i) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida – Shilingi 13,394,230,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo–Shilingi 14,661,518,000.00 ambazo kati yake Shilingi 14,360,118,000.00 ni fedha za ndani, na Shilingi 301,400,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Samahani ya pili, haikustahili hapo ingawa kweli ni muda, lakini huwa Spika hufumba kidogo Waziri asingongewe kengele ya pili.

**MHE. WILSON M. MASILINGI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipata nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kabla sijaanza kuwasilisha taarifa yenyewe, kwa kifupi ninapenda kuchukua nafasi kutoa

salama za rambirambi kufuatia msiba mkubwa wa Sheikh Gorogosi uliotokea kutokana na ajali. Tunaomba roho ya Marehemu ilazwe mahali pema peponi. Amina.

Aidha, natoa salaamu za rambirambi kufuatia kifo cha Profesa Haroub Othman aliyekuwa Mwalimu wetu, pale Chuo Kikuu, katika nadharia ya Maendeleo na Mwanasheria mwenzetu. Roho ya Marehemu ilazwa mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo za rambirambi, napenda kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114 (11), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, tarehe 15 Januari, 2009, Kamati ilifanya ziara kutembelea Kikosi cha 832 KJ Ruvu na kupata Taarifa ya Maandalizi ya kuchukua Vijana wa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria, ifikapo Mwaka 2010. Tarehe 16 na 17 Aprili, 2009, Kamati ilitembelea Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonyesha kuwa hali ya Ulinzi kwa ujumla, ni shwari na Jeshi letu limejipanga vyema kulinda mipaka ya nchi yetu pamoja na kuimarisha amani na utulivu baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani na hasa nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Aprili, 2009, katika Kikosi cha 511, ilitokea milipuko iliyosababisha madhara makubwa eneo la Mbagala. Ili kuona hali halisi ya madhara ya milipuko hiyo, tarehe 02 Mei, 2009, Kamati ilitembelea eneo la tukio na kupata maelezo ya kina kutoka kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi *(Chief of Defence Forces – CDF)* kuhusu tukio hilo. Aidha, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Naibu wake walitoa ushirikiano wa kutosha. Kamati inawapa pole wananchi wote wa Mbagala walioathiriwa na milipuko hiyo ikiwa ni pamoja na Maofisa na Askari wa Jeshi la Wanachi wa Tanzania. Aidha, Kamati inalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Serikali kwa ujumla, kwa ujasiri wa Askari wetu katika kuchukua hatua za haraka na juhudi kubwa ya kukabiliana na athari ya milipuko iliyotokea na kuepusha madhara makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, wakati raia wakiikimbia hatari hiyo, Askari walikimbia kuelekea kwenye eneo la milipuko ambalo ni la hatari na kuweza kuepusha madhara makubwa kutokea. Tunawapa pole na kujivunia ujasiri wao wa kujitolea muhanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 04 Juni, 2009 Kamati ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam, kupokea na

kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2009/2010, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi, Mbunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Taarifa hiyo ilihusu mafungu matatu ya Wizara kama ifuatavyo na kama alivyowasilisha:-

i) Fungu 38 - Ngome;
ii) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na
iii) Fungu 57 - Wizara

Mheshimiwa Spika, katika kikao na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wasaidizi wake Kamati ilielezwa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2008/2009;

(ii) Malengo ya Bajeti kwa Mwaka 2008/2009 na utekelezaji wake;

(iii) Mwelekeo wa matumizi ya fedha hadi Juni, 2009;

(iv) Mafanikio ya utekelezaji wa malengo;

(iv) Changamoto;

(v) Malengo ya bajeti ya mwaka 2009/2010; na

(vi) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kamati ilielezwa namna Wizara ilivyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia dhima, dira, shabaha na malengo ya bajeti kwa mwaka 2008/2009. Aidha, Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuhusu ukusanyaji wa mapato yaliyotokana na uuzaji wa vifaa chakavu, nyaraka za zabuni na makato mbalimbali kwa mafungu yote matatu; ngome, Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa pia kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2008/2009. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, fedha zote zilizopokelewa kutoka Hazina zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya bajeti. Ufafanuzi wa kina kuhusu utekelezaji huo ulitolewa wakati wa kikao cha Kamati tarehe 04 Juni, 2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa Kamati imeridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009. Ni matumaini yetu kuwa Wizara hii itaendelea kuwa madhubuti katika utekelezaji wa majukumu yake ya kimsingi ili kuendeleza na kuimarisha ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alitoa taarifa ya utekelezaji wa maoni na ushauri kila mara tulipokuwa tukikutana kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. Taarifa za Wizara hii zinaonyesha kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Kamati ilielezwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na Polisi, wamefanikiwa kudhibiti kwa kiasi kikubwa na wanaendelea kushirikiana katika kukabiliana na wimbi la ujambazi katika maeneo ya Mikoa ya Shinyanga, Kagera, Mwanza, Mara na sehemu nyingine za nchi kama vile Mkoa wa Pwani, Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro.

Aidha, Serikali imezingatia ushauri wa Kamati yetu ya Bunge wa kutoa Kandarasi kwa Majeshi yetu kama kianzio ili kupunguza gharama za Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuwezesha Majeshi yetu kwa kuwapatia fedha na vifaa vyote vya kisasa ili miradi kwa mfano ule Mradi wa Barabara ya Msata – Bagamoyo ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, ni Serikali kubatilisha Kanuni iliyokuwepo katika Kanuni za Pensheni za Majeshi ya Ulinzi (*Defence Forces Service Pensions and Gratuities Regulations)*, iliyoweka ukomo wa malipo ya pensheni ili wastaafu wote waliopunjwa walipwe mafao yao yote kwa muda wote waliotumikia Jeshi kihalali. Tunashukuru Serikali kwa kukubali ushauri huu wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kuwapa haki zao mashuja wetu hao walioathirika na Kanuni hiyo ya Serikali kuhusu Pensheni.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilituhakikishia kuwa Kanuni hiyo imetenguliwa ili kila aliyetumikia zaidi ya miaka thelathini na sita na nusu alipwe fedha zote zilizo kuwa stahili yake. Waziri aliileza Kamati kuwa Kiasi kinachohitajika kwa waliokatwa ni Shilingi 432,208,305.85 na kwamba fedha hizo ziliombwa Hazina. Kamati inasisitiza kwamba malipo hayo yafanyike haraka iwezekanavyo kwa sababu ni haki ya Wanajeshi wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa na kuridhishwa na hatua za Serikali katika kutatua tatizo la gharama ya umeme na ushirikiano wa wahusika wote. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kulipa madeni ya Majeshi yetu, ambayo yalikuwa yamekaa kwa muda mrefu. Jitihada hizi ziendelezwe kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuhusu malengo ya bajeti na mwelekeo wa kazi za Wizara ya Ulinzi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Serikali inalenga kuimarisha uwezo wa Jeshi kulinda mipaka ya nchi na kudumisha usalama, amani na utulivu baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani. Kamati iliridhishwa na kufurahishwa na mwelekeo huo mzuri na kuishauri Serikali iendelee kuwa madhubuti katika utekelezaji wa azma hiyo yenye maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa ili kufanikisha azma ya Serikali na malengo yake kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaomba kuidhinishiwa makadirio yake ya mapato kwa mafungu matatu kama tulivyokuwa tumetaarifiwa:-

(i) Fungu 38 - Ngome: Sh. 2,650,000/=
(ii) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa: Sh.23,501,000/=
(iii) Fungu 57 - Wizara: _Sh.20,002,000/=
Jumla : Sh.46,153,000/=

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa matumizi, Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi, Mb, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliiambia Kamati kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekadiriwa kutumia shilingi mia tatu tisini na tano bilioni, mia moja sabini na tisa milioni, laki tatu na elfu tano (395,179,305,000/=) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kwa ajili ya maendeleo wamekadiria jumla ya shilingi arobaini na saba bilioni, mia nane sitini milioni, laki moja na elfu kumi na nane (47,860,118,000/=) kama alivyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hivi punde.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa undani Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Mpango wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Baada ya kupitia Kifungu kwa Kifungu katika mafungu yote matatu, Kamati inaunga mkono maombi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na kutoa ushauri ufuatao:-

(i) Madeni yote ya zamani ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo hayajalipwa yachukuliwe na Hazina na kulipwa mapema iwezekanavyo;

(ii) Serikali ihakikishe kuwa watoa huduma za maji na umeme kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa wanadai malipo kwa kuzingatia matumizi halisi kama yanavyoonyeshwa na vipimo halisi hasa *Meters*. Hatua hiyo itaondoa utata katika Jeshi na kuandaa malipo hayo;

(iii) Ili kuwezesha utekelezaji wa mpango wa kuboresha makazi ya Askari na Maafisa wa Jeshi, Serikali iendelee kutumia vyema Mashirika ya Hifadhi za Jamii;

(iv) Kila inapotokea Askari wetu wanaorodheshwa kwenda kwenye Operesheni za Kulinda Amani, Serikali ihakikishe kuwa Askari hao wanakatiwa Bima ya Maisha; hii itaepusha manung'uniko kama yaliojitokeza kwa Askari wetu ambao wameumia vitani huko Kagera na kwingineko ambako wanaendelea kuathirika, lakini tunavutiwa na mpango wa Serikali kuirekebisha hali hiyo, kwa kuboresha mafao yao na pensheni;

(v) Serikali iweke utaratibu utakaofanikisha Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa kutoa mafunzo ya ulinzi na uzalendo na kujenga Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi katika Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa; na

(vi) Ili kutekeleza azma ya kutoa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana wengi wanaohitimu Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Sita kwa ufanisi, kila Wilaya iwe na Kambi maalum ya Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu ukisaidiwa na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Aidha, napenda kukupongeza binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya kuongoza mabadiliko na kuimarisha Bunge letu Tukufu. Pia nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa mara nyingine ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, katika kusimamia masuala ya Ulinzi na Usalama wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimmshukuru Mheshimiwa Dr. Hussein A. Mwinyi, Mbunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, Mbunge, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nawashukuru pia Ndugu Andrew Nyumayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya taarifa na ushirikiano waliotoa wakati wa kupitia Taarifa za Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Majeshi yetu katika Ulinzi wa Nchi, nampongeza kwa dhati Jenerali Davis A. Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF). Nawapongeza pia Luteni Jenerali Abdulrahman A. Shimbo, Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Meja Jenerali Samuel N.Kitundu, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa umakini wao na ujasiri wao katika kazi na utendaji wao katika Ulinzi wa Nchi na usimamizi wao wa Mafunzo ya Ukakamavu na Uzalendo kwa Vijana na Askari wetu. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje , Ulinzi na Usalama, kwa ushirikiano, busara na umakini mkubwa waliokuwa nao katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Shukurani maalum zimwendee Makamu wangu Mheshimiwa Mussa Zungu kwa ushirikiano na msaada wake katika kuiongoza Kamati. Kwa kuuthamini mchango wa Wajumbe wa Kamati, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mwenyekiti na Mheshimiwa Musa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H.Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi na Mheshimiwa Col. Mst. Feteeh S. Mgeni.

Wengine ni Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brg. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dr. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Nawashukuru sana Makatibu walioihudumia vyema Kamati hii wakati wa kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Kamati na hata wakati wa kuchambua Taarifa za Wizara hii, Makatibu hao ni Ndugu Athuman Hussein na Katibu mpya Stella Mlambo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, nakuhakikishia kwamba tunaunga mkono hoja na tunaomba Wabunge wakubali hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa na kukubali maombi yote aliyowasilisha katika hotuba yake. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa uwasilishaji mzuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Msemaji wa Upinzani, ninapenda mtambue tu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii sasa amekaa mbele pale na Waziri wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. *(Kicheko)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia uzima na afya njema, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(3) na (7), Toleo la Mwaka 2007, kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile kwa msaada na imani waliyonayo kwangu katika kuendeleza na kutekeleza majukumu yangu ndani ya Jimbo, ndani ya Chama na hata nikiwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, itakuwa sikuwatendea haki hata kidogo kama sikumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu

Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Dr. Slaa, pamoja na Wabunge wote wa Upinzani, kwa ushirikiano walionipa katika kufanya kazi zangu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza hotuba na kutoa maoni yetu, natoa masikitiko makubwa kuwa Jeshi letu ambalo ni kioo cha utendaji bora katika anga za ndani na za kimataifa, kubambikiziwa au kutumiwa na watu ambao hawana nia njema na nchi hii pale wanaposema kuwa wanaotuhumiwa kuwa vinara wa ufisadi wa TANGDOLD NA MEREMETA wamefanya kwa niaba ya Jeshi. Hivyo sasa ni vyema Watanzania kuweza kuruhusiwa kuhoji ufisadi huo. Kwani Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa kuwa kama tendo limefanywa na mtu mmoja mmoja ni kwa nini sura hiyo ya ufisadi linapewa Jeshi zima kama taasisi? Tunamtaka Waziri atoe masahihisho hayo ili chombo hiki kiwe na rekodi yake ile ile ya uchapa kazi na uaminifu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni kwa nini fedha za usafiri za Wanajeshi wanapokwenda kozi, au wanaposafiri kikazi mara nyingi huamriwa wajigharamie wenyewe na Serikali kuahidi itarejesha fedha, je ni kwa nini Serikali hairejeshi fedha hizo na je Wizara ina mkakati gani wa kuondokana na hilo na kuwapatia haki zao walioathirika na mkasa huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali, Wanajeshi wanapokwenda kozi ya uongozi ndogo au kubwa, ni vyema wakimaliza mafunzo haya wakapewa vyeo vyao huko huko chuoni, kama atakavyofaulu badala ya utaratibu wa sasa wa kurudi chuoni na kukaa muda mrefu hatimaye kufikiriwa kupandishwa cheo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kuelewa ni kwa nini Wanajeshi wananunua baadhi ya vifaa muhimu katika maduka ya Jeshi kwa bei sawa na maduka mengine huku ikijulikana baadhi ya ushuru umeondolewa ili kupunguza makali kwa ajili ya Wanajeshi, je, tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Sera na Sheria yetu ya Ulinzi, ni ya zamani tangu mwaka 1966 huku dunia ikishuhudia mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kisayansi na kadhalika. Hivyo pamoja na mabadiliko hayo, kuna haja ya kuiangalia kwa upeo Sera nzima ya Jeshi ili iendane na wakati huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia pia mabadiliko katika mfumo wa kisiasa baadaye Bunge litunge Sheria ambayo itakuwa ndio nyenzo ya kuhakikisha Sera inafuatwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, aliliambia Bunge la bajeti la mwaka 2008/09 kuwa, nanukuu:-

*"…bila kuhuisha sheria, hatuwezi kufika mbali. Nataka niseme hapa kwamba Kamati imeundwa na imepewa muda hadi mwisho wa mwezi wa tisa iwe imefikisha ripoti yake Wizarani, tuipeleke katika Kamati ya Ulinzi ili tufanye kazi".*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza mchakato huo umefikia wapi? Kwani mwezi wa tisa ulikuwa wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kurekebishwa haraka kwa Sera na Sheria kwani inakandamiza maslahi ya Wanajeshi wetu, kama vile Wanajeshi wanaotumikia Jeshi kisheria kwa zaidi ya miaka thelathini na sita, lakini wakaamriwa kuendelea kulitumikia Jeshi kwa manufaa ya nchi, hulipwa mafao yao kwa miaka thelathini na sita tu na inasikitisha miaka inayoongezeka kwa amri halali huwa hawalipwi mafao yao. Hivyo Kambi ya Upinzani, inaiomba Serikali kurekebisha haraka dosari hii kwa dhamira ya kuboresha Sera na Sheria sambamba na Kanuni ya Pensheni za Majeshi ya Ulinzi *(The Defence Force Service Pensions and Gratuities Regulations),* ili Wanajeshi wote walioathirika na Kanuni hii wapatiwe haki zao zinazostahili. Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni idadi gani ya Wanajeshi walioathirika na Kanuni hii tangu Kanuni hii ilipoanzishwa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ni vyema Sera na Sheria za Ulinzi wa Taifa kuangaliwa upya ili kuweza kuboresha mazingira ya Kijeshi zaidi ili kuufuata Mfumo wa Siasa za Vyama Vingi na Jeshi la Ulinzi linatakiwa kuwa *"non-partisan"* hivyo basi Jeshi kuweka mkakati wake wa kujiimarisha kwa kufuata mwelekeo wa Chama kilicho madarakani ni makosa. Jeshi halitakiwi kufuata Sera za Chama bali linatakiwa kufuata Sheria za nchi na mipango yake au Sera zake kama Jeshi la nchi bila ya kuegemea upande wowote wa Chama cha Siasa. Hili limebainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka wa fedha 2007/2008, ukurasa wa 14, Kifungu cha 19.

Mheshimiwa Spika**,** mbali na shughuli zinazofanywa na sekta ya ulinzi nchini za kuimarisha usalama wa Taifa lakini bado haijaleta tija inayotakiwa na kuweza kunyanyua uchumi wa nchi hii kama inavyotegemewa na wananchi walio wengi na hasa kwa kuzingatia wanavyofanya Majeshi na Askari wa nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi na teknolojia mpya kuanzia Jeshini. Katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2007/2008 ukurasa wa 31, Mheshimiwa Waziri alilieleza Bunge hili kuwepo na utekelezaji wa mradi wa mtandao wa mawasiliano ya kipekee *(independent Telecommunication Network-ITN).* Mtandao huu wa Jeshi ndio ungekuwa msingi mkuu wa kuiwezesha Serikali kutoa huduma ya mawasiliano kwa mfumo wa Serikali Mtandao *(e-Government*).

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ya mwaka jana, hakuongelea maendeleo ya mradi huo ambao tunaamini ungekuwa ni ukombozi mkubwa katika kuzalisha teknolojia ya kisasa kwa Watanzania na kwa Tanzania kwa ujumla wake. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri kutueleza nini kinaendelea kuhusu mradi huu wa *ITN*? Ni kwa vipi Jeshi letu linakuwa ndio wavumbuzi wa teknolojia rahisi zitakazoongeza uzalishaji na kuinua uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, Ili taasisi zetu zilizo chini ya Jeshi la Ulinzi zifanikiwe zinahitaji kuwa wazi, kuwa wavumbuzi na kukubali kubadilika na kuendena na maendeleo ya kisayansi na technolojia. Tunarudia tena kunukuu yale ambayo mwaka jana tuliyaongea ya Mtaalamu wa *Physics Rutherford* alinukuliwa akisema kwamba:-

*"We are short of money so we must think".*

Wanajeshi wetu wafahamu kuwa tuna tatizo la umaskini hivyo, inatulazimu kila wakati kufikiri kwani uvumbuzi unahitajika zaidi na vipaji binafsi *(talented military personnel*) na si vyema kusubiri bajeti, kwani ni finyu na kwa staili yetu ni ukweli kuwa itaendelea kuwa finyu na hata kwa miaka 20 ijayo. Hii ni kuangalia utegemezi bajeti uliokuwepo tangu Marehemu Kighoma Malima, akiwa Waziri wa Fedha mwaka 1993/1994 ulikuwa ni asilimia 38% leo miaka 16 baadaye, utegemezi ni asilimia 33.45%.

Mheshimiwa Spika, tuliishauri Serikali kuhusu, shirika letu la Nyumbu, wabuni magari ambayo yataendana na mazingira halisi ya barabara za Tanzania na ambayo yatatumia gharama na kuleta tija. Hivyo, ni vyema Serikali nayo itenge fedha za kutosha au kuwawekea utaratibu bora wa magari hayo kuzalishwa kibiashara yaani *"Assembly line of production"*. Waziri alikubaliana na hilo, je, ni hatua gani au mkakati gani umewekwa ili Watanzania wanufaike na Shirika letu la Nyumbu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi mbali ya kuwa nguzo hasa ya ulinzi wa nchi yetu pia limekuwa msitari wa mbele katika kutoa huduma mbalimbali kwa umma. Kambi ya Upinzani, inaelewa na kupongeza mchango mkubwa unaotolewa na Jeshi letu katika nyanja mbalimbali za kijamii, kama vile huduma za tiba, kutoa msaada katika maafa au majanga yanayotokea hapa nchini na mengine mengi yanayogusa jamii moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka wa fedha unaoishia juni 30, mwaka 2008, inaonyesha kuna upungufu kadhaa ambapo ni pamoja na malipo yaliyofanywa bila kuwepo hati za kufanyia malipo hayo, madai ya miaka ya nyuma kwa Askari ambayo hayakulipwa na mishahara ambayo haikulipwa lakini haikurejeshwa Hazina, upungufu wote huo ni kiasi cha shilingi 1,751,804,763.00. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini upungufu huu unajirudia kila mwaka na Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kukomesha upungufu huu usitokee tena? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa, limekuwa chachu kwa vijana kupata mafunzo ya kijeshi na kiufundi katika kujenga nidhamu, uzalendo, na uwajibikaji wa siku hadi siku kwa lengo la maslahi ya Taifa kwa ujumla. Hivyo, stadi mbalimbali wanazopata JKT mfano ujenzi, kilimo, ufugaji, useremala, ni kwa kiasi gani vijana hawa wanaendelezwa kwa kuwawezesha kujiendeleza kimaisha mara tu wamalizapo mafunzo yao na kutobahatika na ajira Serikalini? Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwadhibiti vijana wa JKT ambao walimaliza mafunzo yao na hadi leo hawajapata ajira lakini pia ni dhahiri walipata mafunzo ya kutumia silaha, kwa lengo la kutojiingiza katika vitendo vya uhalifu? Kwa sasa Serikali imetenga jumla ya shilingi 13,500,000,000. Kama fedha za kuanzisha utaratibu wa vijana wa mujibu wa Sheria watakaojiunga na Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na dhana ambazo kwa upande wetu na wale wote ambao walipitia Jeshini, ni vigumu kuamini kuwa wale wa kujiunga kwa mujibu wa

sheria walikuwa wanatia hasara kwani uzalishaji ulikuwa haulingani na matumizi. Je, Serikali ina makakati gani wa changamoto hiyo hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kuelewa sababu za msingi ambazo zilizokuwa zimesababisha kusitishwa kwa mafunzo hayo kwa vijana wa mujibu wa sheria. Aidha, ni kwa kiasi gani Serikali imejiandaa ili yale yaliyopelekea kusitishwa kwa "*in-takes*" za mujibu wa sheria hayatatokea tena?

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT limekuwa mfano bora hivi sasa katika uzalishaji wa mali hasa ujenzi wa nyumba bora za kisasa katika maeneo mbalimbali. Pamoja na sifa walizonazo SUMA JKT. Kambi ya Upinzani, inataka ufafanuzi kwa nini SUMA JKT, halijaunda Kamati ya Ukaguzi kinyume na Kanuni Na. 30, 31 na 32(2) ya Kanuni za Fedha za Umma kama ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30, 2007 ilivyobainisha, sambamba na hilo ni kwa nini, Shirika la SUMA JKT, halijaanzisha Kitengo cha Manunuzi kinyume na kifungu cha 44 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni lini SUMA JKT, itaunda Kamati ya Ukaguzi na ni lini SUMA JKT litaanzisha Kitengo cha Manunuzi kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi? Kambi ya Upinzani, inataka kujua viwanda vya kushona sare za Jeshi la Ulinzi na JKT hasa kiwanda cha CAMISUMA na kiwanda cha JKT RUVU, vimefanikiwa kushona sara kwa thamani ya shilingi ngapi; kwa kipindi cha mwaka 2008/2009?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kuelewa Kiwanda cha Kutengeneza Dawa cha TANZANSINO, kimepata faida kiasi gani 2008/2009, tangu kianze kushirikiana na mbia (*Holley Industry Group Company Ltd,)* mwenye uwezo wa mtaji na teknolojia zaidi baada ya kuachana na mbia wa awali?

Mheshimiwa Spika, mafao kwa mashujaa wetu. Mwaka jana tuliomba kuelewa kuhusu jinsi Serikali inavyoshughulikia malalamiko makubwa kwa Mashujaa wetu walioshiriki Vita vya Kagera mwaka 1978/79, walioshiriki Vita vya Msumbiji waliopelekwa Liberia, ambapo wengi wao sasa ni wastaafu na wenye ulemavu na wengine wameshafariki dunia huku familia zao wakiendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, mashujaa hawa niliowataja ambao wengi wao ni walemavu, wanaishi katika maisha ya kubahatisha, wakiwa wanyonge na ikionekana Serikali imewatekeleza muda mrefu; na wanajiuliza hivi kulitumikia Taifa na kupata ulemavu ni adhabu na kama si adhabu ni kwa nini Serikali badala ya kuwaenzi, wanawatelekeza wao na familia zao?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni nani anapaswa kuwajibika kuwaenzi na kuwatunza majeruhi wa vita vya Kagera na Msumbiji kati ya Makao Makuu ya Jeshi na Wizara ya Ulinzi na je pesa zao zikitoka Serikalini zinafikia kwa nani? Ninayaleta haya kwa sababu fedha zinazotolewa haziwafikii walengwa na hawajui ni kiasi gani. Huu ni unyonyaji na kuwakandamiza na kuwadhulumu Mashujaa

wetu ambao tungalitarajia Serikali itawaenzi kwa nguvu zake zote. Aidha, Kambi ya Upinzani, inataka kufahamu Wanajeshi wetu wanaopelekwa *DAFUR* kulinda amani watakuwa na Bima yao ya Maisha? Kwani Kambi ina wasiwasi pia, mafao yanayotolewa kwa mwamvuli wa *UN*. Je, yatakuja kuwasaida vipi Wanajeshi hao watakaorudi salama au kwa wengine watakaopata ulemavu?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kila mfanyakazi, ni mstaafu mtarajiwa hali za maisha za wastaafu wetu, ni mbaya sana kiasi ambacho hawawezi kumudu kukidhi mahitaji yao ya lazima hata kwa asilimia 40%. Ikumbukwe kuwa tarehe 21.4.2009, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi alijibu hapa Bungeni kwamba kima cha chini cha wastaafu ni Shs.50, 000/= na sio Shs.21600/= kwa mwezi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haelewi kuwa wakati huu haikuwa sahihi hadi leo kuna Askari wa JWTZ wanapata kiwango wa Shs.21600/= kwa mwezi?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha akihitimisha hoja yake alisema kima cha chini cha mshahara kwa wastaafu ni Shs.50, 000/=, lakini kwa mujibu wa Gazeti la Serikali, Tangazo la Serikali (*Government Notice)* No. 89 la 21.7.2006, lilieleza bayana nyongeza ya kima cha chini cha pensheni toka shs.21600 hadi 36,000/= ambapo ilitakiwa kutekelezwa kuanzia tarehe 1.7.2004

Naomba kunukuu:-

*"Supplement No. 24 Of 21 July 2006 Subsidiary Legislation. To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No. 29, Vol 87 Dated 21st July 2006. Printed By The Government Printer Dar -Es Salaam, By Order Of Government. The Public Service Retirement Benefit Act (Cap 371).*

*Order Made Under Section 30 The Public Service Retirement Benefits (Minimum Pension (Amendments) Order 2006).*

*1. This order may be cited as the Public Service Retirement Benefits (Minimum Pension (Amendment) Order,2006 and shall be read as one with the Public Service Retirement Benefits (Minimum Pension) order 2003 referred here in as the "principle order" and shall be deemed to have come into operation on the 1st day of July 2004.*

*2. The schedule to the order is hereby deleted and substituted for it with the following new schedule.*

| *Rate %* | *From* | *To* | *Semi-Annually* | *To* |
|---|---|---|---|---|
| *7.5%* | *216000/=* | *36,000/=* | *129,000/=* | *216,000/="* |

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua kwa nini Serikali haikutimiza matakwa ya Tangazo lake, Agizo la Sheria GN No.89, Sheria ya tarehe 21

July 2006, lililotangaza kupandisha *pension* toka Tshs 21600/= kama kima cha chini hadi shs.36000/= kuanzia July 2004 kutotekelezwa hadi sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu hawa wa *pension* wa kima cha chini walitakiwa kupokea Shs.216,000/= badala ya 129,000/= kuanzia tarehe 01July 2004, hivyo kuna ongezeko la tofauti la Shs.87,000/= kila muda wa miezi 6. Inasikitisha kuona kwamba kima cha chini cha pensheni sasa ni Shs.50000/= toka 21,600/= ambapo hali halisi kima cha chini cha *pension* ya mstaafu ni Shs.36,000/= kama GN No. 89 inavyoonyesha. Je, Serikali imepata kigugumizi gani cha ahadi yake kwa wastaafu?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuitanabaisha Serikali kwamba tangu itoe tangazo lake hilo GN No. 89, kila mstaafu wa Serikali anayepata *pension* ya kima cha chini anaidai Serikali Shs.870,000/= kwa tofauti ya Shs.129,000/= hadi 216,000/= kwa kipindi cha miezi sitini sasa, kuanzia ilipoahidiwa pensheni hiyo yaani tarehe 1July,2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kujua, ni kwa nini Serikali inaandaa jambo muhimu na baadaye wanalinyamazia na kuwakandamiza, kuwanyonya wastaafu wa kima cha chini, njia hii si udhalilishaji na ufisadi uliojificha dhidi ya wastaafu? Kambi ya Upinzani inataka kujua ni lini Serikali itawalipa wastaafu wote wa kima cha chini tofauti yao ya Tshs.870,000/= kila mmoja kabla ya kuanza mchakato wa Shs.50,000/= kwa mwezi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua kwa nini Serikali iliondoa pensheni *slip* kwenye malipo ya pensheni ya wastaafu toka July 2004 hadi sasa na kusababisha mchanganyiko mkubwa kwa wastaafu juu ya kuelewa malipo yao halali wanayolipwa. Je, Serikali ilikuwa na dhamira gani juu ya kutowalipa wastaafu haki yao hiyo ya msingi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba Serikali, mstaafu mume au mstaafu mke mmoja anapofariki ni vyema malipo ya pensheni yakaendelea kulipwa kwa mmoja wapo aliyebaki hadi na yeye atakapofariki. Hii inatokana na hali ngumu ya maisha anayoipata mwenza mmoja anayebaki baada ya mstaafu mhusika kufariki.

Mheshimiwa Spika, kambi za Jeshi kuwa karibu na makazi ya raia, ni dhahiri kuwa sasa kumekuwepo na upungufu mkubwa ambao umesababisha kilio na hasara kubwa kwa wananchi pamoja na Serikali kwa ujumla. Mkasa uliotokea hivi karibuni wa milipuko ya mabomu kwenye Kambi ya Jeshi iliyoko Mbagala hadi sasa wananchi wameshindwa kueleweka nini chanzo hasa cha milipuko ambapo baadhi ya wananchi wamepoteza wapendwa wao pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madhara makubwa  yalitokea katika mlipuko wa mabomu katika Kambi ya Jeshi Mbagala na kwa mujibu wa majibu ya Serikali hapa

Bungeni tarehe 9.6.2009, Waziri alisema kuwa hadi June 6, 2009, milipuko ilisababisha vifo vya watu 26 na majeruhi 703, lakini je, Serikali inafahamu uharibifu wa mali kama vile nyumba zaidi ya 9049 pia ziliharibika?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi hapa Bungeni kwamba, Tume iliyoundwa itakabidhi taarifa yake tarehe 20 June, 2009, je, kulikoni hadi leo ripoti hiyo haijatolewa? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulihakikishia Bunge lako Tukufu Jeshi letu limeweka mikakati gani katika kuhakikisha kuwa zana hatari za kijeshi zinatunzwa katika maeneo ambayo hayaingiliani na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kuwachukulia hatua kali wale wote waliozorotesha kutoa chakula cha msaada kwa waathirika na kupelekea malalamiko makubwa juu ya waathirika hao. Katika kupata huduma zao za msingi na kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, posho ya chakula (*ration allowance)* kwa Mwanajeshi ni Shs.150,000/= kwa mwezi ni kidogo mno kwani ni wastani wa Shs.5000/= kwa siku kwa milo mitatu. Hivyo Kambi ya Upinzani, inaomba Serikali kupandisha posho ya chakula kwa Askari wetu angalau iwe Shs.240,000/= kwa mwezi ikiwa ni wastani wa Shs.8,000/= kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi ni kwa nini Wanajeshi wa madaraja mengine wanapewa fedha zao taslimu shs.150, 000/= ikiwa ni posho ya chakula na wengine hawapewi fedha taslimu na badala yake wanakula posho hiyo kupitia wazabuni. Je, ni kweli kiwango cha 5000/= kwa siku kinamalizika kwa huduma inayotolewa? Hivyo, Kambi ya Upinzani, inaiomba Serikali kuwatendea haki sawa Wanajeshi wote wa ngazi zote kwa kuwapatia fedha taslimu Shs.150,000/= kama posho ya chakula, vinginevyo ni kuunda tabaka la haki zinazostahili kwa baadhi ya Wanajeshi tu na kwa hii haipingani kabisa na *"chain of command"* kwa madaraja mengine kama Sheria na Kanuni za Jeshi zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ya wachangiaji saba na siwashawishi mlete zaidi kwa sababu nadhani hii inatosha. Sasa nitawataja watatu wa mwanzo ambao ni Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, alikuwa hajachangia kabisa na Mheshimiwa Mohamad Ibrahim Sanya, naye alikuwa hajachangia, lakini kwa wale ambao tayari wamechangia, nitamuita Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, baada ya hao wawili, kwa sasa namwita Mheshimiwa Yono Stanley Kevela.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuwa mchangiaji wa kwanza. Kwa kweli nilikuwa nafikiria kwamba Bunge hili sitachangia, lakini nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kupongeza hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kweli ametoa hotuba nzuri na mikakati yake kwa kweli ni mizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijachangia, nilikuwa nafikiria kwamba nianze kutoa pole hasa kwa waathirika wa mabomu kule mbagala. Kwa hiyo, natoa pole sana kwa waathirika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi, kwa kweli tunawapa pole sana; kwa sababu ilikuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini mchango wangu utajikita katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza nitajikita kwenye upande wa wastaafu kwamba, hawa wastaafu kama hotuba tulivyokuwa tunaisikia hapa Bungeni, wana matatizo makubwa sana. Kiwango wanacholipwa bado ni kidogo. Ni kidogo kwa maana kwamba Shs.50,000/= kwa mtu wa chini, ni kidogo sana, yaani sijui tusemeje.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naongea na Brigedia mmoja ambaye ni mstaafu anasema kiwango chake ni cha shilingi laki mbili. Sasa laki mbili ukiangalia na mchango wako aliokuwa ametumikia nchi hii, bado ni kidogo sana. Kwa hiyo, ninashauri Serikali iangalie uwezekano wa ku-*review* hivi viwango vya wastaafu maana wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Katika ujana wao, katika utumishi wao wa kazi, Wanajeshi ni watu nyeti sana, ama Wapiganaji na Makamanda, ni eneo kwa kweli *sensitive*. Muda wa kufanya biashara, wa kujishughulisha na shughuli labda za kufuga kuku, ni kidogo sana, hawafanyi hizo shughuli kabisa, muda mwingi wako kwenye mazoezi. Sasa nafikiri kwa kweli lazima tuangalie uwezekano wa kuwawezesha hawa wastaafu wanapostaafu wapewe pensheni ambayo ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nichangie ni kuhusu suala la vitendea kazi. Sio siri kuna vitendea kazi kama meli hizi za jeshi kwenye *deep sea* bado tuna upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna hili tatizo la ndege za kivita za kisasa. Mimi nilipokuwa kwenye jeshi, kulikuwa na F6 sielewi sasa hivi tuna *vision* ya namna gani kwa kweli, ndege bado kuna upungufu sana na siwezi nikaingia *in detail* kwa sababu ni vitu vya kijeshi na Kanuni zetu siyo vizuri tuvieleze zaidi. Lakini kwa kweli kuna haja ya kuongeza meli za kisasa na kuongeza ndege za kisasa kwa ajili ya wanajeshi wetu, kwa ajili ya ulinzi wa mipaka na sehemu mbalimbali.

Halafu lingine ambalo nilitaka kuchangia Mheshimiwa Spika, ni kuhusu suala la maslahi. Kule jeshini nyumba bado ni tatizo. Ni vizuri hawa wapiganaji wetu na Makamanda tuwawezeshe nyumba ziwe mzuri kwa sababu kwa kweli inatakiwa tuwe na jeshi dogo, lakini jeshi hilo dogo liendane na maslahi yake kwani bado sio mazuri. Nyumba zao bado ni tatizo pamoja na mishahara na mambo ya mafunzo, kwa kweli

inatakiwa mafunzo yawe ya mara kwa mara. Wanajeshi wetu wawe na mafunzo mazuri, kwa mfano, sasa kuna teknolojia ya kompyuta, kuna vitu vingi. Jeshi letu lazima liwe la kisasa na lazima liwe dogo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu suala la JKT, mimi kwa vile ni mchangiaji wa kwanza napenda niseme kwamba suala la JKT kwa kweli ni la muhimu sana pamoja na Mgambo. Sasa JKT imesahaulika, tunasema imesahaulika kwa sababu, tunasema litaanza mwaka 2010, lakini maandalizi ninavyoona bado ni kidogo sana. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kwamba hawa vijana wanaomaliza Darasa la Saba, hawa vijana wanaomaliza Kidato cha Nne hata cha Sita na Vyuo Vikuu kwa sababu Kanuni bado ipo, tuanze mapema sana waingie JKT. Tunaposema JKT maana yake ni kwamba kuna vitu vingi sana ambavyo tunaviona kule kwenye JKT. Kwanza ni suala la uzalendo. Uzalendo umepungua sana katika nchi hii kwa sababu JKT kwa sehemu kubwa tumelipuuza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, JKT itakuwa ni mkombozi wa uzalendo, watu watakuwa wanaingiliana, wa Mkoa wa Iringa wanachanganyikana na wa Mkoa wa Kagera wanachanganyikana, kwa hiyo, kukiwa na uzalendo, watu watalipenda Taifa lao. Hata hili suala la rushwa lingepungua kabisa kwa sababu kuna uzalendo.

Halafu lingine nizungumze labda suala la ukakamavu na uzalishaji mali. Kwa sababu JKT kama tukiitumia vizuri hata hili suala la kilimo kwanza, hii *Green Revolution* ndiyo mahali pake. Sasa tunalalamika, watu tunakimbizana na Wamachinga pale Dar es Salaam, Mwanza na wapi kuna Wamachinga. Lakini tukiwafanyia hii JKT, wanakwenda kwenye mashamba yao, mambo yangekuwa mazuri. Sasa Serikali ingeonyesha kwamba sasa hivi ndiyo mapinduzi ya kilimo, *Green Revolution.*

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba suala la JKT tusilipuuzie. Kwa hiyo na Makamanda wetu wange-*train* watu wetu. Kwa hiyo, katika uzalishaji mali. Kwa mfano, sasa hivi hakuna vita. Vita sasa hivi iko kwenye njaa. Suala la njaa lingekuwa halipo. Vijana wetu wangezalisha, wasingekuwa wanazurura zurura. Kwa hiyo, naishauri Serikali suala la JKT tulipe kipaombele pamoja na Bajeti pamoja na kwamba Bajeti ipo, sehemu kubwa nimeona ya matumizi kuliko ile ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine nilikuwa nataka nizungumze kuhusu suala la Bima ya Maisha. Tunaelewa Wapiganaji wetu, Makamanda jinsi wanavyokuwa majasiri, wanakwenda huko Comoro, wanakwenda wapi na wapi, Darfur, lakini: Je, Suala la Bima likoje? Ni vizuri tuangalie nalo kwamba wanapokwenda kule, Bima za Maisha ziwe nzuri na tuhakikishe kwamba wanaporudi wapewe posho nzuri, pamoja na kwamba wanapewa vyeo, lakini vyeo huwezi ukala cheo tu. Lazima uwape na hali nzuri. Unaweza ukamjengea nyumba, ukafanya chochote. Unaelewa hili la nyumba nimepata nilipokwenda Darfur, hii nyumba nilipokuwa Comoro. Sawa unaweza ukampa manyota hapa, lakini: Je, atakula nyota wakati kuna familia inapata shida?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naona hapa unacheka, naona utalifanyia kazi hilo. Halafu lingine ni kuhusu mikopo kwa wanajeshi na wapiganaji.

Mikopo kwa kweli wapewe wale watu, tena iwe ya nafuu. Yaani ikiwezekana Serikali ifanye makusudi kabisa kwamba kama vyombo vya fedha vinatoa mikopo kwa riba fulani labda kubwa au ni kidogo, basi Serikali ichangie kiasi fulani iwe kama ni ruzuku, kwa sababu hawa wanajeshi hali zao siyo nzuri, wanateseka sana. Kwa hiyo, ni vizuri kama wanapewa mikopo yao iwe na riba nafuu sana na sehemu nyingine ichangie Serikali. Nilikuwa naomba kwa hilo mtilie maanani.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naona kwa vile ni mchangiaji wa kwanza, ni vizuri kwamba niwaachie wenzangu watachangia vizuri zaidi kuliko mimi. Baada ya kusema hayo, naomba nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kevela. Namwita sasa Mheshimiwa Mohammed Ibrahim Sanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi na baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah. Mheshimiwa Sanya.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii angalau na mimi nichangie machache kuhusu Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kwanza, natoa shukrani za dhati kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa namna wanavyo-*take on* matatizo ambayo yanajitokeza, wakati mwingine katika hali ya *emergency*. Wanajeshi wa Tanzania ni watu wa kupewa sifa zote kutokana na kazi mahiri wanazozifanya. Ni wanajeshi ambao wanalinda uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, sisi kama tutakuwa na kilimo kwanza, afya, elimu, biashara na viwanda, lakini yote haya yanaweza yakafanyika kwa ufanisi iwapo ulinzi wa nchi utakuwa mzuri. Amani ya nchi inajengwa na vyombo viwili, katika nchi, Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi. Wa mwanzo kufika ni Jeshi la Polisi pahali panapotokea tatizo lolote. Ikishindikana hapo tunatumia wanajeshi wetu kuweza kwenda kuhimili hali na kuweka hali kuwa shwari.

Mheshimiwa Spika, lakini inasikitisha sana kuona kwamba haki za askari wetu hasa wa Jeshi la wananchi bado hazijazingatiwa vilivyo. Tunapiga kelele haki za walimu, haki za madaktari, haki za wakulima, lakini wanajeshi tumewasahau. Tumewasahau kwa namna gani? Askari mwanajeshi yeyote katika makulaji yake au kula yake lazima kunakuwa na vigezo ambavyo anatakiwa avipate ili wafanye kazi vizuri. Nakumbuka Jeshi la wa Tanzania lilivyoanza katika miaka ya 1960.

Pale Zanzibar ilifika wakati baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 hata ndugu zetu akina dada walikuwa hawataki kuolewa zaidi ya kuolewa na wanajeshi au Polisi kwa sababu wanajua kwamba nikiolewa na Mwanajeshi au Polisi, nakwenda kuishi vizuri. Atapata chakula kizuri na atapata mafao mazuri. Leo dhana ile imetupwa. *(Makofi)*

Wanajeshi wanalipwa Sh. 5,000/= umtarajie ale asubuhi, ale mchana ale na usiku! Mwanajeshi ni raia kama tulivyo sisi, lakini kwa vigezo vya utendaji wake wa kazi na ili afanye kazi kwa ufanisi anahitaji *balance diet* itakayomwezesha kuweza kufanya kazi katika harakati za aina yoyote. Utaona wakati wa miaka ya 1964 kwa Mheshimiwa Karume wa mwanzo, wanajeshi walikuwa wanapewa mpaka karanga kwa mwezi sijui

kilo ngapi, mafuta kiasi gani, nyama ya aina gani, chakula cha aina gani, chepesi wakati wa mazoezi. Leo unapomlipa Sh. 5,000/= atakwenda kuchapia *chips* na kuku wa barabarani ambacho hakina faida yoyote zaidi ya kupata *cholesterol* na *starch* katika miili yao. *(Makofi)*

Lazima hili tuliangalie katika ukuaji wa uchumi sambamba na kuwapatia chakula ambavyo vinakwenda na kero za wanajeshi. Inasababisha hata kuona wazabuni wanapewa zabuni za kupeleka mboga mboga, *okay you can provide vegitables*, lakini huwezi uka-*provide* kuchinja ng'ombe ukawachukulia manyama tu ukawatupia kambini wanajeshi, *is a very sensitive organ.* Nyama ile hujui imechinjwa wapi, ng'ombe amepimwa vipi, unampelekea nyama *open*, sijui kama imeathiriwa na mwanadamu mwingine, kwa utashi wao tu wa kijinga kwa sababu katika kila nchi kunakuwa na wajinga kama hawa tuliokuwanao ambao wanataka utajiri kwa kuwachinja watoto albino. Kwa hiyo, wanaweza wakajitokeza tu watu ambao vichwa vyao ni vyepesi, havifahamu uzito wa namna gani mwanajeshi awe *provided* na chakula kilichokuwa kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali iwe makini kuwaongezea angalau wapate laki tatu kuanzia mwakani, ndiyo tunaweza tukajua kwamba wanajeshi wetu wameangaliwa na kuhusu makazi hakuna asiyejua. Hata sisi Wabunge ambao tunatembelea katika Kamati zetu kutembelea maeneo yao. Wakati mwingine huwa tuna wasiwasi kwa sababu kila tunapokwenda tunaona matatizo yale yale yapo. Kwa mfano, matatizo ya maji, matatizo ya sehemu za kujisaidia na matatizo ya makazi yao. Kwa nini iwe hivi kila mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tulitegemea kwamba Kamati inapotembelea inaona kwamba kuna *advancement* yoyote ya maeneo yao wanayoishi. Lingine ni kuhusu suala la uhamisho. Ni haki ya kila askari awe wa Jeshi la Polisi au Jeshi la Wananchi, kutoka sehemu moja ya Muungano au Mkoa mmoja kwenda mwingine au Kambi kwa Kambi. Lakini taabu wanayoipata wakati wa uhamisho huwa haziambatani na *cheque* zao za uhamisho. Halafu hata wanapofika huko wanakopelekwa katika uhamisho inawachukua muda mrefu sana kudai haki zao hizo. Hizo ni haki za msingi!

Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba Wizara husika ya Jeshi la Wananchi wakati wanapompa askari uhamisho wanampa na *cheque* yake mkononi ili tuondokane na aibu na kuwadhulumu haki zao hawa ambao ndio Watendaji na Walinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke mwaka 1978 walipopelekwa Uganda sisi tuliambiwa tujitayarishe tufunge mikanda kwa sababu ya hali ya uchumi. Chakula kama kipo au hakipo, lakini waliopelekwa *front line* ni wanajeshi. Wakapoteza maisha yao, wakaacha familia zao, wengine wakarejea walemavu mpaka leo wapo. Kwa nini tusiwape heshima ya leo wakayaona yaliyofanywa na wenzao, waliorudi wanaangaliwa vipi na wao wakawa na moyo wa utendaji katika Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, suala la wastaafu, *this must be a jock.* Unampa mstaafu Sh. 50,000/= jamani! Kwa nini tusitazame hali inavyokwenda? Hali ya maisha ni ngumu! Tusijidanganye tukasema kwamba hali ya maisha ni ngumu halafu anayestaafu hasa

Mwanajeshi au Polisi kakaa miaka mingapi kulitumikia Jeshi lake, kacheza na silaha za moto, anaweza akapoteza hata maisha katika mazoezi, leo anastaafu unampa Sh. 50,000/=.

Mimi ningependekeza wastaafu wote wawe wanakwenda sambamba na kima cha chini cha mshahara ili kila unavyopanda na yeye awe anajisikia anapanda. Kumkwamisha katika Sh.50,000.00 kwa miaka miwili, mitatu, mitano inakuwa tunamdhulumu haki zake za msingi wakati anapokuwa amestaafu.

Tuchukulie mfano, tuna wanajeshi ambao wamerudi Uganda walioathirika na vile vita, wamebakia 146 ambao hawana viungo, wengine mikono, wengine miguu, tunao katika nchi yetu ya Tanzania, wako upande huu Bara, wako Zanzibar, wanalipwa Sh. 50,000/=. *Just imagine* wewe kama binadamu umekosa kiungo, halafu anakuja mtu anakupa Sh.50,000/= kila mwisho wa mwezi, ina maana amekupa Sh. 1,600/= kwa siku. Hawa wako 146. Ukichukua Sh. 50,000/= kwa kila mmoja inakuwa Serikali imetumia Sh. 7,600,000/= kwa mwezi. Hivi hatuoni kwamba huu jamani, sijui niseme vipi? Angalau basi tuwafanyie laki moja iwe kwa mwezi Serikali inatumia kwa Wahanga wale Sh. 14,600,000/= na hiyo ni *just a drop in the ocean* kwa Serikali iliyo makini.

Kutumia Shilingi milioni 14 kwa mwanajeshi ambaye amepoteza kiungo, ambaye aliacha familia yake, ameipatia sifa nchi yake, anachukua Amri ya Amirijeshi Mkuu, akaenda mbele akapigana, anarudi unakuja kumlipa Sh. 50,000/=, *this is not fair*. Tutawafanya hawa waliokuwepo nao wajiulize, hivi hawa wanafanywa hivi, mimi nitafanywa nini? Ni sawa na mtu kwenda kung'oa jino, anapomwona mwenzake ananung'unika sana anapovutwa jino, ndiyo yeye anavyojiuliza sijui mimi itakuwaje nikiingia huko chumbani. Kuna wengine hata hukimbia na ganzi lake akaona kwamba hali yenyewe ndiyo kama hii! Hawa ni watiifu, wana nidhamu ya hali juu kabisa. Kwa hiyo, nidhamu zao za kufanyia kazi katika Jeshi lao na nchi yetu na kuchukua taratibu na Sheria za Jeshi na sisi lazima tuwaenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wana wakati mgumu sana. Wakati mwingine tunasoma kwenye magazeti, wanapanda kwenye madaladala maskini, wanagombana na raia, kumbe *depression* zake zile anaondoka zao kambini, anarejea nyumbani hana pesa mfukoni, watoto wanamsubiri, mama watoto, wanataka na wao waishi kibinadamu, siyo kumpa *uniform* tu na viatu. Lazima tuwajengee mazingira kwamba anafanya kazi, anajua mwisho wa mwezi anapata nini. Anafanya kazi anapostaafu anajua kwamba yeye ametengenezewa kiasi gani na Serikali yake kwa muda wote alioutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni wazabuni. Wazabuni wanatoa huduma kwa askari wetu. Hawa wazabuni wanapotoa huduma wanatumia fedha zao, wakati mwingine ni fedha za mikopo kutoka katika mabenki ambayo inawapandishia riba katika mabenki. Sasa wewe unapomcheleweshea *cheque* yake na yeye ndivyo anavyopunguza au kuchelewesha huduma kwa askari wetu. Lazima wazabuni zitengwe pesa. Sasa kwa mkakati maalum katika kipindi hiki cha mwaka tumalize madeni yao ili askari wetu wapate huduma. La sivyo, huduma watakosa.

Mheshimiwa Spika, wakikosa huduma nao utendaji wao utakuwa dhaifu. Kwa hiyo, ningependelea sana hawa wazabuni, jamani hebu tuwaangalieni wanajeshi wa nchi za wenzetu. Leo Uturuki ndiyo imechukua nafasi nzuri ya ku-*supply* majeshi mengi ya *NATO,* vyakula vyepesi na mimi napiga kelele siku zote hata wanajeshi wenyewe wanaweza wakakifanya hiki kitu.

Mheshimiwa Spika, nenda Njombe, nenda Mbeya, kuna viazi vyeupe ambavyo ni vizuri vya kutengeneza *pringles* au *chips* au biskuti wanazotumia wanajeshi. *It is easy to provide them,* itakupa uhakika wa chakula chao, twende tu tukachukue huu utaalam wa viwanda vidogo vidogo tu, tukatengeneza vyakula vyao, tukavi-*pack* vizuri, tuka-*supply* kama tulivyokuwa tunafanya miaka ya 1960. Siyo kuwaacha wanajeshi wakawa wanakula nyama au wanakula mboga mboga zilizochelewa, zilizopitiwa na muda. Tuwafanye nao wajisikie waone kwamba wana-*provide facility* ya ulinzi lakini na wao wanaangaliwa kimaslahi. *(Makofi)*

Halafu kuhusu hili la mabomu kulipuka Mbagala, tatizo, wakati mwingine Wizara haziwasiliani vizuri. Inakuwaje katika Kambi ya Jeshi kama ile unaweka silaha nzito halafu unaruhusu watu wanajenga maeneo ya karibu na Kambi? Mimi naelewa kuna kitu kinaitwa *Baffle Zone. Baffle Zone is almost 500 meters from the Camp.* Sasa ilikuwaje wanajeshi na wao wasipige ripoti kwa wahusika kwamba mbona raia wanakuja kujenga karibu na sisi? Inakuwa ni gharama kubwa sasa kuwaondoa wale, kuwatafutia makazi mengine wajenge mahali palipokuwa mbali na wanajeshi. Lazima makambi yawe na Sheria zake na taratibu zake ili yasivamiwe.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa leo kwa hayo nafikiri yanatosha kabisa, lakini naomba tena na tena Serikali yetu kwa umakini wake ihakikishe kwamba wanajeshi wastaafu wanapata haki zao wakati wanapostaafu wazipate na wale *pensioners* waongezwe fedha *from 50,000 to 100,000* na wapate kwa muda. Kuna wanajeshi hivi karibuni walivumilia karibuni miezi sita, wastaafu pesa zao hawalipwi.

Kweli tuna matatizo, lakini sijui niseme nini? Lazima tuangalie matatizo na uzito wa matatizo. Askari wetu wanajeshi wanafanya kazi nzito, wanacheza na silaha na vile vile sio vibaya hata wakati mwingine tunapotoa ajira kuna tabia ya watu wakisikia ajira tu wanakwenda kuandikishwa wanajeshi Visiwani nao huondoka huku Bara wakaja Visiwani.

Kwa Visiwani waachieni wa Visiwani haki zao. Wa Bara chukueni haki zenu kwa mujibu wa taratibu za Jeshi, naelewa zipo taratibu nzuri. Tukiwaona watu wanakuja kutoka Bara mnatuvunja moyo kwa sababu ni sehemu ya Jeshi la Muungano. Wanzibar wana haki kuajiriwa kwenye Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi nao wapate haki zao. Ili hali hii iende vizuri kuondosha hizi kero za Muungano, basi inapotokea taarifa kama hizi, washirikishwe viongozi wa maeneo mbalimbali.

Hata tukishirikishwa sisi Wabunge, wala kusiwe na dhana kwamba wanajeshi hawawezi kuwa *CUF, CUF* anaweza kuwa mwanajeshi tena mzuri tu. Kwa sababu Jeshi haliangalii, linaangalia ulinzi na ndiyo maana tukasisitiza kwamba Jeshi la JKT ili liweze

kutoa vijana wazuri na vijana wazuri wasichaguliwe kwamba huyu anatoka chama gani, ana itikadi gani, kwao wapi, baba yake ni nani.  Akiwa Mheshimiwa Sanya mwanawe anataka jeshi aingie tu jeshini.  Kwa nini asiingie.  Ndivyo wenzetu wa Marekani wanafanya siku hizi.  Utaona wanajeshi wa kila rangi wapo ndani ya Jeshi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi kwa leo sina zaidi isipokuwa nawashukuru sana wanajeshi. Endeleeni kuwa wastahimilivu, kuweni wavumilivu, kuweni na tabia na heshima za jeshi, mnalipatia jeshi letu sifa kubwa ndiyo maana mkawa mnapelekwa Darfur, mnapelekwa Lebanon na huko nako tufanye mazingira ya kwamba wanapewa *insurance* ili inapotokea dharura yoyote waweze kuwa *evacuated rescued* na wapewe haki zao za msingi ili wajisikie kwamba Serikali yao inawaangalia wanajeshi wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.  Ahsante sana.  *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mohammed Sanya. Sasa namwita Mheshimiwa Tatu Ntimizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah wakati huo huo Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru ajiandae.  *(Makofi)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.  Awali ya yote naunga mkono hoja ya Wizara hii.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini labda tu niseme kwamba wakitoka kwenye vita vijana wanapewa Sh. 50,000/= sijui tafsiri ikoje!  Mimi nilifikiri Sh. 50,000/= wanapewa yaani ni pensheni yao.  Sasa imekuwa kutoka kwenye vita!  Labda Waziri atueleze vizuri au mimi labda sikusikia vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, nilikuwa na machache ya kuzungumza kuhusu Wizara hii.  Ni Wizara ya Ulinzi, sio mipaka tu, hata wananchi waliomo ndani ya Tanzania.  Lakini mimi nilikuwa naomba nitoe tahadhari moja kwamba ajira katika majeshi tuizingatie sana.  Tusichukue kisomo au ujuzi tu, lakini na nidhamu.  Kwa kweli tangu tumeanza kusema kwamba tumchue wa *Form Four* mwenye kushinda, mwenye *Form Six* mwenye Digrii, mwenye nini, *collection* ya namna hii ina uzuri wake kwa kuwa wamekuwa wasomi, lakini kuna madhara yake kuhusu nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hili kwa sababu, huwezi kukuta majeshi wanagombana wenyewe kwa wenyewe kwa mfano Jeshi la Ulinzi likagombana na Polisi, Polisi wakagombana na Magereza, Magereza wakagombana na Usalama au na raia. Lakini imejitokeza sasa hivi wanajeshi wakipata matatizo wanachukua sheria mkononi jambo ambalo linaaibisha sana jeshi.  Hili ni jeshi la wananchi, si jeshi la mtu.

Nilisikitika sana kusikia kwamba wanajeshi wamekatiwa maji, halafu hawa wanajeshi wanatoka vijana kwenda kuwapiga wataalam wa maji.  Haijapata kutokea katika historia ya jeshi.  Kwa nini tufikie mahali hapa?  Wanajua utaratibu ulivyo, lakini kwenda kupiga wataalam wamekatiwa maji ni kweli Serikali lazima iendeshwe kwa taratibu zake.

Wizara nayo inategemea kutoa huduma, lakini huduma hiyo ihudumie pia, huwezi kukuta Wizara ya Maji inadai Jeshi la Polisi au Magereza linadai mabilioni ya pesa halafu wanakumbushwa Wizara hailipi au Jeshi lenyewe halilipi matokeo yake wanakwenda kukata maji, vijana wanaibuka na virungu, silaha walizopewa kulinda wananchi kwenda kupiga hawa watendaji ambao hawana hatia.

Hata Magereza nilisikia pia nao wamepiga watu Ukonga. Sasa haya majeshi *recruitment* hii tunafanyaje? Mimi kwa kweli nasikitika sana kama mmojawapo ambaye nilikuwa katika vyombo hivi, leo kusikia vijana wetu ambao tumewaajiri kwa kupitia sifa mbalimbali wanakuwa na sheria zao mkononi. Wanaaibisha majeshi, wanaiaibisha Serikali, wanawaaibisha na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana turudie tufanye hadidu za rejea. Tulikuwa tunaajiri vipi? Sifa zilikuwa zipi? Ilikuwa ni urefu tu, kama mimi hapa. Mimi nafikiri sasa hivi hatujali urefu, tunajali sifa za kisomi. Mimi naona turudie tena kutazama upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu jinsia. Tangu Madawili katoka kuna *General* mwingine sijamsikia sijui vipi! Naomba sana asiwe zawadi peke yake. Mimi mmojawapo nilikuwa katika Jeshi la Polisi, nilipata cheo cha Ukamanda. Lakini mara baada ya mimi kutoka wameendelea kuwa makamanda, kuna vyeo vikubwa kuliko hata mimi nilivyokuwa nimepata. Sasa huko vipi?

Kijana wangu namheshimu sana na yeye ananiheshimu. Lakini hebu Mwamunyange tazama kidogo hii jinsia, kwa kweli siku nyingi, nitakuwa mkali kidogo. Wameingizwa pale, aah, leo silii! Wameingizwa pale kwa uwezo na kwa sifa maalum, licha ya kuwa wanawake. Sasa leo tukiishia *reference* ni Madawili, hawa waliopo! Litazamwe hilo tupate jibu la uhakika leo. Kuna maandalizi au wapo? Naomba tusiwadharau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana kukosa maandalizi baada ya kustaafu. Askari wa majeshi karibu yote wa vyeo vya chini hawana maandalizi ya maisha yao baada ya kustaafu, licha ya kuongeza pensheni hii ya Sh. 50,000/=. Lakini tunawatayarisha vipi wakati wakiwa kazini? Imekuwa ni matatizo! Baada ya muda unasikia uvamizi, Askari Jeshi alikuwepo, au Polisi alikuwepo au Magereza alikuwepo ni kutokana na kutowaandaa hawa vijana. Sisi wakubwa kule tunapata nafasi nzuri, unastaafu na mshahara mzuri, unapewa ulinzi, unapewa magari, unapewa nyumba. Hawa walisababisha mpaka wewe ukapata nafasi hiyo, tunawatazama namna gani kama Serikali? Ni vijana ambao kwa kweli wanapata matatizo, ndiyo maana sasa umekuwa ujambazi. Vijana wanatumika kujiandalia maisha yao ya kesho jambo ambalo sio zuri kwa heshima ya majeshi yetu.

Naomba sana, Serikali itazame kama watapewa mikopo ni muda huu, siyo kuwapa mkopo amekwisha kuwa mtu mzima. Wapewe mikopo tu wajiandalie maisha yao angalau wajenge nyumba zao ili akitoka kwenye jeshi kule ambako anapata nyumba

bure, chakula bure na blanketi na shuka bure ajiandalie mahali pa kukaa. Hakuna kitu kitakachomletea heshima binadamu kama kuwa na mahali pa kukaa.

Askari wengi wa vyeo vya chini katika majeshi yote hawana namna ya kuishi baada ya kustaafu. Sasa tunaliabisha jeshi, tunaaibisha pia hata Serikali yetu na nchi yetu. Askari wanajeshi hawa, wanajua matumizi ya silaha, sasa ni rahisi kuchukuliwa na hawa majambazi, wanasema wewe ni mtaalam twende.

Kuna kesi mbalimbali ambao vijana wetu wamo ndani ya majeshi na wengine ambao wamestaafu ndani ya majeshi, wanatumika katika kazi hizi za ujambazi. Ni kutokana na hali halisi kwamba hawana maandalizi ya maisha. Ni vijana ambao wanakaa katika makambi, hawana namna ya kufanya biashara, hawana namna ya kufanya kazi nyingine zozote kutokana *Force General Orders* ambazo wanazitumikia. Wewe na bunduki wewe na lindo, wewe na kazi nyingine, biashara ya aina yoyote ile. Hivi sasa tu labda pengine masharti kidogo yamelegezwa, utakuta katika kambi kuna ka-*kiosk* anauza soda, anauza sigara, anauza biskuti. Lakini kazi hasa ya kumletea matumizi mengine au fedha za ziada kujenga maisha yake hamna. Hata hii sijui imelegezwa legezwa vipi kwa sababu zamani utakuta Kambi A safi kweli kweli.

Lakini kwa sababu ya hali ngumu ya maisha labda ndiyo maana tumekubaliwa kuweka vioski katika makambi yetu. Lakini maandalizi, kama sio leo lakini natoa kama tahadhari, tuanze sasa kuifanyia kazi. Huyu askari anaweza kukaa miaka 10 katika jeshi bado yeye ni *private.* Pengine baada ya miaka 12 atawekwa yeye ni *pensionable*. Anataka kuondoka, hana maandalizi, lakini kazi aliyoifanya katika miaka ile akiwa ndani ya jeshi ni ya thamani sana kwa ulinzi katika nchi yetu kwa mmoja mmoja na hata kwa nchi kwa ujumla. Sasa hii thamani naomba tuiweke katika thamani. Thamani ya kazi zao tuiweke katika thamani ya maisha yake ya baadaye, tuwasaidie vijana hawa, lakini to *enforce discipline* na wakati huo huo tuangalie hatima yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hayo, kwasababu nilikuwa katika Mkoa wa Majeshi, kichama wakati ule, niliona *discipline* ilivyokuwa inakwenda. Sasa naanza kusikitika sana sijui Mkoa wa majeshi tuurudishe? Au kwasababu ya vyama vingi, lakini ninaomba sana vijana hawa tuwatazame kwa macho mawili, tuwatazame kwa huruma hatima yao, lakini bado tu-*insist discipline.*

Mheshimiwa Spika, *Collection* ya kuingiza vijana katika majeshi inaanza kutugharimu sisi wenyewe kutokana na hayo wanayoyafanya wale wachache ambao hawana nidhamu na wale wachache ambao wanataka utajiri wa haraka haraka na kuonekana kwamba yeye ni jeshi. Hatutaki kuonyesha kwamba wewe ni jeshi, wewe ni mtumishi katika jeshi. Usiuvae ujeshi ukadhalilisha wengine, dhamana hii mmepewa na wananchi wote na ndio maana mkaitwa Jeshi la Wananchi. La sivyo, tungesema tu Jeshi la Ulinzi, yakaishilia mbali. Lakini mthamini tafsiri ya Jeshi la Wananchi na kazi ambayo imefanyika na nidhamu ambayo mnatakiwa kuionyesha kwa wananchi ili waendelee kuheshimu na kuwaenzi na kuwatetea mahali popote mtakapoonekana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakushukuru sana na ninaendelea kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. ANNA M. ABBDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nami nichangie hoja hii aliyoitoa Waziri wa Ulinzi. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake. Pia nampongeza kwa lugha aliyoitumia katika hotuba hii, ameeleza mambo mazuri, lakini anajua kabisa haya mambo mengine hayajatimia, lakini ameyaeleza kwa uzuri sana. Kwa hiyo, sisi ndio tuna wajibu sasa wa kuyaeleza yale tunayoyaona kwamba pengine alitumia lugha nzuri, lakini kulikuwa labda na uzito unaofuatana na yale aliyoyasema.

Kwanza, pia naipongeza Kamati ya Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama. Imefanya kazi nzuri sana tena sana. Ninawashukuru sana. Hata yule Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwasababu tunaye kwenye Kamati ile, mengi aliyoyasema, tumeyashughulikia kwenye Kamati. Naomba kushukuru sana kwamba Kamati hii imefanya makubwa. Hata hiyo posho ya Sh. 5,000/= inayosemwa leo, imeanza Aprili mwaka huu kwa juhudi ya Kamati. Kwahiyo, tukitoka hapo tunaendelea na juhudi nyingine, lakini watu wasifikiri kwamba ilikuwepo tangu zamani, sio kweli. Ni juhudi ya Kamati iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Kamati, tumeelezwa kwamba kwasababu ya kubatilisha matumizi ya Kanuni ya Pensheni za Majeshi na Ulinzi, wale ambao wamefanya kazi baada ya muda wao wa kustaafu na wakaamriwa kwa mujibu kabisa wa taratibu za kijeshi kuendelea na kazi, kuna deni la shilingi takribani milioni 432, limeshafanyiwa hesabu.

Ndio kusema Wizara inajua watu wale ni watu gani, wangapi na kila mmoja anadai kiasi gani. Sisi tungependa kujua, lakini hili sio la Wizara hii, pesa hizi ziko Hazina na tunai-*address* Serikali, mtujibu, hizi hela zinapatikana lini? Kwasababu sasa hivi tunasema haya kwa ajili tu tunazungumzia mbele kwenye Wizara inayohusika, lakini Wizara hii kazi yake imekwisha. Imekwishasema, jamani eeh, kwa kubatilisha. Aliyebatilisha hii ni Amiri Jeshi Mkuu. Sasa kama Amiri Jeshi Mkuu amebatilisha hii Kanuni, maana yake kinachofuatia ni hizo fedha zitoke. Sasa mimi sijui katika Serikali tunaendeshaje mambo. Amiri Jeshi Mkuu, amesema ameshabatilisha, Wizara imeshasema kuna fedha kiasi fulani kinatakiwa, tungependa kujua fedha hizi zitatoka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba hapa Wizara inaomba hela hizi, zinaonekana ni nyingi sana, Shilingi bilioni 443, Shilingi milioni 340 na ushee, zinaonekana nyingi sana; lakini kuna jambo moja ambalo tumelisemea, halijapata majibu. La kwanza, ni fedha nyingi kati ya hizi zinakwenda kwa wale wakubwa wa Jeshi, Wastaafu, Majenerali, hela zao ziko humu. Mbona wengine tulistaafu! Mbona mimi hela zangu haziji Bungeni, zile za ustaafu wangu?

Mimi nilikuwa mtumishi huko nyuma, nika-*qualify pension;* nilikuwa Serikalini. Samahani sio Bungeni. Bungeni sasa hivi napata *gratuite*, lakini nilikuwa Serikalini. Hela yangu haipitii kwenye Wizara nilikoondokea, hela yangu inapitia *Treasury*. Ni kwanini hawa wanajeshi inakuwa hivi? Maana yake inajulikana wanahitaji kiasi gani, pelekeni *Treasury* ili hawa fedha zao zionekane zinakwenda kwenye shughuli za jeshi.

Kwa kweli tunawapa shida kubwa sana, kwamba wanawahudumia wale, halafu hata wastaafu wale wengine wa kitaifa, kwa mfano wastaafu Marais, mbona wanashughulikiwa na Ofisi maalum na Waziri alitujibu hapa kwamba yeye anao 12 tu. Lakini hela zao pia wanapata, lakini mimi nasema tunawapa shida sana jeshi. Tunaomba fedha hizi za wastaafu wale wakubwa, zipelekwe moja kwa moja *Treasury*, ama mkiwapa hawa, basi isiwe ni sehemu ya bajeti yao ili wao bajeti yao itumike tu kwa mambo ya ulinzi. Hilo ndilo ambalo mimi ningependa kulisisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kurudisha *JKT* kwa mujibu wa Sheria, lakini sasa tunaomba nayo Serikali iiwezeshe *JKT*. Hapa Kamati inasema kuwa na uhusiano mkubwa sana na *VETA*, tunataka vijana hasa hawa wa kiwango cha chini cha elimu, acha wale wanaokwenda kwa mujibu wa sheria, watoke pale wana vyeti vya *VETA* kama ni kilimo ana cheti cha *VETA*, kama ni ufundi wa kushona ana cheti cha *VETA*. Huyu ukishamwezesha na ufundi ule, atakwenda kuutumia uwezo huo na ujuzi huo huko nje. Sio sio lazima aajiriwe! Atajiajiri mwenyewe kwasababu ni fundi.

Kwahiyo tunaomba sana jambo hili. Mimi nakubaliana na wenzangu waliotangulia kwamba kilimo kwanza ni pamoja na *JKT* kuonyesha mfano, tena pale tuna watu wenye nidhamu, wanaamka kwa nidhamu, watakwenda kufanya kazi kwa nidhamu, kila kitu kwa nidhamu, mpaka wanamaliza siku. *Production* kama tunataka ya mfano twende *JKT* na baadaye Magereza, nao wana nafasi nzuri ya kufanya kazi hii. Tunaomba sana wawezeshwe; kwa mfano pale Ruvu maji yapo, hebu wapeni kazi ya kufanya kama umwagiliaji pale mwone, watatoa mbegu yote tunayoihitaji nchini hapa, watatoa chakula chote tunachohitaji, watafuga, watatoa mayai ya kutosha Dar es Salaam. Kwa hiyo, hili jambo hatulifanyi, tunaachia achia tu, hapa uwezo tunao mkubwa sana. Kwahiyo, mimi ningeomba sana Serikali iwawezeshe hawa jamaa wafanye kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri amezungumzia ulinzi wa bahari, hapa ndipo namsifu sana kwa lugha. Hivi ni ulinzi gani wa bahari? Kwasababu hata mafuta ya kuendesha kile chombo, nadra, hayapo, eeh! Kwa hiyo, jamani, tunachukulia mambo haya ya ulinzi kama sijui ni kwa utani utani tu! Kilimo kwanza, mimi nakubaliana na waliotangulia. Hakuna kilimo wala amani, wala utulivu. Kama hatutaimarisha majeshi yetu kwa kuwapa vifaa, nyenzo na kila kitu kinachohitajika; hapa sizungumzii tu Jeshi la Ulinzi, nasema Polisi, Magereza, wote. Mimi nasema tusisikilize sana mambo ya *IMF*, Shirika la Fedha la Dunia, mnataka vipaumbele; jamani amani, utulivu, usalama, ndio mtaji wa kilimo kwanza.

Mimi ninasema vijana wetu wanafanya kazi nzuri sana, lazima maslahi yao yaendelee kuboreshwa. Lakini yapo mambo ya lazima kwa vijana hawa wanaotufanyia kazi ya ulinzi. Kwanza, wasiwe na malalamiko, hasa ya stahili zao, kusiwe na

malalamiko. Sasa sina hakika kama hizi shilingi bilioni 400 tulizopewa ni pamoja na kulipa madeni yao, sina hakika. Naomba Waziri anithibitishie kama tutalipa madeni yao yale ya nyuma, kuna madeni, huku tumesema mengine ya nyuma yalipwe yachukuliwe na *Treasury*, tunataka *commitment* ya Serikali kwamba madeni haya yachukuliwe kweli na yalipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la maji na umeme, kuna tatizo. Nasikia Waziri Mkuu alikwishakulishughulikia tatizo hili akawaita wanaohusika; sasa tunachoomba wawekewe mita kila mahali, ndio utaratibu, haya mambo ya kukadiria nayo ni magumu, ndio tatizo linalotokea. Maji wanakadiriwa, umeme wanakadiriwa, sasa hata kukadiriwa kwenyewe unatakiwa uende ukasome, uende mle ukakadirie. Kwa kweli tena wanakaa ofisini, nasikia huko ofisini wanakadiria matumizi ya umeme. Hili nalo linaleta ugomvi kati ya wale wanaotoa huduma na wale wanaotumia hii huduma.

Tunaiomba Serikali ishughulikie suala hili wawekewe mita, wahakikishe kwamba kuna mita inasomwa na Jeshi litalipa umeme au maji kwa kadiri walivyotumia. Hapo ndipo tunaweza sasa tukafanya mambo ambayo tunaweza kusema nani hakutimiza wajibu wake. Kwa kweli hili jambo mimi sielewi ni kwanini? Kwasababu hata sisi wengine tulipokuwa tunapata umeme au simu bure, au nini, wakawa wanatubambikizia bili. Kwa hiyo, hawa wengine wanabambikiziwa. Tunaomba hili lirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nangependa kuzungumzia jambo moja. Mimi nathamini sana uhuru wa kila mtu kusema humu ndani na hasa inapokuwa ndio haki yetu. Kwa hiyo, kila mtu avumilie yale mwenzake anayosema. Kuna siku moja wiki iliyopita, niliamsikia Mbunge mmoja anasema, namheshimu sana Waziri Mkuu, lakini kwa hili moja la kumtetea Mkapa, aah! Haa! Hiyo sio utamaduni wetu, maana yake umeondoa heshima yako yote kwa Waziri Mkuu kwa hili. Afadhali hata usingesema, wewe ungesemea la kwako tu, lakini kusema simheshimu Waziri Mkuu kwa hili moja, kwa kweli hapa aah, heshima yangu inakuwa ya mashaka mashaka, sio jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nikasikia mwingine anasema kwamba aah, anayetaka kumtetea Mkapa aende Mahakamani. Sasa mimi nikisema na hata anayetaka kumshitaki aende Mahakamani ili mtu anayependa aende akamtetee. Hili jambo tutakuwa tunabishana hapa kwasababu gain? Mimi nasema kama kuna mtu anamtetea Rais mstaafu - Mheshimiwa Mkapa, mwache aseme na wewe sema yako, lakini usianze kumsema mwenzio anayemtetea. Mimi nasema hili nalo linakuzwa. Leo nimesikia kuna gazeti linasema, hao wanaomtetea, sijui kitu gani kitu gain; sasa tukisema na ninyi mna uhusiano na wale wenye magazeti, mtasema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema, utaratibu mzuri ni mtu aseme hapa anavyoona inafaa. Lakini tusihukumiane kwa mtu anavyotaka kusema. Baada ya kusema hayo naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kushiriki kwenye mjadala huu mzuri. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi

la Kujenga Taifa kwa hotuba yake nzuri. Lakini nimshukuru kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara yake, Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania na JKT. Namshukuru yeye, Naibu Waziri, Makamanda wote na wapiganaji wote.

Pili, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza msimu huu kuzungumza, nitoe rambirambi kwa wenzetu ambao wamepoteza maisha yao katika kipindi hiki cha mwaka huu uliopita na pia niwapongeze Wabunge wapya, akiwemo ndugu Charles Mwera – Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale - Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba - Mbunge wa Busanda, kwa ushindi ambao ameupata na huenda leo tukapata nyongeza ya Mbunge wa kukamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kwa kusema kwamba Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania ni Jeshi lenye historia iliyotukuka, kama ulivyosema leo asubuhi. Lina historia iliyotukuka, limefanya kazi nzuri ndani ya nchi yetu na katika Afrika. Nchi yetu tunasema ni kubwa, lakini nchi ndogo katika dunia, lakini mambo yetu ni makubwa. Katika taasisi ambazo zimeweza kuonyesha kwamba Tanzania mambo yake ni makubwa, ni Jeshi la Wananachi wa Tanzania. Sote tunajivunia jeshi letu. Wengine tumepata bahati ya kufanya kazi kwa karibu zaidi katika historia yetu, tumefahamiana na baadhi ya Makamanda na wapiganaji, ni watu safi sana.

Sasa niseme dogo tu; ni kwamba nguvu ya Jeshi ni nidhamu kwasababu nidhamu ndio inajenga mshikamano wa fikra na vitendo. Sasa huko nyuma tuliweza kutofautisha nidhamu tukisema kwamba kuna aina mbili za nidhamu. Kuna nidhamu ya uwoga na kuna nidhamu ya kujituma. Sasa nidhamu ya uwoga inaweza kuwa na nguvu sana, sio tu katika Jeshi, katika mambo mengi tu ambayo ni ya *organizational*, ya kimfumo. Tatizo lake ni kwamba kama kile chanzo cha uwoga kinatoweka toweka mambo yanaparaganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nidhamu ya kujituma ambayo wenzetu kiingereza wanaita *Self Imposed Discipline*, ile inatoka ndani baada ya kuelewa kwanini, huhitaji tishio. Ndio maana wakati ule sisi tulitia nguvu sana suala la uzalendo na siasa katika mafunzo ya majeshi yetu. Kazi hiyo ilikuwa inafanywa na makamisaa. Sasa tumetoka kwenye chama kimoja, tuko kwenye vyama vingi, hakuna chama ndani ya Jeshi na tulikubaliana. Wewe unafundisha siasa, ni lazima mwelewane juu ya siasa gani mnafundisha. Hamwezi kupeleka siasa ya *CCM* wala ya chama kingine chochote; ndio maana tukatoa kila kitu na sheria ipo. Lakini ni lazima watu wawe na nidhamu ya kujituma. Kwahiyo, msingi wake ni lazima uwe uzalendo. Sasa iko kazi ya kuufuma ule uzalendo uweze kufika mahali uwafanye watu wawe na nidhamu bila kutetereka.

Sasa nasema wenzetu wamemudu sana maana yake bado Jeshi letu ni imara, lakini yanatupa taabu sana kwenye shule, maana yake ni lile lile, kwenye shule zetu, kwenye vyuo, katika sehemu nyingine, kilichokuwa kinatufanya tushikamane zaidi ilikuwa ile sura ya siasa. Sasa vyama vingi sura ile ya siasa imepungua, hatujaweza kukaa na kuweka uzalendo lakini katika sura pana; elimu ya uraia yenye sura pana. Kwa hiyo, hiyo mimi nilidhani ni changamoto ya kwanza. Wenzetu wa majeshi watafakari zaidi, waweze kuimarisha zaidi kusudi Mheshimiwa Ntimizi isije siku moja akaja akalia hapa.

Lakini sote tunatakiwa tutafakari ili katika kila taasisi hasa ya watu wengi tuweze kuona tutakabili vipi suala la kujenga nidhamu ya kujituma badala ya kuwa na nidhamu ya uwoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema la pili kwa kifupi tu. Wakati fulani hapa tumeambiwa Bungeni kwamba mwakani tunakusudia, Serikali imetoa tamko, kurudisha JKT na watu wamepokea kauli ile na wamefurahi. Kwasababu watu wengi wanafikiria kwamba katika matatizo ambayo tunayapata sasa ni kwasababu tulisitisha utaratibu wa Jeshi la Kujenga Taifa; vijana wetu hawana mahali pa kutengenezwa pamoja.

Sasa nasema mimi vilevile natarajia tutaifanya kazi hiyo ya kurudisha Jeshi la Kujenga Taifa, lakini ni lazima tujiandae kwasababu mazingira nayo yamebadilika sana. Kwanza idadi ya vijana wa mujibu wa sheria ni wengi kweli kweli! Wanaomaliza *Form Six* ni wangapi? Wanaomaliza *Form Four* na kwenda kwenye kozi mbalimbali za *Diploma* na kadhalika ni wangapi? Wanaomaliza Vyuo Vikuu ni wangapi? Kwasababu sasahivi tuna wanafunzi kwa mwaka huu unaomaliza, karibu 82,000 hapa ndani ya nchi. Tunapofikiria kuurudisha utaratibu huu wa *JKT* ni lazima kujiandaa kweli kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ni lazima kujiandaa juu ya ni nani atakuwa ni mfundishaji? Sio ufundishaji tu wa mambo ya *military science,* ni lazima kufikiria makamisaa wa aina mpya. Mimi nilirudishwa, mwalimu alinirudisha kutoka Algeria. Nilikuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Afrika, Makao Makuu yangu yalikuwa Algeria. Nilirudishwa ili nije kuwa Kamisaa wa *JKT* kukabiliana na hali kwasababu vijana wako kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, *Form Six,* Vyuo Vikuu, wanauliza maswali hawapati majibu. Mwalimu akaniita kutoka Algeria ananiambia bwana, huko nataka uende uwajibu wasomi wale, kazi kweli! Sasa maelfu sasa hao wasomi. Kwahiyo, ni lazima maandalizi yafanywe kweli kweli! Halafu mazingira yamebadilika, kuna ugonjwa wa *UKIMWI.* Jeshini kule wanakwenda wanawake na wavulana, wasichana na wavulana katika mazingira mapya, nidhamu yake inatakiwa ifikiriwe vizuri. Kwahiyo, nasema hilo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ulinzi wa mgambo. Mimi ndiye niliyetumwa kuanziasha ulinzi wa mgambo Dar es Salaam mwaka 1971. Katibu wetu na ndiye Mtendaji Mkuu alikuwa *General* Msuguri, wakati ule Kanali wa kikosi cha tatu pale Lugalo. Tumefanya naye kazi ya kuanzisha Mgambo na unaitwa ulinzi wa mgambo, wengine siku hizi wanasema Jeshi la Mgambo.

Namshukuru sana Waziri, hotuba yake safi, lugha safi, hakusema habari za jeshi. Hakuna jeshi la Mgambo, ni mlinzi wa mgambo. Nao vile vile msingi wake ni uzalendo, ingawa ulinzi wa mgambo sio kwa ajili ya kutafuta kazi. Kwamba watu fulani wanatafuta walinzi wa shughuli zao za biashara zao, wale watu wanatufuta wafanye ulinzi wa mgambo ili waende kupata kazi, hapana. Mimi nadhani tufanye kazi vilevile wale Makanda wa Mgambo, ambao ni ma-*DC* na ma-*RC* wafanye kazi ya ukamisaa. Suala

zima kubwa la ulinzi wa mgambo, ni wananchi kuungana na majeshi kulinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili namimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ya mwaka 2009/2010. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake na niipongeze Serikali kwa maandalizi ya bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda pia niipongeze Wizara, Jeshi la Wananchi, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda nchi yetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu katika bajeti ya mwaka 2009/2010, naomba nitangulize kilio na ombi la wananchi wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Arumeru Magharibi. Hivi karibuni katika miaka ya karibuni, kumekuwa na utata wa mpaka kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambalo ni Jeshi letu na wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi, hasa Kata tatu za Mlangarini, Nduruma na Moshono. Katika Jimbo langu la Uchaguzi la Arumeru Magharibi, tuna Kambi tano za Jeshi la Wananchi wa Tanzania ikiwemo Oldonyo Sambu, Oljoro (kuna kambi mbili, Nengung’u na *Packers).*

Hivi karibuni kumekuwa na mzozo kati ya mpaka wa Jeshi la Wananchi Kambi ya *Tanganyika Packers* na wananchi karibu 60,000 wa Kata ya Mlangalini, Mushono na Luluhumo. Hivi karibuni mwaka huu Jeshi la Wananchi limeweka mabango na kukata mipaka mipya kwenye maeneo ya wananchi. Nasema kwenye maeneo ya wananchi kwa sababu hawa wamekuwepo pale tangu miaka mingi sana karibu miaka 40, 50, 60, karibu umri wangu wote, wako pale mpaka wakati Kambi hiyo ya wanachi wa Tanzania ya sasa ikiwa mali ya *Tanganyika Packers* wananchi hawa
wako sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, shida sasa ni kwamba wananchi wameambiwa wasifanye maendeleo ya aina yoyote wala wasishughulike na ardhi ile ambayo imechukuliwa ama imekuwa *annex* na jeshi kwa kufuata mipaka mipya ya mabango mapya waliyoweka miezi miwili iliyopita.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kabisa unyeti kabisa wa ulinzi wa nchi yetu, nafahamu unyeti wa jeshi letu la Wananchi wa Tanzania lakini bado linabakia ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ombi la hawa wananchi wa Arumeru ambao wamenituma hapa ni kwamba wanaomba jeshi libakie kwenye sehemu waliyoko ya *Tanganyika Packers* nao waendelee na shughuli nyingine za maisha kwa kutumia ardhi yao na kutumia miundombinu ambayo wamejijengea kwa miaka hiyo yote ya wao kuwepo katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inafahamu jitihada tulizofanya kwenye ngazi ya Wilaya, ngazi ya Mkoa, ngazi ya Wizara na hata Ofisi ya Waziri Mkuu. Kuhusu jambo hili, wananchi wa Arumeru wanaomba Serikali iamue moja kati ya mawili. Wananchi hawa waonyeshe mahali pa kwenda na wapewe fidia zao au wabakie na mipaka hii ya sasa na waendelee kuishi. Sasa hivi kuna hali ya wasiwasi, hofu na kutokuaminiana, amani inaweza kuvurugika. Nasema inaweza kuvurugika kwa sababu wananchi ni wanyonge, jeshi lina mabavu, lakini hatujafikia hapo. Lakini ni vizuri Serikali iondoe hali hii iliyoko kati ya wananchi na jeshi lao la ulinzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba sasa nichangie katika hotuba ya bajeti kuhusiana na dhana ya ulinzi, majukumu ya ulinzi wa nchi yetu na taifa letu. Mipaka yetu bado imebakia ni ile ile ya siku zote, lakini majukumu haya katika wakati huu wa sasa yamepanuka na yamechukua sura mpya ambayo ni lazima tukae na kutafakari. Ukiangalia vitendo vya uovu ama maovu kama yalivyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ikiwemo sasa hali mpya, uovu mpya wa uharamia wa mabaharia kuteka meli za nchi mbalimbali za mataifa mbalimbali kitu ambacho huko nyuma hatukusikia. Somalia iko karibu sana na Tanzania, ni mdomo na pua, hii inafanya jukumu hili la ulinzi liwe pana na liwe kubwa. Tukitazama uvuvi haramu unaoendelea katika mipaka katika bahari yetu, hii imepanua tena dhana na jukumu hili la ulinzi katika nchi yetu, nisitaje au nitaje kwa kifupi tu uhamiaji wa haramu katika mipaka yetu inayotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upana ama uzito wa majukumu haya sasa hivi ni lazima nchi yetu ijipange upya na kulitizama jeshi letu kwa upya kabisa, jeshi letu lipewe nguvu ya kulingana na uzito wa majukumu yaliyoko sasa, majukumu ya ulinzi kama nilivyotaja. Lakini nguvu mpya ya kwanza ya kupewa jeshi nashauri Serikali itazame upya mafao ya walinzi wetu, vyombo vyote hivi vya ulinzi leo tunazungumzia jeshi, tukija kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani tutazungumzia Polisi.

Ni vizuri sasa tujue kwamba wanajeshi wetu wana motisha gani? Wanapewa nini? Mafao yao ni nini? Mimi nimeshangazwa kidogo niliposikia kwamba wanajeshi wetu tunawapa posho ya Sh. 5,000/= kwa siku ni kweli sungura mdogo, ni kweli kabisa sungura mdogo lakini Sh. 5,000/= haiwezekani. Sh. 5,000/= kwa mwanajeshi ambaye umemfungia kwenye *barracks* au mwanajeshi hata kama hayuko kwenye *barracks* yuko nje mwenye familia Sh. 5000/= ni kiwango cha chini kabisa. *(Makofi)*

Kama mtikisiko wa uchumi duniani umeleta tafsiri ya kwamba kuna sehemu ambayo tusaidie lazima Serikali iokoe. Nafikiri hapa pia kwenye Jeshi la Wananchi kwenye ulinzi wa nchi yetu, huo mtikisiko unafika huko ni lazima tuangalie kwa upya kabisa viwango vya posho, viwango vya mishahara, hatimaye viwango vya pensheni zao zinakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama sasa hivi uovu mkubwa unaoendelea nchini kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyosema, unakuta baadhi ya wahalifu, baadhi ya majambazi wanakuwa wametoka kwenye vyombo hivi vya dola, watu wanaojua kutumia silaha. Nini kinachowapeleka kule? Ni kwa sababu ya hali ngumu ya maisha.

Wakiondoka hawakuwa wamefanyiwa maandalizi yoyote, nao ni watu muhimu katika jamii wanakwenda kutumia ujuzi ambao tumewapa ambao jeshi limewapa kwa kufanya vitendo viovu.

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa kiwango hiki cha *allowance* cha posho hasa posho ya kila mwananchi wetu itizamwe, *then* tutizame mishahara yao. Mimi nafikiri hilo ni muhimu sana. Lakini kwa upande mwingine napenda tu kusema kwamba kutokana na uzito wa majukumu haya ya ulinzi ya sasa tunataka zana mpya, teknolojia mpya, mafunzo mapya kwa walinzi wa nchi yetu. Ni vizuri Serikali ikafahamu hiyo na ni vizuri tuishauri Serikali iwapatie wanajeshi wetu zana za kisasa za kupambana na maovu yanayoendelea kwa mfano katika huu uhalifu wa uvuvi haramu, nafahamu meli iliyotumika imekodishwa ama imeombwa mahali.

Mheshimiwa Spika, kama tutataka kupigana na maovu haya ambayo sasa yamechukua sura mpya na uzito mpya ni lazima tuwe na zana na mafunzo yanayolingana na uharibifu na maovu yanayotendeka sasa hivi kwenye jamii. Kwa hiyo, ni lazima tuwape jeshi letu fedha za kutosha za kuweza kununua vifaa hivyo na kuendesha mafunzo na kuleta teknolojia mpya katika Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mara nyingi sana Serikali imekuwa inajaribu kusema kwamba wataanzisha Jeshi la Kujenga Taifa. Hili ni jambo zuri, linaongeza ajira, inaongeza ukakamavu, inaongeza na nguvu ya Jeshi la Wananchi wetu ama vyombo vya dola. Lakini mimi ninasita kuamini tamko la Serikali kwamba Jeshi la Kujenga Taifa litaanzishwa mwakani kwa sababu Serikali imekuwa inasema hivyo hivyo mara kwa mara na wameshindwa kutekeleza. Sasa katika hili ningependa kushauri kwamba Serikali ijiandae na kutoa fedha za kutosha kwa jeshi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. COL. SALEH ALI FARAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi asubuhi hii au mchana huu wa leo ninakushukuru kwa kupata nafasi na mimi nichangie machache katika bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi. Kwanza sina budi kumshukuru au kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu kwa jinsi anavyoliendesha jeshi letu lililojaa nidhamu na utii mkubwa sana. *(Makofi)*

Vilevile, sina budi kumpongeza Waziri wa Ulinzi kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa asubuhi ya leo sina budi kuwapongeza wataalam wake, sina budi kuwapongeza wakuu wangu wa Jeshi waliobakia sasa hivi pamoja na wataalam wao wanaofanya kazi. Vilevile sitawasahau askari ambao wanafanya kazi ngumu, askari wote wa vyeo vya chini au sisi tunaita *other ranks. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi ningependa niende kidogo chapu chapu katika yale ambayo nimefikiria kuyasema. Jeshi kama jeshi kwa kweli linatakiwa litazamwe vizuri ili liweze kufanya kazi inayotakiwa na jeshi tukilitizama ni *institute* iliyowekwa pale kwa kazi za dharura. *Institute* yenyewe ya dharura na kwa kazi za dharura, kwa hivyo lazima litizamwe vizuri na lenyewe liwe na wataalam ambao wanaweza wakakabili hizi hali kwa wakati wote na kwa ustaadi mkubwa sana. Kwa hiyo,

kwanza sina budi mimi kupongeza na katika kupongeza huko kama ningepata nafasi ningejaribu kutoa mfano, lakini sidhani kama nitapata huo muda.

Kwa kweli suala zima la Mbagala, Mbagala sina budi kupongeza Jeshi kwa taarifa nilizozipata, kazi nzuri iliyofanyika kuweza kuhifadhi au kutazua tatizo lililotokezea haraka kama ilivyokuwa imetokea. Sio kazi nyepesi kwa muda wa masaa matano kunatokezea vurugu ya milipuko halafu raia wanakimbia askari mpaka wastaafu kadri nilivyopata taarifa mimi walikuwa wanakimbilia kambini kuona kuna nini ili waweze kusaidia.

Kwa kweli ni moyo wa ajabu sana. Hali ilikuwa tete, hali ilikuwa haiwezi kukamatika, lakini ninashukuru uongozi wa ngazi za juu umeweza kuikamata hiyo hali na kuirejesha katika unafuu ambao sasa nafikiri tutangoja ripoti kusikiliza kitu gani kitakachoweza kufanyika baada ya kupata ripoti kamili kuhusu hilo. *(Makofi)*

Kwa kweli ninachoomba tu ni kwamba makamanda wetu wawe wajasiri zaidi, kwa mara nyingi ikitokezea tatizo kama hili ili waweze kuweka hali nzuri zaidi. Mimi hili naliita ni tatizo au dharura ya tatu katika *experience* yangu ya jeshi. Kwanza, vita mimi nilikuwa naita ni dharura iliyojitokeza tukapigana na Idd Amini. Ile ilikuwa ni dharura na ilikuwa ni kazi ya jeshi, tumetekeleza kwa ufanisi mkubwa mpaka kumshinda Amini na kuondoka. Kwa kweli sidhani kama ndani ya Afrika, kama kuna jeshi lililofanya kazi kubwa namna hiyo. Hili jeshi lilinolewa ndiyo maana likafikia hapa. *(Makofi)*

Dharura nyingine ambayo mimi naikumbuka ni wakati wa vita ambapo tuliziangusha ndege zetu sisi wenyewe, ile ilikuwa ni dharura kubwa sana. Lakini jeshi liliweza likadhibiti kazi ile na tukaendelea vizuri. Dharura ya tatu hii nayo ambayo ninaipongeza, kwa hiyo kwa hilo ndiyo lilikuwa langu la kwanza nijaribu kutoa pongeza na kutaka mambo yazidi kwenda vizuri. *(Makofi)*

Sasa kuna suala moja ambalo nilikuwa naliona niliingie kwa namna ambayo wakati nasoma *history* vita ya kwanza na vita ya pili vya dunia jinsi Hitler alivyofanya na hii ipo katika kilimo kwanza.

Kilimo kwanza nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri kama tutaweza kushirikisha kiwanda cha nyumbu kiweze kutengeneza *power tiller* hili litakuwa ni jambo zuri sana. Kwanza watapata *experience* hawa watu halafu kazi zitakuwa zimefanyika kwa nidhamu ya kijeshi na *power tillers* zitakuwa kwa sababu itakuwa katika *line of production* ambayo itaweze kusaidia maisha ya kiraia na itaweza kusaidia maisha ya jeshi ya baadaye. *(Makofi)*

Hili suala nilikuwa naliona lingefikiriwa vizuri zaidi. Vilevile sijaacha kuwafikiria JKT nao wakipewa nafasi ya kuzalisha au wakipewa nafasi ya kufundisha kwa viwango vya *VETA*. Vilevile nilikuwa nina wazo lingine moja kwa upande wa Jeshi letu. Hivi karibuni tulipata maafa na hii nilikuwa naizungumzia itakuwa kwa pande zote mbili za Muungano. Ndani ya nchi yetu kuna maziwa na kuna bahari kuu, Zanzibar

mwezi uliopita palitokea maafa makubwa sana ile meli ambayo ilichukua watu ikazama au ikadidimia bandarini wakati imefungwa kamba kwa kweli yalikuwa ni masikitiko makubwa sana. wengine walikuwa wanasema wanavyoweza kusema.

Lakini pale ndiyo mimi niliona unyonge na umaskini unavyoikabili nchi. Nilipokonyoka kidogo nikaenda pale kuangalia, kwa kweli hali ilikuwa inasikitisha. Sasa mimi nilikuwa naomba ndani ya taratibu za jeshi katika kuendeleza harakati hizi za dharura, kuna kikosi au kuna *unit* inaitwa *search and rescue.* Hii inasaidia wakati wa maafa uraiani, hiki kikosi hatuna. Ningeomba kianzishwe rasmi ili kiweze kuchukua nafasi yake ndani ya jamii. *(Makofi)*

Suala la jeshi, watu huwa wanafikiri ya kwamba tunangojea au wanajeshi wamekaa wanangojea vita, lakini vita vinapigana wakati wa amani ndiyo panapopigana vita vikubwa kutayarisha majeshi yenu, yawe tayari na vilevile kuhami wananchi wetu jinsi itakavyokuwa wakati wa amani na wakati wa vita jeshi ndiyo linarudisha wananchi nyuma kwa usalama wao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama hakuna vikosi maalum tutakavyovianzisha sasa kwa makusudi mimi naona tutapata taabu. Kwa hiyo, ni vyema tuwe aidha, *nevy* yetu na *Police* M*arine* na nini tuanzishe *coastal marine* ambayo itaweza kukidhi haja ndani ya bahari na ndani ya maziwa tuliyokuwa nayo. Hili ni kubwa sana, nilikuwa najaribu kulifikiria, nafikiri kwa nafasi niliyopata na wenzangu wote kujaribu kunifilisi kwa sababu nilikuwa na *points* kama sita za kuzungumza haya, naona yanaweza yakatosha kwa mchango wangu wa leo kama mmojawapo wa Wabunge wa humu ndani. Ahsante nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Col. Farah. Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye aliyekuwa mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu na pia ndio wa mwisho kwa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Kwa hiyo, tutakaporejea saa kumi na moja tutasikiliza majumuisho kwanza kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi kwa dakika 20, jumla wanazo dakika 45 na dakika zilizobaki ni kwa ajili ya Mheshimiwa Waziri mtoa hoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge nilikuwa nimepata maombi ya ufafanuzi ya maandishi kutoka kwa Mbunge mmoja ambaye aliisoma nyongeza ya pili ya kanuni zetu inayozungumzia utaratibu wa uteuzi au uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda kwenye vyombo vingine vya uwakilishi. Sasa yeye amesoma kwenye ukurasa wa 96 pale kwamba tukiwa na mmoja inabidi tupige kura ya ndiyo au hapana, ndivyo yeye anavyosema.

Waheshimiwa Wabunge, ukweli nyongeza ya pili inahusu uwakilishi katika vyombo vingine vya uwakilishi vilivyo nje ya Bunge. Kwa hiyo, tafsiri Tume ya Huduma sio nje, Tume ya Huduma ni sehemu ya Bunge, ni Tume yetu sisi. Pale aliposema kwamba neno Tume linatumika kwenye kanuni sehemu ya kwanza ya hiyo nyongeza ya pili kwenye kifungu cha kwanza kinazungumzia Tume ya Bunge.

Tume ya Bunge inayozungumzwa hapa sio Tume ya Huduma za Bunge iliyopo kwenye kanuni ya tatu, hii ni Tume ambayo itachaguliwa na Tume kwenda kufanya kazi

mahsusi nje ya Bunge.  Mathalani kuna suala linahitaji mbali ya Kamati Teule, Bunge linaruhusiwa kuteua Tume yake kulifuatilia jambo fulani. Sasa hapo kura zikifungana ndiyo tunapiga au akipatikana mmoja basi tunapiga kura ya ndiyo au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho kabisa, mambo haya yanatoka tu kwa Mwenyezi Mungu, huwezi kwa kweli hata ufanyeje. Mambo mengine ndiyo tukubali hali iliyojitokeza kwa sababu hata tafsiri ya jambo hili limetukuta katika uchaguzi.

Kwa mfano, Mbeya Vijijini wenzetu CHADEMA waliweka mgombea mwanasheria mahiri, hakutazama vizuri sheria, sheria inasema anayeruhusiwa kufanya kuwa shahidi ni Hakimu, lakini kisheria katika nchi, hata Wakili wakujitegemea anaruhusiwa kazi hiyo ila kwenye sheria ya uchaguzi bahati mbaya wamesema ni Hakimu.  Yeye akapeleka kwenye kampuni ya uwakili akapata muhuri lakini Tume ikamwondoa na ikitokea hivyo mnasikitika tu kwamba amekosa nafasi ya kugombea, lakini ndivyo sheria ilivyo.

Sasa na hili la leo, nimeona nilifafanue zaidi kwa sababu kuna hisia kama hizi, ninaandikiwa hapa, kwa hiyo, likae hivyo Waheshimiwa tuheshimu kanuni katika chaguzi zozote, Mkurugenzi wa Uchaguzi akishamaliza vyombo vinavyomsimamia haviwezi kusema tena vitengue. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, inaonekana kwa hisia zilizoko hapa umepita katika tundu la sindano, lakini ndiyo bahati yenyewe. Kwa hiyo, wewe ni mjumbe halali wa Tume ya Utumishi wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.53 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, Jeshi letu ni mfano wa kuigwa Barani Afrika, ni la wananchi hasa!  Nalipongeza kwa uaminifu wa kazi nzuri linalofanya katika kulinda mipaka yetu toka liundwe mwaka 1964.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kupendekeza kuundwa/kuanzishwa kwa Kambi ya JKT eneo la Mgandu (shule ya zamani ya Kirurumi Ukimbu) ili pamoja/sambamba na

kazi zake likabiliane pia na wimbi la majambazi/majangili kwenye mapori hayo ya kuanzia Itigi – Ukimbu – Mhesi – Rungwa – Chaya. Ni eneo lenye rutuba pia kwa kilimo na tajiri kwa misitu ya mbao na nyuki wa asali.

Nilishauri lipeleke Mkoani kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na *RCC*. Yote haya nilifanya, lakini sijapata jibu mpaka sasa kama ombi/pendekezo hili limekubaliwa au liko hatua gani mpaka sasa?

Naomba kupatiwa maelezo kuhusu hoja hii ya kuanzishwa kwa Kambi ya JKT pale Mgandu, Magharibi Kusini mwa Itigi.

Nawasilisha.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vita kuu ya Maji Maji ilianzia Kipatimu na kwa kuwa mnara wa mahali ambapo vita vilianza umejengwa: Je, Serikali haioni busara kupeleka japo kifaru kwenye mnara huo ili kupendezesha mnara huo na kifaru hicho kiwe chakavu?

Naunga mkono hoja.

**MHE. ELISA DAVID MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na JKT kwa hotuba yake ya bajeti ya 2009/2010. Aidha, naipongeza Serikali kwa maandalizi ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mchango wangu katika bajeti hii, naomba niwasilishe maombi ya wananchi wa Arumeru Magharibi kuhusu mipaka mipya ya JWTZ, Kambi ya *Tanganyika Packers* na wananchi wa Kata tatu za Mlangarini, Moshuna na Nduruma katika Jimbo langu la uchaguzi la Arumeru Magharibi.

Mheshimiwa Spika, JWTZ lina Kambi tano za Oljoro, Kambi mbili, Oldonyosambu, Negung'u na *Tanganyika Packers*. Mahusiano kati ya JWTZ na wananchi wanaoishi karibu na kambi na vikosi hivi yamekuwa mazuri na kumekuwa na amani na kuaminiana na watulivu kwa muda wote. Lakini hivi karibuni JWTZ, Kambi ya *Tanganyika Packers* wameweka mipaka mipya katika maeneo wanayoishi wananchi katika Kata za Mlangarini, Moshono na Nduruma, hali ambayo imeleta wasiwasi, hofu na hekaheka katika jamii. Kwa kuwa wananchi hawa bado wanasubiri maamuzi ya Serikali yao kuhusu hatima yao katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, JWTZ ni letu na wananchi hawa ni wetu. Tunaomba Serikali ione haki ya wananchi hawa ambao wamekuwa katika maeneo hayo husika hata kabla ya JWTZ halikupewa sehemu hiyo iliyokuwa ya *Tanganyika Parkers* katika miaka ya 1970.

Jambo hili limekuwa la muda mrefu na maombi haya ya wananchi yamezungumzwa katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Wizara na hata Ofisi ya Waziri Mkuu.

Tunaomba Serikali itoe uamuzi na itamke hatma yao wananchi hawa waende wapi na kwa fidia gani na haki gani? Ili kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, bila matatizo, naunga mkono hotuba ya Waziri kwa asilimia 100. Nampongeza kwa dhati Waziri, Naibu wake pamoja na Mkuu wa Majeshi na wapiganaji wote kwa Ulinzi wa nchi yetu hasa kwenye mipaka yetu.

Kama Waziri alivyoahidi kuunda Jeshi ndogo lenye taaluma na zana za kisasa, naomba nifahamishwe kuhusu ndege za kivita zilizoko *Mwanza Air Port* ambazo nimekuwa nikizisemea kila mara, ni lini zitaondolewa eneo hilo au hapo ndio zimefika? Je, kwa sababu ndege hizo zinatakiwa zirushwe kwa ajili ya mazoezi lakini ndege hizo aina ya *MIG* – 21 tangu mwaka 1993 hazijarushwa.

Je, ndege hizo haziwezi kuharibika kwa ajili ya kutokurushwa au kutofanyiwa mazoezi? Kati ya ndege hizo nzima ni ngapi?

Ili tuweze kujilinda vizuri, ni vizuri na tuweze kuona maadui zetu endapo itajitokeza ni vizuri Jeshi letu likaona umuhimu wa kuimarisha vyombo vyetu kama Rada, ndege za kivita, kikosi cha kutungulia Makombora na kadhalika.

Ukiacha vifaa vya kutengeneza, vifaa muhimu zaidi ni wanajeshi wenyewe (wapiganaji) Serikali inajali kwa kuwapa stahili zao, bila kuchelewa, askari wetu waandaliwe vizuri, tusubiri vita, kama vile kwenda Darfur. Ng’ombe wa mnada hanenepeshwi siku moja. Wapo askari (JW) hadi leo hawajalipwa posho, nauli na kadhalika. Wana malimbikizo ya madai, Jeshi letu ni Jeshi lenye nidhamu, lenye kupenda kufuata maadili, naiomba Serikali isiwe na kigugumizi cha kuwalipa stahili kwa wapiganaji wetu na hasa wale wa ngazi za chini.

Wataendelea kuwa na nidhamu na watafuata maadili endapo Serikali itatekeleza mahitaji ya stahili zao

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ziombe mamlaka husika zisirudie tena tabia ya *TANESCO* kwenda kukata umeme hasa maeneo maalum, pia ukataji wa maji maeneo ya kambi za wapiganaji wetu. Majadiliano yafanyike kabla ya uamuzi wa kwenda kukata umeme au maji. Busara itumike zaidi maeneo ya jeshi, hospitali, Ikulu kwa kuwa ni maeneo muhimu sana, hayaruhusiwi kuguswa hovyo hovyo.

Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza mno kwa kazi nzuri ya kulinda mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kurekebisha kambi za jeshi na kujenga nyumba mpya za wapiganaji. Kazi hiyo ifanywe kwa kutumia vikosi vyetu ambavyo wataalam wapo na nguvu kazi ipo.

Uanzishaji wa JKT ambao unatarajiwa kufanyika na wenye lengo zuri sana ufanywe kwa makini huku ikizingatiwa madhara ya sasa ya ugonjwa wa UKIMWI kutokana na tabia baadhi ya maafande ya kuwataka wasichana kimapenzi.

Michezo katika kambi ni muhimu kwa wanajeshi lakini kwa Taifa pia. Katika miaka ya nyuma Jeshi lilitoa wachezaji wazuri sana hasa katika riadha na *netball*. Ni wakati muafaka kwa sasa Jeshi kuwa na timu za kuitangaza Tanzania hasa Riadha.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nampongeze Mheshimiwa Mwinyi - Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Nchimbi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mkuu wa Majeshi Tanzania, Mnajimu Mkuu na Kamanda na Wapiganaji wote kwa kazi nzuri na kutuletea heshima kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa makusudi mazima ya kurudisha Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu wanaomaliza masomo yao. Hali hii ninaiunga mkono na kuomba Serikali, kazi hiyo ianze mara moja.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeze Serikali kupitia Mkuu wa Majeshi na watendaji kwa utaratibu mzuri waliouweka kwa wastaafu wanaomaliza muda wa kufanya kazi kwani huwa hawachukui muda mrefu kulipwa mafao yao. Taratibu hizi ziendelee na kama kuna uwezekano muda uzidi kupungua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa kustaafu, kweli kazi ya Jeshi ni ngumu na inataka moyo na kujituma zaidi, lakini ninaona askari wadogo wanastaafu na bado wana uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kuongeza muda wa kustaafu hasa kwa wale wanoonekana bado wana uwezo wa kufanya kazi, kwa sababu kuwastaafisha katika umri mdogo ni kuongeza idadi ya wazururaji na wengine kujishughulisha na vitendo vibaya vya ujambazi na makuzi ya kuongezeka vitendo vinavyosababisha UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu ya Wizara yake na wale wote walioshirikiana nao kutunga bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi ni nguzo kuu ya Ulinzi katika Taifa letu, pia linakuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma mbalimbali kwa umma na tunapongeza mchango mkubwa unaotolewa na Jeshi letu kama vile kutoa msaada wa maafa, majanga na mengineyo kama Ulinzi wa mipakani.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wetu kwa kazi ngumu walionayo ni lazima tuwatunze na tuwape heshima kubwa katika nchi hii ili wapate kuzidisha ari katika kazi yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, maslahi yao yaboreshwe na makazi yao yaboreshwe ili waweze kufurahia maisha yao. Leo utamkuta mwanajeshi anauza karanga au anauza *juice* kwenye kigenge ili aweze kutimiza mahitaji yake. Hii yote ni unyonge wa kuwa na mshahara mdogo, posho ndogo. Kama askari huyo amepata uhamisho hapewi posho ya safari au posho ya kujikimu kule anakokwenda, anaambiwa nenda malipo baadaye. Hiyo sivyo apewe kabla ya uhamisho ili akaanzie maisha.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wanapostaafu wapate mafao yao kwa wakati wasiwe wanasumbuka wengine wanadai mpaka wanakufa hawapati. Hii inawakatisha tamaa na pia Sh. 50,000/= ni ndogo iongezwe ifikie angalau Sh. 100,000/=.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabomu yaliyolipuka Mbagala ni watu wengi wamepoteza maisha na wengi wameathirika na kupata ulemavu wa aina mbalimbali. Je, Serikali inawaangalia vipi waathirika hawa kwa kupewa matibabu au vifaa, kama miwani kwa wale waliopata ulemavu wa macho au wale waliharibiwa mali zao au yote kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, sio vizuri raia kuruhusiwa kujenga karibu na Kambi za Jeshi ili kuepuka madhara kama yaliyotokea Mbagala.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mchango wangu ni huo na nawaombea Waziri na Naibu Waziri maisha marefu na kila la kheri. Naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya hotuba hii nikiwa ninatanguliza pongezi kwa Waziri na wataalamu wake. Hata hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu, sasa napenda kuchangia katika vipengele vituatavyo:-

(1) Askari wanaofanya ulinzi mipakani wanakaa muda mrefu na kuwa na mazoea na eneo hilo kitendo ambacho kinasababisha utendaji kushuka. Natoa mfano hai wa askari wanaolinda mpaka katika Mkoa wa Kigoma.

(2) Mheshimiwa Spika, nyenzo za usafiri kumekuwa tatizo na hasa kwa askari wanaokaa nje ya kambi. Tatizo hili linasababisha kuchelewa kwenda kazini mbali na kwamba Jeshi limejitahidi kuwa na magari makubwa ya kuwapitia. Naishauri Serikali ipange kwa makusudi mazima kununua magari ya kutosha kwa ajili ya Jeshi letu.

(3) Naipongeze hatua za dharura zilizochukuliwa wakati wa mlipuko wa mabomu katika ghala la Mbagala. Askari wa uhandisi walifanya kazi usiku kucha kuhakikisha wanaokoa maisha ya wananchi. Aidha, kazi ni zile hatua za kuokoa maafa zaidi kwa kuokota mabomu yote yaliyosambaa katika eneo hilo.

(4) Kuhusu JKT – nashauri kuwe na utaratibu mzuri wa kupata vijana wa kwenda kujiunga kwenye *CTS.*

Wizara inafahamu kwamba miongoni mwa silaha za kijeshi zilizoko katika Kambi za Jeshi letu huko Tabora ni pamoja na mabomu. Kutokana na milipuko ya mabomu katika Kambi ya Mbagala Mjini Dar es Salaam, ninaishauri Wizara iimarishe utaratibu wa kuzikagua silaha za aina hii katika Kambi za Jeshi letu nchini kote pamoja na Tabora.

Kuna malalamiko mengi ya kucheleweshwa malipo ya pensheni pamoja na mafao mengine kwa askari waliostaafu. Napendekeza Serikali/Wizara iweke mkakati utakaoweza kulimaliza au kulipunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hili ili askari wetu wastaafu waweze kuishi maisha bora.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naomba niungane na Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi, kwa maandalizi mazuri ya hoja iliyowasilishwa Bungeni hivi leo. Naunga mkono hoja hii na kulipongeza Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kulielezea Bunge, jitihada gani zimetumika katika kujibu malalamiko ya wapiganaji kuhusu madai yao mbalimbali na hasa wastaafu wanaoandamana kila mara na kutumia vyombo vya habari ambavyo vyenye nia na kudhalilisha utendaji wa Jeshi letu?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kurejesha mafunzo ya JKT nchini, mimi kwa niaba ya wananchi wa Rukwa – ningeomba Serikali ifikirie kuanzisha Kambi ya JKT – Luwa au eneo la Milindukwa ambako JKT waliwahi kuwepo.

Mheshimiwa Spika, naliomba hili kwa sababu kazi mojawapo ni pamoja na kuzalisha chakula. Eneo ninalotaja lina uhakika wa hali nzuri ya hewa na eneo kubwa la ardhi linalofaa kwa kilimo. Kipindi hiki ambacho Serikali imepania kilimo kwanza : Jeshi letu nalo litumie nafasi hii kutekeleza azma hii. Lakini kwa sasa, maandalizi yaanze kwa kuoanisha maeneo, kuandaa watendaji, kuandaa makambi na zana za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ulinzi katika mipaka yetu hasa ya Ziwa Tanganyika eneo la Kasanga, Kirando, Karema – yanavamiwa kila mara na baadhi ya majirani wa kutoka nchi za *DRC*, Rwanda/Burundi na kuleta madhara ya mara kwa mara. Eneo la Ulinzi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ni mrefu sana na linatakiwa kuwa na doria za mara kwa mara kwa kushirikiana na boti za Polisi na za Maafisa wa Uvuvi, katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, mengi yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Waziri, yanahitaji fedha. Lakini pia katika kipindi hiki, wananchi wanasubiri kama kweli JKT itaanza rasmi – mwaka ujao. Wote wanasubiri kuona kama ni kweli au tunawahadaa. Hili jambo liwe la kufa na kupona. Tuanze angalau na vijana wachache, angalau lianze. Tusikubali kushindwa.

Mheshimiwa Spika, nitaendelea kulipongeza Jeshi letu kwa jinsi walivyoshughulikia tatizo la milipuko ya Mbagala na tutumie nafasi hii kujifunza zaidi nini tunatakiwa kujiandaa tukijua kuwa yapo maeneo mengine ya namna hii yanayoweza kusababisha mambo kama hayo yasitokee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kumtakia Waziri na timu yake waendelee kufanya kazi nzuri sana.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara. Nampongeza Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na viongozi wote wa JWTZ na JKT.

Mheshimiwa Spika, pili, naanza mchango wangu kwa kuzungumzia juu ya maslahi ya wanajeshi, angalau yaongezeke kwani kiwango wanachopata hakitoshi hali ya maisha imepanda sana hivyo waangaliwe upya juu ya mishahara na posho zao. Nawapongeza wanajeshi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, tatu, natoa pongezi kwa Serikali kwa kufufua mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa Kitanzania. Hii itasaidia kuwajenga katika uzalendo, ulinzi, usawa na umoja wa kitaifa, uzalishaji mali na ufundi stadi. Hii itasaidia sana kwani maadili ya vijana wetu hivi sasa hayaridhishi kabisa.

Mheshimiwa Spika, nne, namalizia kwa kutoa pole kwa milipuko ya mabomu yaliyotokea Mbagala – Dar es Salaam. Kwa kweli, lilikuwa ni janga la kitaifa.

Naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge kutoa rambirambi zangu kwa Naibu Mufti wetu ambaye alifariki dunia kwa ajali ya gari huko Lindi. Mungu aiweke mahali pema Peponi roho yake. Amen.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi pamoja na Naibu wake kwa utendaji wao mzuri akishirikiana na majemadari wote katika Wizara hii muhimu katika Ulinzi wa nchi yetu, hasa mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpa pole Mkuu wa majeshi na Jeshi kwa jumla kwa kadhia ambayo imetokea kule Mbagala hivi karibuni na kupelekea vifo kwa wanajeshi na raia kwa jumla. Sisi bado tunaliamini Jeshi letu na kufahamu kwamba yaliyotokea na ajali kama zile zinazotokea katika nchi nyingine kijeshi. Hapa zaidi ni kusisitiza raia kutokujenga karibu kabisa na makambi ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Jeshi upande wa kikosi cha wanamaji kwa kutoa mashirikiano mazuri kule Zanzibar katika ajali ya meli hii, imetoa picha nzuri kwa wananchi wote kwamba Jeshi linajali maisha ya Watanzania, hivyo pongezi zaidi zimwendee Brig. S.S. Omar ambaye aliongoza wanamaji hao katika tukio.

Mheshimiwa Spika, sasa labda niingie katika maoni yangu kuhusu utaratibu mzima wa kuwaenzi makamanda wetu wa kijeshi hasa wale wanaoanzia vyeo vya ukanali na kuendelea kwa sababu hivi sasa makamanda hawa hasa wataalam kutakiwa na nchi jirani kwa utumishi huo huo wa kijeshi. Katika hili, si suala la kubeza hata kidogo, kwa sababu hii ni hatari sana kwa kudhibiti siri za ndani ya jeshi letu, lakini pia hatma yake hatuifahamu hasa. Hivyo mimi napendekeza kabisa viongozi hawa wanapostaafu watengewe sehemu maalum za kumalizia maisha yao bila kuyumba.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia kwa kukiangalia kikosi cha wana maji cha Kigamboni hasa kitengo cha karakana kwa kukipa fedha nyingi kukiboresha, hii itasaidia sana katika kuzalisha vipuri pamoja na kuzifanyia matengenezo meli ndogo ndogo kupitia chelezo chake hivyo kitaweza pia kukiingizia mapato ki-ufindi na kuwawezesha vijana wa sehehmu hizo watakapostaafu wataondoka na utaalamu mahsusi.

Mheshimiwa Spika, michezo katika Jeshi ni kitu muhimu sana, sio tu kwa afya zao, lakini bado hivi sasa michezo imeshuka sana. Nalishauri Jeshi liongeze juhudi zake na kurudisha hadhi ya Jeshi kimichezo kama enzi zile za akina Philbert bay na wenzake. Katika hili, sababu haipo, kwani uwezo wanao hasa ukizingatia wana afya nzuri na wanapata matunzo yanayoridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vituo vyetu vya Ulinzi kupitia umulikaji wa vyombo vinavyoingia na kutoka vinapaswa vitiliwe mkazo kwa kuviimarisha zaidi kwa kuhakikisha lengo la kuwepo kwao hakupotezi maana yake, hasa kile cha *Wazo Hill* ukizingatia kimezungukwa na mazingira magumu ya vumbi na milipuko ya kiwanda cha saruji. Vijana wale wanapaswa kuangaliwa afya zao na pia kupata chakula maalum na mzunguko wa kuishi pale uwe wa muda mfupi.

Mwisho, nawapongeza wanajeshi kwa kutozurura mijini wakiwa na sare. Hili linaiongezea Jeshi hadhi. Ahsante.

**MHE. JOHN M.CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Katibu Mkuu na wapiganaji na walinzi wa Taifa letu wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa Taifa letu. Naomba kutoa maoni yangu kwa maeneo yafuatayo:-

Nilipata nafasi kutembelea Jeshi letu Kigamboni na tulielezwa mengi pamoja na mafanikio ya kutengeneza *"special boats"* za Ulinzi na matatizo lukuki ya uchakavu wa meli zetu za kivita. Katika hali halisi ya *"Piravy"* uharamia katika Bahari Kuu, wizi wa rasilimali zetu kama samaki, ni lazima uimarishaji wa Jeshi letu la *"Navy"* ukubalike kama kipaumbele na tuimarishe *Navy*. Fedha iliyotolewa kwa ukarabati wa *Navy operations in million 727* tu hizi hazitoshi kukarabati meli zilizochakaa. Jeshi hili ni muhimu mno kwa hali halisi ya sasa. Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kutenga fedha zaidi kwa bajeti hii au zifuatavyo :-

Tatizo kubwa nililoona ni mafuta ya kuendeshea meli za kivita. Mwaka Jana 2008/2009 zilitengewa milioni 200 tu. Nimeona mwaka huu fedha zimeongezwa kufikia Shilingi bilioni 1.4. Naipongeza Serikali kwa kusikia kilio cha *Navy*. Nasisitiza mahitaji ya mafuta yaendelee kutengwa kama dhana ya Ulinzi wa mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, dhana kwamba Jeshi halifanyi biashara inapaswa kuangaliwa tena. Kitengo cha Nyumbu kina nafasi kubwa kutengeneza bidhaa mbalimbali ambazo zinaweza kuuzika. Bidhaa hizi ni pamoja na vifaa vya kilimo na *'power tiller'*. Serikali ikubali kutoa fedha za kutengeneza vifaa vya kilimo badala ya kuagiza kutoka nje. Fedha za kuimarisha uchumi katika hali ya mtikisiko wa uchumi zipelekwe Nyumbu kutengeneza vifaa vya kilimo kama *plau, tractor* ndogo.

Mheshimiwa Spika, vitengo vya kuzalisha mali kama vile Kitengo cha Ujenzi kipewe kazi za Kujenga majengo ya Serikali – kazi zote za *TRA* zipelekwe kwa kitengo hiki kwani wana ufanisi na uwezo wa Kujenga na pia ni nafasi nzuri ya vijana wetu kupata ujira na rushwa kwa ujenzi huu hakuna.

Mheshimiwa Spika, kitengo cha fenicha kizuri sana. Fenicha zote za Serikali zitengenezwe na JKT, uwezo upo na ni nafasi nzuri ya kufundishia vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Kenya wanatupiga na kuiba mifugo. Jeshi liingilie kati na lionekane lipo. Naunga mkono taarifa ya Mbunge wa Rorya na Ulinzi uimarishwe. Tusiogope kuimarisha Jeshi ndiyo nchi inavyojengwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi kumshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa kutayarisha bajeti ya Wizara na kuiwaisilisha hapa Bungeni. Pamoja na shukrani hizo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni lilitokea jambo ambalo kwa Watanzania wengi lilikuwa geni sana. Hili ni mlipuko wa mabomu huko Mbagala. Mlipuko huo ulisababisha madhara makubwa, ikiwa ni pamoja na vifo, ulemavu, kubomoka kwa nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua yafuatayo:-

(i) Hivi ni nini hasa chanzo cha mlipuko wa mabomu hayo?

(ii) Je, ni kwa kiasi gani uzembe ulihusika katika mlipuko wa mabomu hayo na kama ulikuwepo ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa maafisa waliohusika?

(iii) Je, ni watu wangapi (askari na raia) wamepoteza maisha katika ajali hiyo? Pamoja na Serikali kuhusika katika mazishi ya Marehemu hao: Je, ni msaada gani mwingine na wa kiasi gani Serikali imewapa jamaa za Marehemu?

(iv) Je, ni watu wangapi wamepata ulemavu wa kudumu na Serikali inachukua hatua gani kuwatunza na kuwahudumia maisha yao yote, hasa ikizingatiwa kwamba, wengi wao watashindwa kujiingizia kipato kwa ulemavu ambao umesababishwa na Serikali?

(v) Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam - Mheshimiwa Lukuvi, aliunda Tume ambayo moja ya hadidu rejea ilikuwa ni kufanya tathmini ya nyumba zilizoathirika na mabomu hayo: Je, matokeo ya tathmini hiyo ni nini? Ni kiasi gani cha fedha kitatumika katika kuwafidia waathirika wa mabomu hayo?

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii imejifunza nini kutokana na mlipuko huo na inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hali au ajali ya namna hiyo haitokei tena?

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa ambazo Jeshi letu limepata kwa utendaji wake mzuri wa kazi, bado kuna tuhuma zinazowahusisha na vitendo vya ujambazi. Nataka kujua: Je, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 ni askari wangapi walikamatwa wakijihusisha na vitendo hivyo na ni hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika hao?

Mheshimiwa Spika, kuna Watanzania wengi (askari na raia) walioshiriki katika vita ya Kagera mwaka 1978/1979. Vita hiyo ilikuwa na lengo la kumng'oa Nduli Amini aliyeivamia nchi yetu bila sababu za msingi. Katika hiyo kuna Watanzania wengi walioumia na wengine kupata ulemavu. Bahati mbaya sana askari na raia waliopata ulemavu wa kudumu waliachwa bila msaada wowote ule. Mwaka jana nikichangia bajeti ya Wizara hii kwa maandishi, nilishauri kwamba Serikali iwaangalie Watanzania hao na kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, aidha, niliishauri Serikali iwaorodheshe waathirika wote wa vita hiyo na kuwasaidia. Mimi nilitaja jina la ndugu Saidoni Mzumbwe wa Isansa –

Mbozi kama mmoja wa waathirika waliopata ulemavu kutokana na ushiriki wake katika vita hiyo. Hata hivyo, hajapata msaada wowote na anaendelea kupata taabu kubwa. Ndugu Mzumbwe amekuwa akipata matibabu ambayo ugonjwa wake umesababishwa na athari za vita hiyo na kwa gharama kubwa sana. Naomba kujua Wizara, imechukua hatua gani katika jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, mashirika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu ni muhimu sana kwa Jeshi letu hasa katika maeneo ambayo yanahusu mashirika yenyewe. Pamoja na jitihada za Wizara katika kuyaboresha, bado jitihada zaidi zinahitajika. Naishauri Serikali itenge pesa zaidi ili kuwezesha shughuli za utafiti na uzalishaji kwa Shirika la Mzinga ziweze kufanyika kwa ufanisi zaidi. Aidha, kwa Shirika la Nyumbu kutengewa pesa zaidi kutaliwezesha kufanya vizuri zaidi katika maeneo ya utafiti wa magari na mitambo, utengenezaji wa mashine za kufyatulia matofali na trekta ndogo. Hatua hii sio tu italisaidia Jeshi peke yake, lakini pia Watanzania wengi wapenda maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Mafunzo hayo yatarejesha na Kujenga uzalendo miongozi mwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Makamanda wote na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri inayoeleweka na kuonyesha wazi mpangilio wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na azma thabiti ya kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu hasa wasomi kwa vile kwa sasa vijana hawa wameanza kupoteza moja ya msingi imara wa amani na utulivu ambao ni uzalendo kwa nchi yao. Kukosekana kwa uzalendo kunaweza kuleta maafa nchini na kuzua uvunjifu wa amani tulionayo.

Mheshimiwa Spika, zaidi, natoa pongezi kwa Wizara kufanya marekebisho ya maslahi – pensheni kwa wanajeshi wastaafu wote ili waweze kumudu maisha ya ustaafu lakini pia kuwatendea haki kwa kazi yao nzuri, ya hatari na ya kizalendo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kufahamu ni huduma gani hutolewa kwa wanajeshi wanaopata ulemavu wa kudumu kutokana na kutekeleza wajibu wao? Nahitaji ufafanuzi huo kwa vile kumekuwapo na malalamiko ya hapa na pale toka kwa baadhi ya waathirika kwamba wametelekezwa. Malalamiko kama haya yanaweza kuwakatisha tamaa wanajeshi wengi.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu jitihada za Serikali za kuwapatia wanajeshi usafiri wa uhakika kutoka maeneo yao ya makazi kwenda na kurudi kwenye maeneo yao ya kazi/ofisi. Haipendezi kuwaona wanajeshi hasa wa vyeo vya chini wakisubiri usafiri wa msaada wa daladala na kadhalika kwa upande wangu naona

wanastahili (wanajeshi) kupewa heshima yao sio kusafiri kwa kusukumana nao kwenye mabasi ya raia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mfupi, naunga mkono hoja na kuwatakia heri katika utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa kwenye bajeti ya Wizara.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na kuipongeza Wizara hii kwa yafuatayo:-

(1) Kurejesha tena Jeshi hili la Kujenga Taifa nchini ;
(2) Kutunza na kuendeleza amani, utulivu na usalama nchini ;

(3) Kutatua na kuweka mazingira mazuri ya makazi na maslahi ya watumishi ndani ya jeshi ; na

(4) Kukubali Serikali kulipa pensheni kwa wastaafu na malimbikizo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipongeza Wizara, napenda nitoe changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana hao, kwa kuwa Taifa litawachukua vijana wengi kambini kwa ajili ya kuwapa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya taaluma mbalimbali, naiomba Serikali kuwapa kipaumbele vijana hao mara ajira zinapojitokeza kulingana na fani atakayokuwa amefuzu. Tukumbuke kuwa Jeshi hilo litakuwa na wasomi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuwekewa nafasi maalum VETA. Naomba Serikali iweke utaratibu wa kila mwaka kwa kila Chuo cha Ufundi hasa cha VETA ili mara wanapofuzu vijana waweze kupokelewa katika vyuo hivyo na baadaye waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza ujenzi wa nyumba, pamoja na juhudi nzuri za makusudi za kuboresha makazi kwa ajili ya wanajeshi wetu, bado kuna haja ya Wizara kuendelea kuwa na uendelevu wa mikataba ya ujenzi na *NSSF* au mashirika/mifuko ya hifadhi kama ilivyofanya hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa vijana katika Kambi za JKT wawe wasomi. Tukumbuke kuwa vijana wanaojiunga na Jeshi hili wengine ni wasomi. Hivyo, ili kuendana kisomi, walimu sharti wawe wasomi kulingana na mazingira ya sasa ya Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa juhudi ya kujaribu kuilinda mipaka ya nchi yetu kwa kutumia bajeti finyu sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuikumbusha Serikali kuwa mipaka ya nchi yetu iliundwa kwa dhati na sisi wenyewe. Mikapa ya nchi yetu tunakopakana na Zambia ni wazi tu na kama ikitokea mtu akataka kuidhuru Tanzania kupitia maeneo yale atafaulu. Mipaka yetu pande zile askari ni wachache na vitendea kazi hawana.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali izikague *custom* zake hususan Kasesya Jimbo la Kalambo wajionee mpaka huo usio na gari la doria wala mashine za kupekulia. Wananchi hawana uelewa wa ulinzi shirikishi. Kwa sababu hiyo, mifugo huibiwa na kuvushwa huko, pengine hata ng'ombe 40 hutoroshwa kwa kupitia kule kwa wakati mmoja. Ipo *custom* ya Mozi kwa kupitia Mwimbi nayo pia iko hoi. Mtula nako kuna soko la kimataifa lakini *custom* iko Mozi ambako ni zaidi ya kilometa 12. Je, askari wa Mozi wakiitwa kwenye tukio Mtula watawahi? Naomba Ulinzi uimarishwe mpaka wa Zambia na Tanzania upande wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kurejesha JKT. Itajenga nidhamu ya vijana na kuimarisha uwajibikaji. Hata hivyo, natoa rai kwa Serikali kutoa elimu kwa watoto/vijana wanaokwenda JKT kuwa JKT sio kozi ya kupatia ajira ili wasitoke na dhana hiyo halafu badala ya kushiriki ulinzi hawakupewa kazi.

Mheshimiwa Spika, posho ya wanajeshi iangaliwe upya na maslahi mengine kama vituo vya afya mipakani viwekwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORCE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(1) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyakarabati majengo ya kKmbi ya JKT Makutopora na Kambi ya Ihumwa na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha ikiwa ni pamoja na magari (mabasi) ya kubeba askari kwa kuwa wanapata shida kubwa ya usafiri. Je, katika bajeti ya mwaka 2009/2010 ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa kazi hiyo?

(2) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya maaskari wa JWTZ kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu?

(3) Je, Serikali ina mpango gani wa Kujenga nyumba (makambi) ya kutosha ili wanajeshi wote wakae kambini badala ya uraiani?

Mheshimiwa Spika, narudia tena kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Wanajeshi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, nampongeza Mheshimwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake ambayo inalenga utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2005.

Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi kwa mashirikiano na utendaji kazi katika Wizara hii, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wa Wizara kutokana na kazi zao nzuri ambazo wanazifanya katika kuimarisha Ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuandaa ni kuimarisha Jeshi la Ulinzi wa Mgambo kwa kuwapatia mafunzo ya ulinzi kuanzia mwezi Juni, 2008 hadi Novemba, 2008 katika Mikoa mbalimbali nchini. Bado Jeshi letu la Mgambo linafanya kazi kwa kujitolea na wako katika hali ngumu sana kimaisha.

Hata hivyo pamoja na kazi ngumu zote wanazozifanya zinapotokea ajira za Jeshi hawapewi kipaumbele katika kupatiwa ajira hizo na Serikali huamua kuchukua askari katika Jeshi la Kujenga Taifa *JKT* na *JKU* bila kuangalia kuwa wapo askari wetu ambao wameshapata mafunzo ya kijeshi.

Pia kutokana na hilo, hujitokeza tabia ya watendaji waliopewa jukumu la kuorodhesha vijana kwenda Jeshi, kukiuka sheria na kuchukua vijana walio nje ya Jeshi na kutoa kauli kuwa wametoka JKU au JKT na hii waliamua kutokana na kilio ndani ya ukumbi bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, hivi tunakwenda wapi? Askari wetu wa mgambo tunawafahamu kazi zao, juhudi zao, uzalendo wao, kujitolea kwao pia na mafunzo yao. Tunakwenda wapi?

Naiomba Serikali kupitia Wizara hii ipitie tena upya mchakato uliotumika wa kuwapata vijana wa Jeshi ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kwani hivi sasa hali ni mbaya sana na tukiangalia tunakwenda katika uchaguzi wa mwaka 2010.

Hata hivyo, vijana waliotakiwa kuorodheshwa kimkoa, kiwizara walitakiwa vijana 100 kwa kila Mkoa.

Katika Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba wamechukuliwa vijana 115 tu badala ya 200. Je, hawa 85 wamepatikana wapi kujaza hapo. Naomba mchakato urudie hali ni mbaya sana Kaskazini Pemba. Ahsante nashukuru.

Hii imesababisha kuleta malalamiko mengi sana kwa askari wetu wa Jeshi la mgambo na kujiona hawana haki katika nchi hii na hili limejitokeza katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha sheria maalum itakayowatambua askari mgambo na kuletwa Bungeni haraka iwezekanavyo.

Angalau kuhusu ajira za Jeshi zinapotokea kupitia moja kwa moja mgambo bila kupita sehemu nyingine. Askari wetu hawa tumewaamini, wamepata mafunzo kamili na hawana dosari katika ajira hizo. Bila kufanya hivyo tutaendelea kulidhalilisha Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, nathubutu kusema kwamba, hivi karibuni katika Kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba cha kujadili ajira za jeshi, askari wa mgambo wamedhalilishwa na kutolewa hatimaye kuambiwa Jeshi letu hatulitambui vijana wa mgambo hao.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi, bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni imetokea ajali mbaya ya milipuko ya mabomu katika Kambi ya Jeshi la Wananchi Mbagala. Ajali hiyo ilisababisha maafa makubwa ya vifo, majeruhi, uharibifu wa mali, nyumba na hasara kubwa ya silaha katika Jeshi la Wananchi. Serikali na taasisi mbalimbali na Jeshi la Wananchi zilifanya kazi kubwa kuwahudumia wananchi na Jeshi kuhakikisha milipuko haiathiri zaidi katika ulipuaji wa mabomu katika tukio hilo, ni vyema sasa Jeshi liangalie uwezekano wa kambi zisiishi karibu ya wananchi. Serikali ihamishe wananchi na kuwapatia maeneo mengine kwa kufuata sheria za kijeshi zinasemaje ufuatwe ili jeshi lisiwe karibu na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa naipongeza Serikali kwa kurudisha Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafunzo ya vijana wetu wanapomaliza mafunzo ya shule kupitia Jeshi, kutawafanya kuwa wakakamavu na kuwa na maadili.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hivi sasa inakumbwa na maafa katika bahari ya Hindi, meli kuzama na boti kuzama. Meli kubwa kuiba samaki katika bahari yetu ya Hindi Serikali iongeze vitendea kazi na kuongezewa boti za kisasa ili kukabiliana na matukio hayo.

Fidia kwa wanajeshi ni ndogo sana, ni vyema zikaangaliwa upya na ziongezwe. Wastaafu wa Jeshi la Wananchi zisichelewe kwa sabablu wana maisha magumu wakistaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Jeshi, napongeza kwa kazi inayofanyika. Kazi ya ujenzi huo na ifanyike kwa kasi zaidi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanajeshi wamekuwa na utovu wa nidhamu kwa kujihusisha na uhalifu na kuwafanya wananchi kutokuwa na imani na kujiuliza kulikoni pale wanapokamatwa wachukuliwe hatua kali, wanatia dosari Jeshi letu.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema na kutujalia Waheshimiwa Wabunge kuchangia hotuba hii adhimu ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mkuu wa Majeshi na wapiganaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya za Ulinzi wa nchi yetu pamoja na misaada wanayoitoa kwa jamii nchini na nje ya nchi kwa nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sina wasiwasi na utendaji kazi na Wizara hii, nina mchango mdogo ili kuweka sawa baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu lina heshima ya hali ya juu na wapiganaji wanajituma na kuwa na uvumilivu wa hali ya juu. Lakini kuna tatizo dogo ambalo askari wadogo huwa hawapatiwi malipo haya. Suala hili kama lina ukweli, ninaiomba Serikali irekebishe hali hiyo kwa sababu malipo haya yanamgusa kila mmoja wetu na wala hayachagui mkubwa na mdogo iwe unakaa katika nyumba yako au ya kupanga.

Mheshimiwa Spika, kikawaida kambi zetu za jeshi huwa zina maeneo makubwa sana na zinatakiwa ziwe mbali na makazi ya watu. Lakini wananchi wetu huwa wakaidi na kuendelea kuyatumia maeneo hayo kwa kujenga nyumba na wengine huyatumia kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni hatari, kama ilivyotokea Mbagala, roho za watu zimepotea, nyumba zimekwenda na kuigharimu Serikali fedha nyingi kulipa fidia. Ninaiomba Serikali kuwa makini kwa hili kwa kuwaondoa wale wote waliovamia maeneo hayo, kwani wahenga wanasema huruma hailei mtoto na usipoziba ufa utajenga ukuta.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Kambi ya Kisakasaka wananchi wengi wanalima pembezoni mwa kambi hiyo iliyoko Zanzibar Jimbo la Dimani na eneo kubwa lililoko Jimbo la Fuoni. Hivi sasa wamehamasika zaidi na kilimo na wanaendelea na kilimo cha kustawisha miti ya kudumu. Kwa hiyo, sasa umefika wakati wa Jeshi kuweka mipaka ya kambi ili kuondoa migogoro baadaye ambapo hivi sasa kitu hicho hakipo.

Mheshimiwa Spika, suala hilo naomba litekelezwe kwa haraka. Kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI**: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Wapiganaji, Watendaji na wote chini ya Uongozi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mkuu wa Majeshi (CDF) na Makamanda wote, wa kazi nzuri wanayoifanya katika kulinda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mlipuko wa mabomu uliyotokea katika Kambi ya Jeshi Mbagala, Makambi yote yahakikishe wananchi hawajengi nyumba karibu na Makambi hayo.

Kutokana na unyeti wa masuala ya usalama wa nchi kwa ujumla ni vyema Jeshi likawa na utayari wakati wote na hasa kuwa na vifaa vya kisasa (zana za aina zote).

Vikosi vya Majini (Navy) na Kikosi cha Mafunzo Morogoro, vipatiwe fungu maalum, kwa mazoezi ya mara kwa mara ili kuwajengea uzoefu wapiganaji chipukizi ili kuziba pengo la wastaafu.

Bidii zaidi ziongezwe kwa kujenga nyumba za askari na usafiri.

Hospitali ya Lugalo iboreshwe zaidi kwa hadhi ya kuwahudumia Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA**: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Majeshi, pamoja na Wasaidizi wao wa ngazi mbalimbali, kwa matayarisho mazuri ya bajeti hii.

Aidha, nina maoni yafuatayo katika maeneo haya:-

Katika nyakati tofauti, nimekuwa ninaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuipanua Hospitali ya Jeshi iliyoko katika Kambi ya Tabora. Serikali imekwisha ahidi kwamba, inaandaa mradi mkubwa wa ujenzi wa Hospitali ya Jeshi Tabora. Nasisitiza umuhimu wa serikali kuupa kipaumbele mradi huu ili utekelezaji wake uanze mapema iwezekanavyo.

Jeshi letu la Ulinzi katika makambi yake yaliyoko Brigedi ya Magharibi hususan katika eneo la Tabora, linadaiwa takriban Sh. 228.8 millioni na Shirika la TUWASA (Tabora Urban Water and Sewerage Authority). Deni hili linajumlisha baki ya deni la Sh. 125,5 mpaka Juni, 2008 na Sh. 103.2 mpaka Juni, 2009.

Kwa nyakati tofauti, Maafisa wa TUWASA, wamekuwa wakifuatilia ulipwaji wa madeni haya Makao Mkuu ya Jeshi, bila mafanikio makubwa. Kwa hiyo, napenda kutumia fursa hii kuiomba Wizara hii, itenge fungu litakalopunguza deni hili kwa kiasi kikubwa au kulilipa lote. Kuendelea kuchelewa kulilipa deni hili, kuna athiri sana uwezo wa TUWASA kutekeleza majukumu yake ya kuzalisha na kusambaza maji safi na salama Mjini Tabora.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Wapiganaji wa JWTZ na JKT, kwa maandalizi mazuri na kazi nzuri wanazozifanya ili kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kuwa salama. Aidha, nawapa pole sana kwa tukio la Mbagala, ambalo lilisababisha hasara kwa wananchi na watu 30 walifariki.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi, suala la milipuko kwenye makambi yetu ya kijeshi hatujawahi kulisikia. Milipuko ya Mbagala imelistua sana Taifa na hata baadhi ya watu kujiuliza ni jinsi gani Jeshi au Majeshi yetu yanafuatilia uhifadhi wa silaha

kwenye maghala yake. Inavyoonekana, hakuna mikakati ya kutosha ya kuhakikisha kuwa, kuna uangalizi wa mara kwa mara wa maghala hayo ya silaha, hasa silaha nzito ambazo huwa hazitumiki mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Majeshi yetu yakawa na ratiba mahususi ya uangalizi wa silaha hizo wa mara kwa mara, hususan zile zisizotumika mara kwa mara. Aidha ni vyema silaha nzito zikatunzwa mbali na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, makambi mengi ya jeshi, yamezungukwa na makazi ya watu, pamoja na kwamba, yalitangulia kujengwa na baadaye wananchi kuhamia maeneo jirani na makambi hayo. Hata hivyo, makambi mengi yamekuwa yakishindwa kuwazuia wananchi kujenga makazi yao jirani kabisa na makambi hayo kutokana na kuwa hakuna mipaka ya sheria ya makambi hayo.

Ninashauri kuwa ni vyema makambi hayo kuwa na mipaka iliyopimwa kwa mujibu wa sheria ili kuwadhibiti watu wanaovamia maeneo ya jirani na makambi yetu hasa za JWTZ na JKT.

Mheshimiwa Spika, makambi yote yanayohifadhi silaha nzito, yahamishiwe kwenye maeneo ya mbali na makazi ya watu na pia umbali wa kambi na makazi ya watu usipungue mita 300 au kadiri Jeshi litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa makambi yanayozungukwa na wananchi, yajengewe uzio na yasihifadhi silaha nzito nzito.

Mheshimiwa Spika, askari wetu wamekuwa wakilalamikia suala la resheni kucheleweshwa na kuwa chakula wanachopewa hakilingani na fedha wanayokatwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa, wanajeshi hao wapewe uhuru wa kuchagua ama kuendelea na utaratibu uliopo au kupewa fedha hizo kwa wanaopenda hivyo. Hii itaondoa malalamiko kwa askari wetu kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka juzi, serikali kupitia Waziri wa Ulinzi na JKT, iliahidi kuchimba kisima kwenye Kambi ya JWTZ Mwanyanya iliyoko Jimbo la Bububu Zanzibar, hadi leo kisima hicho hakijachimbwa na wanajeshi wanaendelea na utaratibu wa zamani, ambao haufai, kama nilivyochangia mwaka juzi kwenye bajeti hiyo. Naiomba sana serikali itimize ahadi yake, kisima hicho hakitagharimu fedha nyingi, kwa sababu *water table* katika eneo la kambi iko karibu sana (chini ya mita tano *deep*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ninalitakia utendaji mwema Jeshi letu zuri la Ulinzi na JKT.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA**: Mheshimiwa Spika, sina budi kuwashukuru Waziri wa Ulinzi, Naibu wake, Mkuu wa Majeshi na watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa kuwasilisha bajeti hiyo ya Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, napenda Waziri anipe maelezo ya kina, juu ya nafasi ya ajira ya Jeshi kwa upande wa Zanzibar. Nafasi zilizotengwa kwa ajili ya Zanzibar ni vyema zote zitumike kwa Zanzibar. Zipo tetesi nafasi hizo zinataka kufanyiwa ujanja ili zijazwe na Bara. Huu ni Muungano na Jeshi letu ni la Muungano, nafasi hizo zitumiwe kwa Zanzibar. Wakati wa majumuisho, napenda Bunge lielezwe hatua zilizochukuliwa juu ya ajira hiyo.

Mheshimwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina, juu ya wanajeshi waliopelekwa vitani. Kwenye Bunge hili, Waziri Mkuu alitoa kauli juu ya malipo kwa wale askari walioshiriki vita vya Uganda; leo tunashangaa wazee wetu waliopigana vita vikuu vya dunia, Waingereza wamethubutu kuwalipa Watanzania walioshiriki. La kushangaza, serikali yetu inashindwa kuwalipa wanajeshi wetu waliopigana Vita vya Nduli Idi Amin. Naamini hii ni heshima kubwa, lakini haitumiki dukani, ukiangalia hali ya maisha ya binadamu. Naomba Mheshimiwa Waziri, atoe maelezo ya kina juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba Waziri wa Ulinzi, anipe maelezo yakinifu juu ya Askari wanaopelekwa kozi mbalimbali za Jeshi na hasa upande wa Zanzibar na kuelezwa wajilipie baadaye watarejeshewa fedha zao na huwa hawarejeshewi. Mimi ninao ushahidi kamili juu ya suala hili, ukizingatia Jimbo ninaloliongoza ndipo ilipo Makao Makuu Nyuki BRD.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo kwa Mheshimiwa Waziri, juu ya maduka yaliyomo kwenye makambi ya jeshi, ambayo wafanyabiashara wanatoa huduma hizo na wanasamehewa ushuru wa TRA. Vifaa vyao havina tofauti ya bei na wafanyabiashara wanaolipa ushuru.

Niliongea kwenye bajeti iliyopita, lakini hakuna mabadiliko. Ni dhamira nzuri ya serikali kuwaondoshea uzito wa maisha wanajeshi wetu. Hadi leo, marekebisho bado hayajaamuliwa. Namwomba Waziri anipe maelezo juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Mheshimiwa Waziri, kurudia suala la Zanzibar kumuweka Brigadia yule Mzazibari, kwa sababu kuna mambo mengi yanayojitokeza kuweza kutatuliwa na anayajua mazingira ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko ya askari kuhusu *ration allowance*, nalo lichunguzwe ukweli ulivyo. Askari wamefanyiwa ujanja kwa sababu hawana pa kukimbilia juu ya haki zao.

Matatizo ya maji Kambi ya Baruai na Nyuki, hadi leo hawajapatiwa mashine, yaani pump ya maji. Nyumba za Jeshi Makao Makuu Nyuki Brigade zinavuja, zinahitaji kuezekwa upya. Naomba Mheshimiwa Waziri, afafanue juu ya michango yangu.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Navy; upungufu wa kuwapatia fedha kidogo za uongozaji wa kikosi hicho hasa ukiangalia vyombo vya bahari, vinakaa muda mrefu bila

ya kutembea; meli ikikaa tu bila ya kutembea inazidisha ubovu. Utengenezaji wake unakuwa na gharama kubwa sana. Nashauri wapewe mafuta ili kufanya kazi zao ipasavyo, ukizingatia uharamia na wizi kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia nikawa mzima wa afya kamili, nikaweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kukushukuru wewe na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wako wote, kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote, kwa jinsi walivyoandaa hotuba ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana serikali, kwa kuanzisha tena JKT, kwa vile vijana wetu wengi wamepoteza mwelekeo na kutokuwa na kazi za kufanya, kiasi kwamba watoto au vijana wakimaliza shule, wanashindwa kuajiriwa na kushindwa la kufanya na kusababisha ongezeko kubwa la waporaji, majambazi walaji unga na mwisho kusababisha janga kubwa la Ukimwi na kupunguza nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hili ni Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, naamini vijana hao watakaochukuliwa, watakuwa ni wa Kitanzania sio kwa kuwabagua hawa ni wa chama Fulani, hawa ni wa Chama Tawala, serikali kutumia vigezo kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuanzisha JKT ni lazima tuanzishe mazingara yaliyo mazuri ili vijana wetu waandaliwe katika maadili yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maafa makubwa yaliyotokea Mbagala, serikali iliahidi kutoa taarifa mbona mpaka leo taarifa haijatolewa kuhusu nini kilitokea mpaka maafa hayo makubwa yakatokea? Wananchi wamepata maafa makubwa na kupoteza makazi, samani na watu wao. Tunaiomba serikali iharakishe tathmini ili wananchi wasizidi kuteseka, kwa kukosa mahali pazuri pa kuishi. Vile vile katika tathmini ya mwanzo, serikali ilikataa kulipa nyumba nyingi kutokana na kutopata madhara makubwa; je, wananchi maskini watapata wapi pesa za kutengeneza?

Mheshimiwa Spika, kuna usemi usemao; "usiziba ufa utajenga ukuta." Sasa huo ufa usipotengenezwa ukuta ataujenga nani?

Mheshimiwa Spika, naiomba serikali ihakikishe watu wote waliopata maafa japo madogo, basi wawalipe vinginevyo serikali itakuwa haikuwatendea haki wananchi hao. Vile vile katika maafa hayo, watu wengi walipata matatizo ya afya zao, macho na masikio; je, Serikali bado inaendelea na jitihada za kuwatibu na je wote wamepata matibabu?

Mheshimiwa Spika, wale waliopoteza maisha yao serikali inasemaje?

Mheshimiwa Spika, kwa vile Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni la Muungano, naomba serikali ikitoa vyeo itoe kwa uwiano. Vile vile vijana wakiajiriwa, wasiangalie vyama wanavyotoka, kwani Zanzibar kuna upendeleo mkubwa katika kuajiriwa jeshini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia mawazo yangu, natumaini serikali itawafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI**: Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kwa kurejesha mafunzo ya JKT nchini. Naishauri iweke utaratibu mzuri wa namna ya kuwawezesha watumishi wote, ambao hawakupitia JKT, kipindi iliposimamishwa ili kila mmoja aliyestahili kwenda JKT aende.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu limejikomboa kwa kurejesha JKT, naipongeza Serikali sana. Watanzania wenye umri mdogo, wamezaliwa na kukulia katika nchi yenye mfumo wa vyama vingi, nchi yenye watu wenye pesa nyingi na watu wenye kipato kidogo sana, nchi inayoendelea na haiwezi kujitenga na mfumo duni, ulio na mabadiliko tele. Nchi yenye demokrasia iliyokua haraka, kwa kweli ni JKT itakayoturudisha katika mstari nyoofu. Naomba mjipange vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali ianglie Kambi ya Kaboya 21 JK. Ni miaka mingi ninaomba wajengewe hospitali ya Jeshi. Kambi hii hutoa huduma kwa vijiji vilivyozunguka bila ubaguzi vikiwemo Itoju, Kabale, Izigo, Bushumba, Katoke, Kimbugu, Nyakashenye, Bisole, Mayondwe, Bugasha na wengineo. Hospitali ndogo waliyonayo, inatoa huduma nzuri sana; naomba ipatiwe jengo la kutosha kutoa huduma kwa familia za askari hao na wananchi wanaozunguka. Nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali ikipatie Kikosi 21 KJ Kaboya, usafiri wa basi kwa ajili ya askari na familia zao. Kwa sasa, tunashukuru kwa huduma tulizowahi kupewa likiwemo lori moja zuri. Hata hivyo, lori siyo usafiri unaofaa kwa wakati wote kwa askari na familia na majirani zao. Nitafurahi sana ombi hili likipewa uzito na kupata jibu jema.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. ANTHONY M. DIALLO**: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ilemela limo katika Wilaya ya Ilemela, ambayo ni Wilaya mpya. Hadi sasa, Wilaya yetu haina Hospitali ya Wilaya, Tunaomba JWTZ ifikirie kuruhusu hospitali yake iliyo Wilayani Ilemela iwe pia Hospitali ya Wilaya ya Ilemela na kuwa na Daktari wa Wilaya na kadhalika.

Hivi karibuni Wanajeshi wa Kikosi cha Anga Kiwanja cha Ndege Mwanza, walivamia eneo la Nduku na kuvunja nyumba za wananchi. Taarifa ilitolewa kwa Mkuu wa Wilaya na Mkoa. Jeshi halina haki ya kutafuta sheria na hawawezi kunyakua ardhi bila kufuata sheria. Kama wana shida ya ardhi, inabidi wafuate sheria kwa kuwafidia wananchi ili watoke kwenye eneo kihalali. Naomba yafuatayo waliohusika waadhibiwe; Wananchi waliovunjwa na kuharibiwa mali zao walipwe fidia; na Wizara ipeleke Maafisa wake kuwaomba radhi wananchi walioathirika na vitendo vya wanajeshi hao.

Taarifa kamili naomba uiombe toka kwa Mkuu wa Wilaya au Mkoa Mwanza.

Naomba jibu wakati Waziri akifunga hoja/mjadala wake.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Watendaji wenzake, kutokana na hotuba yao iliyowasilishwa hapa mbele yetu.

Hotuba inaeleweka na inakidhi kwa kiasi fulani, dhamira na malengo ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, bado nina masikitiko kuhusu masuala ya ajira ndani ya Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa taarifa tuliyoipata ni kwamba, miezi miwili hapo nyuma, vijana waliandikishwa na kupimwa; hata hivyo, idadi ya vijana waliotakiwa haikufikia kutokana na matatizo mbalimbali ya kiafya.

Mheshimiwa Spika, Wizara tunaiomba ihakikishe idadi iliyosalia inajazwa na Vijana wa Zanzibar ili nafasi yao isipotee na ioane na taratibu za kimuungano. Nathibitisha kwamba vijana wapo wa kutosha.

Kwa wale wanaobainika wana maradhi madogo madogo na yanatibika bila ya usumbufu, tunaomba wasaidiwe kwa sababu hakuna aliyekamilika. Pia kwa hao ambao walikwisha kupimwa, waangaliwe kama matatizo yao ni madogo wapewe fursa ili wajiunge.

Kwa wale wajanja wa kuiba vyeti, Jeshi lihakikishe hakuna msamaha.

Nashukuru kwa dhati kutokana na jitihada zetu katika kazi ngumu. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE**: Mheshimiwa Spika, michango yangu ni kuboresha Jeshi letu.

Iwepo mikakati mahususi kabisa kuhusu Jeshi letu, wakati ndio huu tusingoje vita au matatizo.

Mheshimiwa Spika, Makambi yote Tanzania ni machafu, hayana ardhi, ukilinganisha na kazi inayofanyika au iliyofanyika wakati wa Nduli Iddi Amini, ilikuwa

ni ukombozi mkubwa hasa kuanzia Mkoani Kagera kwenyewe, Rwamishenye, Kaboya, Biharamulo, Makao Makuu ya Jeshi Mkoa Twiga. Hivi serikali inaridhika kabisa kuona wanavyoishi watu hao? Mishahara na posho zao ndogo sana; hivyo askari ana mke na watoto maisha hayo hasa huu mtikisiko wa uchumi hata wewe mwenyewe ukipewa elfu tano hiyo kama haitaishia kwenye chai tu. Chakula kutoka kwa wazabuni, wakati umefika wapewe pesa yao waweze kujipangia bajeti yao. Wapewe pesa ya mwezi mzima wakahemee wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mara kwa mara maswali yanaulizwa Bungeni kuhusu wastaafu; je, bajeti hii imewaweka wapi? Je, pensheni zao zimeboreshwa au ndio hivyo? Ngoja ngoja miaka inapita na hilo linakatisha tamaa vijana kujiunga na Jeshi, wakiona wastaafu hawakumbukwi, wengine walemavu, viziwi, vipofu, walikatika miguu na mikono. Je, hili tatizo limefanyiwa kazi vipi?

Mheshimiwa Spika, je, lini serikali itaweka kumbukumbu kama motisha ya sehemu ya Kyaka ambako kuliathirika na vita hivyo, angalau kufanyia hapo Siku ya Mashujaa hata wakazi wa sehemu na wazee wetu watafurahi sana isiwe kutupa jongoo na mti wake?

Mheshimiwa Spika, kuna magofu mengi serikali ikiyathamini yataweza kuwa utalii mmojawapo. Hii ni changamoto serikalini.

Mheshimiwa Spika, wahalifu kwenye mipaka yetu nayo ni kero kubwa sana na ina madhara makubwa sana ya kusikitisha, wengine wanapita wamevaa nguo za Kimasai wakifika ndani wanavua; hivi wizara na serikali mnalijua hili? Je, inalisemaje kuwa na vitambulisho?

Je, ulinzi wenyewe ukoje au tulifanyeje kupambana nalo au kumaliza kabisa wizi wa ng'ombe, mauaji kwa wakulima, wananyang'anywa ng'ombe wao, wanapigwa wanauawa pamoja na kubakwa. JKT nitashukuru kurudishwa, lakini kuna mambo muhimu yafuatayo:-

Wale vijana waliojifunza silaha za moto, baada ya hapo wakarudishwa mitaani; je, Serikali haioni wakiendelea kukaa huko wanaweza kujifunza uhalifu? Wapewe kipaumbele cha kwanza kwenye ajira. Tusiendelee kuwatupa na lisiwe tatizo.

Tutoe vipaumbele kwenye vitendea kazi; magari, pikipiki na vifaa vingine vyote.

Kuna tatizo la jeshi lililoko Kigamboni, linalotengeneza boti. Hicho kikosi kinafanya kazi nzuri sana, kiboreshwe waweze kufanya kazi kwa usanifu mzuri, boti hizo zitasaidia sana hata Ziwa Victoria tunaweza kupata mbili. Sisi tuna wahalifu wengi sana, lakini polisi hawana vitendea kazi vya kutosha.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Jamhuri ya Muungano ni chombo muhimu sana, ambacho majukumu yake ni makubwa kwa ulinzi na usalama

wa nchi yetu.  Chombo ambacho ni jasiri, kwa mfano, kule Comoro kilifanya kazi vizuri bila athari yoyote; hivyo kuna haja ya kukipongeza.

Mheshimiwa Spika, ajira za Jeshi kwa upande wa Zanzibar hususan Pemba, zimekuwa za ubaguzi zaidi, kwani ajira hizo hupitia kwa Masheha na Wakuu wa Wilaya; hivyo ajira hizo huenda kwa watu wa aina moja; ingekuwa bora zitangazwe ili watu wengine waweze kupata ajira hiyo,  kwa maana wako wengi wenye uwezo wa kujiunga na ajira hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi ni la Muungano lakini JKT si Chombo cha Muungano; hivyo si kuchanganya mambo mawili ambayo utekelezaji wake ni tofauti kidogo, ingawa kazi zao zinalingana hasa kwenye masuala ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Jamhuri ya Muungano ni chombo cha ulinzi, hivyo kujishirikisha kwenye mambo ya siasa kama kule Konde Pemba hivi sasa kwenye uandikishaji wa Daftari la Wapiga Kura ni kutolitendea haki kwa vile wananchi wana imani sana na chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, mabomu yaliyolipuka Mbagala ni aibu sana kwa chombo hicho, hivyo basi lazima ripoti itolewe ili kujua ni sababu gani ya msingi iliyotokea mpaka kukatokea maafa makubwa kwenye chombo hicho.

**MHE. MANJU SALIM MSAMBYA**:  Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja kwa kuwatakia Wizara kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pamoja na kuunga hoja mkono nina haya ya kusema:

Serikali iliamua kufanya jambo zuri la kupeleka Vikosi vya Jeshi katika maeneo Fulani fulani ya nchi yetu, hususan mipakani, ambavyo vinajulikana kwa lugha ya Jeshi kama *detach.*  Nia ya vikosi hivi au *detach* ni kuimarisha doria na ulinzi hasa mipakani.

Kwa upande wa Kigoma, tunashukuru kupatiwa *detach* hizo karibuni mwambao wote wa Ziwa Tanganyika.  *Detach* hizo zipo pia Mkoani Rukwa (Ziwa Tanganyika) katika Jimbo la Kigoma Kusini, ambako mimi ni mwakilishi.  Zipo *detach* maeneo ya Vijijni vya Karago (Kata ya Sumika), Kijiji cha Kirando (Kata ya Sumuka), Kijiji cha Singunga (Kata ya Singunga) na Kijiji cha Rukoma (Kata ya Igahila na Bulingu).

Napenda serikali inijulishe inaendeshaje shughuli za ulinzi na doria bila kuwapa wanajeshi wetu vitendea kazi? Doria lazima zifanywe kwa kutumia mitumbwi, *engine* za kusukuma mitumbwi hiyo, pamoja na mafuta (petroli) na vilainishi.  Kwa nini watumishi wa *detach* hizi wanakuwa ombaomba wa vitendea kazi toka kwa wavuvi?

Je, Wizara ya Ulinzi isingeona kuwa ni busara kuwapa vitendea kazi wapiganaji wake?  Hata hivyo, napenda nieleze masikitiko yangu kwa wapiganaji wetu walio Vituo vya Mkoa wa Kigoma, kwa kitendo cha kujidhalilisha. Wavuvi wanachangia petroli/vilainishi, kila mtumbwi wa mvuvi unachangia lita tano kuwapa wanajeshi hao.

Inajitokeza kuwa, viongozi wa *detach* hizi wanayauza mafuta haya kwa baadhi ya wavuvi hao wanaochangia. Wanayauza kwa bei rahisi chini ya ile ya soko. Hivi wavuvi wanatoa petroli/vilainishi hivi kwa nia kwamba wanajeshi wetu wafanye biashara? Wavuvi wetu wanavamiwa kila mara majini wakati wakiendesha uvuvi ziwani. Jeshi halijaonesha juhudi ya kupambana na majangiri hawa waziwani kwani wavuvi wananyang'anywa na kuuwawa kila mara.

Ni kwa namna gani Jeshi la Ulinzi na JKT wamesaidia kuvirejesha vifaa vilivyoporwa na kuthibitika kuwa vimekamatwa kule Kongo na taarifa kutolewa Serikalini?

Hivi karibuni wapo wavuvi waliokamatwa na kunyang'anywa zana za uvuvi Kata ya Sumka Kigoma Kusini na kupelekwa pamoja na zana zao hadi DRC na wakatupwa majini karibu na Pwani ya Ziwa Tanganyinga upande wa DRC. Mmoja wa watu hao, napenda nitangaze maslahi kuwa ni mwanangu, kwani ni mtoto wa kaka yangu. Imebainika kuwa, Serikali ya DRC tayari imekamata zana za kijana huyu, pamoja na wenzake, lakini wanaelezwa wapeleke fedha za kukomboa mali (zana) zao. Kwanza, hawa watu wamenyang'anywa mali za kuzalishia; na pili, vijana hawa wamepata taarifa kwenye *detach* zao za Sumka, yaani Karago na Kirando, lakini hakuna msaada.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA**: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kazi kubwa mnazofanya za ulinzi na ujenzi wa Taifa. Hata hivyo, ninayo maelezo ninayotaka yapate majibu.

Ipo *Detach* ya Kasanga katika Jimbo langu la Kalambo, imefanya kazi nzuri ya ulinzi lakini kumetokea dhoruba za hapa na pale, mfano, askari kujiingiza katika ugomvi wa raia mfano huko Kapele, Kitongoji cha Kantalamba. Hii ni dosara mbaya, naomba irekebishwe mapema. Pili, kuingilia wavuvi wanaovua Ziwani bila mpango, kuwapiga na kuwalazimisha mambo yaliyo chini ya Wizara ya Uvuvi. Naomba kuwe na maelewano na raia badala ya kuvurugana.

Kuhusu eneo la Bismark Fort ambayo ni ngome ya zamani iliyokuwa Makoa ya Jeshi la Ujerumani, eneo hili lina magofu mengi ya kumbukumbu za kale. Watalii toka Ujerumani huja kuona ngome hii, lakini kwa mshangao hufukuzwa eti ni Makao Makuu ya Kijeshi. Kwanza ni aibu kubwa, *detach* yetu kuendelea kuishi katika magofu. Tumelisema hili miaka nenda rudi. Je; ni lini mtajenga *detach camp* juu ya eneo la Bandari ya Kasanga badala ya kugombana na wananchi?

Limetokea tatizo lingine la Jeshi kunyang'anya viwanja kadhaa vilivyopimwa pale bandarini, vikiwa vimejengwa tayari msingi wa ujenzi wa hoteli ya kitalii. Hii sasa ni vurugu. Kama tayari mmetoa fedha za ujenzi, badala ya kugombana na wananchi kwa kiwango hicho, namsihi Waziri aje Kasanga atatue jambo hili. Yapo maeneo mazuri kwa ujenzi wa Kambi, badala ya kutumia nguvu kugombana na wananchi na kutumia nguvu za kijeshi. Hili naomba majibu.

Mwisho, naomba wanajeshi hawa wapewe vifaa vya kutosha vya majini kwa ajili ya patrol na magari safi kwa ajili ya usafiri wao.

Kwa uanzishaji wa Kambi za JKT, Rukwa tulikuwa na Kambi ya Luwa JKT; fufueni kambi hii au eneo lolote.

Jimbo langu la Kalambo tuko tayari kutoa eneo la kutosha kwa ajili ya Kujenga Kambi na maeneo ya miradi na mafunzo, mfano, eneo la Matai, eneo la Sundu (Mwazye) au eneo kati ya vijiji vya Katuka na Mao, linalofaa sana kwa kilimo cha mazao ya mahindi, alizeti, maharage na matunda ya aina zote.

Naunga mkono hoja na kuomba majibu ya hoja zangu za *Detach* ya Kasanga na ombi la Kambi ya JKT.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Watendaji wote katika Wizara na vikosi mbalimbali katika Jeshi hili

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa ushirikiano mkubwa nilioupata katika Jeshi hili Mkoani Tabora – Urambo, pale nilipohitaji kuonana na akina mama ambao ni wake wa maaskari na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali kama utengenezaji wa batiki, sabuni, maziwa ya soya.

Mheshimiwa Spika, akina mama hao wana moyo na wanapenda sana kujiendeleza kimaisha, naomba nitoe ushauri wangu kuwa, kama itawezekana akina mama hawa kuwa na SACCOSS ambazo zitapata msaada wa kuwaendeleza, kwani unapotambua mchango wa mwanaume, utambue pia na mchango wa mkewe ili askari hawa hata watakapotoka kazini, kuwe na miradi ya kifamilia kuondokana na umaskini. Huu ni ushauri tu.

Nampongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa ushirikiano kwanza kwa Wabunge na katika vikosi vyao maeneo mbalimbali. Kivi karibuni, Naibu Waziri amefanya ziara Mkoani Tabora, tuna imani ziara yake imeona makazi ya askari hao na itazingatia kuboresha maisha yao ya makazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuishauri Wizara au Jeshi, kuangalia ujenzi wa Kituo cha Ndege Mkoani Tabora, ambacho kitakuwa ni Kiwanja cha Jeshi, kwani Tabora kuna historia na inafahamika ni mkoa muhimu sana kwenye jeshi hili. Kuwa na kiwanja chao ni jambo ambalo litaimarisha Jeshi hili, kwani Mkoa huo hauna barabara imara. Reli pia si nzuri, uwanja wa ndege tulionao si mkubwa, hauna ubora, mvua inaponyesha ndege hazitui. Tunajua umuhimu wa Tabora tunajiandaaje?

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa Jeshi kwa janga la Mbagala, kwani hakuna jambo lisilo na hasara na kuna mambo ambayo hayazuiliki.

Mheshimwa Spika, tuangalie kwa umakini mipaka ya maeneo ya Jeshi, kwani kuna matatizo makubwa sana kwa wananchi kuingilia maeneo ya Jeshi. Tuzuwie tatizo kuliko kusubiri mpaka litokee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja. Kwanza, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa utendaji wao wa kazi mzuri. Ukiachia tatizo la upungufu wa Bajeti yao kuwa ndogo kila mwaka, wamekuwa wavumilivu sana na wanajitoa kwa dhati kulitumikia Taifa hili. Mungu azidi kuwabariki.

Aidha, nampongeza Mkuu wa Majeshi na Wasaidizi wake wote na Maafande wote. Baada ya pongezi hizo, naomba nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, umri wa kustaafu wanajeshi (askari) ni kutokana na jinsi wanavyopanda vyeo vyao. Hivyo, wengi wao hustaafu wakiwa na umri mdogo. Hali hiyo husababisha maisha yao kuwa magumu sana wawapo uraiani, kwani hushindwa kumudu maisha japo hulipwa kiinua mgongo.

Wengi wao huwa na majukumu ya kulea na kusomesha watoto wao, kwa kuwa huoa wakiwa na umri mkubwa, kutokana na sheria au kanuni za Jeshi kuwataka wasioe au kuolewa hadi kufikisha miaka mitatu kazini.

Mheshimiwa Spika, ugumu wa maisha, huwapelekea wengine hata kujiingiza katika shughuli zisizo halali ili kukidhi haja za maisha yao.

Nashauri askari wanaoelekea kustaafu wakiwa na umri mdogo, wapewe muda maalumu wawapo kazini, kujiunga na kozi za ualimu au uuguzi kulingana na elimu zao ili wafikiapo kustaafu, wasaidie kufundisha katika shule zetu za Kata kulingana na utashi wa mtu mwenyewe, kwa kuwa bado tuna tatizo la walimu na wauguzi katika zahanati zetu za Kata. Hali hiyo itawapa nafasi nzuri askari hawa kujikimu kimaisha pia kutumikia taifa hili kikamilifu. Kuhusu utaratibu wa askari hawa kupatiwa mafunzo ya ualimu na uuguzi, naomba tuwasiliane niko tayari kutoa ushauri.

Naomba Wizara iweke utaratibu wa kutoa mikopo ya nyumba, pindi tu askari anapooa au kuolewa ili afikiapo muda wa kustaafu, awe ameshamaliza deni lake na hivyo kutoa mwanga kwa kiinua mgongo chake kufanya kazi nyingine na kuyafanya maisha kuwa mazuri.

Naomba ulinzi mipakani, Jeshi lishike nafasi yake ili kutokutoa mwanya kwa maharamia wa nchi jirani, kuingia na kusababisha mtafaruku ndani ya nchi yetu. Mfano, Tarime wizi wa ng’ombe wa nchi jirani unasababisha ugomvi mkubwa sana wa kikabila baina ya Watanzania waishio huko. Hivyo, endapo Jeshi litaimarisha ulinzi katika mpaka wa maeneo husika, litapunguza wizi usiotazamiwa na kudumisha amani na imani miongoni mwa wananchi.

Naomba Wizara ijitahihidi kuomba fungu la kuongeza mishahara ya askari wetu ili kupunguza udhalilikaji wa askari wetu wapitapo mitaani na kuondoa vishawishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimwa Waziri na timu yake yote, kwa hotuba yao nzuri sana. Zaidi sana, naipongeza pia Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa kazi nzuri ya kuipa nguvu Wizara hii.

Naomba kuchangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya vigezo vinavyoonesha kuwa Wananchi/Watanzania wako nyuma kimaendeleo ni tabia ya kuibaiba na hasa wizi wa mifugo. Hii ni tabia ya kishamba sana, kwa kuwa mtu yeyote mstaarabu hawezi kuwa na tabia ya kumwibia mwenzake mali yake. Wilaya zetu za wafugaji, hasa Manyara kuna tabia hii. Naiomba sana Serikali, itafute suluhisho la kudumu la kukomesha wizi wa mifugo, kwa kuwa tabia hii inapelekea kukosa amani katika jamii. Amani, utulivu na usalama, ndiyo kaulimbiu ya Tanzania.

Mheshimwa Spika, kwanza, niishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuirudisha JKT. Hii itawajengea afya njema, maadili na nguvu, vijana wetu kama ilivyokuwa zamani. Pia itapunguza muda wa vijana wengi kubakia katikati ya jamii na kuzurura au kufanya uhalifu. Badala yake tunaimarisha nguvu kazi ya Taifa letu.

Pamoja na pongezi hizi, naomba vijana wa kike wapewe fursa nzuri ya kushiriki mazoezi haya bila kuwabughudhi na kuwapotezea muda. Kuna baadhi ya viongozi wanatumia madaraka yao vibaya, kuwasumbua vijana wa kike wakiwa kambini. Serikali iweke mikakati mahususi, kuwalinda askari wa kike, tukizingatia hali halisi ya sasa ikiwepo maradhi sugu kama UKIMWI na kadhalika.

JKT iwe chanzo cha kuzalisha mali ili kuinua Pato la Taifa. Badala ya mazoezi yasiyo na tija na adhabu nyingi sana huko Jeshini, vijana watumiwe kuzalisha mali au kufanya mazoezi ya maonesho ya kulipia ili kuinua Pato la Taifa. Pamoja na hali mbaya ya kiuchumi, bado faida ni kubwa kuliko hasara kwa kuwapeleka vijana wetu JKT. Mimi naliunga sana mkono jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote, kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuwa na mpango mzuri sana wa kurejesha tena mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Mafunzo hayo ni muhimu sana kwa Kujenga Taifa la watu wenye nidhamu, akili, ujasiri, ubunifu, uvumilivu, uchapa kazi na wanaowajibika.

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia vijana kibao wanakimbilia mijini wanataka kazi nyepesi, wanapokosa wanaishia kwenye magenge ya kunywa pombe, kuvuta sigara na kucheza bao. Lengo la mafunzo haya ni kurejesha tena Taifa la Wazalendo. Naomba Serikali iharakishe mpango huu mzuri mwaka huu, wale wote waliomaliza form four, form six, colleges na short courses, waende kwenye mafunzo wakati wanasubiri cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, makambi yetu hapa nchini yamejengwa jirani na makazi ya raia. Hii ni hatari sana kwa usalama wa wananchi wetu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia balaa iliyotupata Kambi ya Jeshi ya Mbagala; watu wamepoteza maisha, mali zao, kupata ulemavu na wengine kuathirika kisaikolojia. Tunaomba Ripoti ya Wataalam walioteuliwa kuchunguza tatizo hilo, itolewe mapema ili Serikali ichukue tahadhari kwa makambi mengine. Kuendelea kuchelewa kwa taarifa hiyo, inaleta mashaka kwa Watanzania kuwa Serikali haijui nini maana ya jambo la dharura! Tunasubiri mabomu yalipuke tena kwenye kambi nyingine?

Mheshimiwa Spika, kinga ni bora kuliko tiba. Serikali kukalia taarifa hiyo, inaleta maswali mengi yasiyokuwa na majibu.

Mheshimiwa Spika, tabia ya wanajeshi kujichukulia sheria mikononi, haipendezi kwenye macho ya jamii. Askari yeyote ni kioo kwenye jamii, mtu akionewa akiwepo askari anajua atamtetea. Sasa wanapoamua kumwadhibu raia wakati kuna vyombo vya sheria, siyo vizuri wanajidhalilisha!

Serikali imekuwa inapeleka wanajeshi wetu kupigana nchi za nje na kurejesha Amani maeneo mbalimbali. Najua katika vita kuna kushinda na kushindwa, katika kupigana kuna kuumia, kuuwawa, kunusurika na kadhalika. Kwa ufupi, askari anapotaka kwenda vitani, anawaza mawili; kurudi salama au kutorudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Serikali yetu ikaweka bima ya maisha ya askari wetu kabla ya kwenda vitani. Kazi yao ni hatarishi sana, hivyo watazamwe vizuri na watendewe haki ya msingi. Pia mishahara yao iangaliwe ilingane na kazi kubwa wanayoifanya.

Pensheni za wastaafu wa Jeshi ziendane na hali ya maisha inavyopanda.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kulipongenza Jeshi la Wananchi, kwa kazi nzuri sana wanazozifanya na nimpongeze Waziri pia kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili tu, ambayo ningemwomba Waziri anipatie majibu. Maswali hayo ni kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa idadi kubwa ya wanajeshi wanatokea Kanda ya Ziwa na kwa idadi kubwa wanatokea Mkoani Mara; na kwa kuwa kwa muda mrefu sasa Mkoa wa Mara

umekuwa katika mapigano ya muda mrefu ya koo kwa koo na yale yatokanayo na wizi wa ng'ombe na yale yatokanayo na migogoro ya ardhi; hivi ni kwa nini Wizara haijaona umuhimu wa kuwatumia wanajeshi hao toka Mara katika majadiliano yanayoendelea katika kukomesha vita hivi Mkoani Mara? Jeshi la Wananchi linasema nini kutokana na kukosekana kwa amani katika Wilaya ya Tarime kwa muda mrefu sasa?

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kujua ni nini mikakati ya Wizara katika kuhakikisha wanapata meli za kivita katika bahari yetu na hasa upande wetu wa Tanzania hasa tukizingatia vitendo vya maharamia vinavyokua siku hadi siku?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba kuwasilisha.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wote, walioshiriki katika kuandaa makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka huu wa 2009/2010; imeandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa nchi jirani zinazoizunguka Tanzania, zimekuwa na misukosuko na uvunjifu wa amani katika nchi zao kama Kenya, Uganda, Burundi na kadhalika, lakini sababu ya umahili wa Jeshi letu, nchi yetu ya Tanzania kwa kiasi kikubwa imeendelea kuwa na amani, utulivu na usalama. Nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo, bado ujambazi wa kutumia silaha unaendelea katika maeneo ya mpakani hususan Mkoani Kagera. Hivi sasa ujambazi wa kutumia silaha unaendeshwa na majambazi kutoka nchi jirani na kwetu. Wiki mbili zilizopita, askari wetu ameuawa na majambazi huko Biharamulo na majambazi yakaondoka na silaha.

Kwa nini na ni lini Jeshi la Ulinzi na Usalama pamoja na asasi nyingine na majeshi mengine yanayohusika wataweka mkakati wa kudumu/endelevu wa kulinda mipaka yetu na kuzuia ujambazi huu?

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa kilichotokea Mbagala ni ajali. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwani madhara yangeweza kuwa makubwa zaidi. Mkiiangalia Dar es Salaam, Makambi mengi ya Jeshi yako karibu na makazi ya wananchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaweka watu au makazi ya watu mbali na Makambi ya Jeshi ili kuepusha ajali kama hizi?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa tamko lao la kurudisha JKT. Vijana wetu wengi wamekosa ukakamavu, uvumilivu na uzalendo. Wamelelewa kama mayai. Najua vijana wanaohitimu Kidato cha Nne na cha Sita ni wengi sana, Makambi ya JKT yaliyokuwepo, hayajaongezeka mengine na hata ubora wake umeshuka. Ili zoezi hili lilete manufaa, inabidi maandalizi makubwa ya miundombinu husika yafanywe. Je, Serikali ina mpango gani mkubwa wa kuweza kuchukua vijana wote hao?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nilipongeze Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa nidhamu waliyokuwa nayo wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, hali za wanajeshi wetu bado si za kuridhisha. Posho za wanajeshi wetu ni ndogo sana; Sh. 5,000 kwa mwanajeshi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, makazi ya kijeshi si ya kuridhisha. Vitendea kazi vya wanajeshi ni vya hali ya chini kabisa mfano, magari ya Land Rover hayaelekei kabisa kufanyiwa kazi na Jeshi, ni mepesi kwa kazi za kijeshi, wanajeshi wanunuliwe magari mazito, madhubuti kwa kazi kama vile Land Cruiser.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kuunda Jeshi Dogo la Ulinzi la Wananchi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa; Jeshi Dogo hata liwe na taaluma, zana na vifaa vya kisasa kama nini, lakini udogo una athari mbaya wala hausaidii chochote.

Mheshimiwa Spika, kwani kuwa na Jeshi kubwa lenye sifa hizo zilizotajwa kuna ubaya gani?

Mheshimiwa Spika, kazi ya Jeshi ni ya kugangamala, kazi ya kijeshi isiwekwe sawa na uraia, tusiwe na Jeshi likawa sawa na raia.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wanajeshi wanastaafu wakiwa wadogo?

Mheshimiwa Waziri amesema, Wizara imelinunulia Jeshi vifaa vya kutendea kazi, mbona zinapotokea ajali hatuoni vifaa hivyo vikitumika kwa haraka? Mfano, hivi karibuni kule Zanzibar, kumetokea ajali ya kuzama kwa meli pale Bandarini, lakini meli ile imekaa wiki nzima bila kuokolewa na Jeshi la uokozi lipo; kulikoni?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi (Mb) - Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi (Mb) - Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa JWTZ - Jenerali Davis Mwamunyange, Mkuu wa Utawala - Generali Abdul-rahmani Shimbo, Makamanda na Wapiganaji wote wa JWTZ na JKT.

Mheshimwa Spika, Majeshi yanafanya kazi sana, yamefanya kazi ya ulinzi wa mipaka yetu na yanatumika katika shughuli mbalimbali na masuala ya kimaendeleo kitaifa, ikiwemo ile ya kushiriki katika majanga mbalimbali pale yanapojitokeza.

Mheshimiwa Spika , pamoja na kazi hiyo nzuri, lakini ni ajabu Wizara ambayo inalo jukumu kisera katika jeshi, bajeti yake kwa muda wote haitoshelezi; ni aibu kwa jeshi letu kuwa katika uhaba wa vitu mbalimbali zikiwemo uniform na nyingine muhimu za kufanyia kazi, magari na kadhalika. Kudharau au kutokutoa kipaumbele kwa jeshi

kupatiwa zana bora za kazi ni hatua za kuhatarisha nchi kwa masuala mbalimbali, yakiwemo ya kiulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu kwa serikali, itilie mkazo mahitaji yote na kuyatekeleza bila kuyasogeza mbele kwa mwaka wa fedha ujao.

Jeshi (Makambi), lazima yawe mbali na maeneo ya wananchi. Makambi yaliyojengwa ambayo yapo maeneo ya makazi ya watu, basi ule utaratibu wa ujumbe wa raia kuwa umbali wa mita 500 (eneo la Buffer Zone), uheshimiwe ili yasije yakajitokeza yale yaliyojitokeza Kambi ya Jeshi Mbagala, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii, nitoe rambirambi kwa ndugu, jamaa na Watanzania wote waliofiwa na jamaa zao kupitia tukio hilo la kusikitisha. Nichukue nafasi hii, kutoa wito kwa serikali kutoa fidia kwa wahanga wote waliopoteza maisha yao na siyo vibaya kuwatumikia nishani ya ushujaa uliotukuka, kwani walikuwa kazini na katika kuhakiki silaha zetu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia serikali ikaona umuhimu wa kutoa fidia ya haraka, kwa waliopoteza nyumba na mali nyingine kama hatua ya kuwafariji. Kufanya hivyo, itakuwa ni kusahihisha makosa ambayo Serikali kupitia Mamlaka zake, walishindwa kusitisha ujenzi holela kuzunguka Kambi hiyo ya JWTZ Mbagala.

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kupitia Hotuba ya Waziri Mkuu, kuhusu shabaha ya serikali kurejesha JKT kwa Mujibu wa Sheria, hasa kwa vijana wanaojiunga na Vyuo Vikuu. Mpango huu ni mzuri sana, kwani utasaidia katika maandalizi ya kwajengea maadili ya uzalendo, vijana wetu ambao ndio tegemeo la kuwa viongozi wa nchi yetu kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu huo, unaolenga vijana ambao watabahatika kwenda Vyuo Vikuu; ni vizuri pia kama utaratibu huu ungewagusa vijana wote, hasa wale wanaohitimu Kidato cha Sita, kwa maana itakuwa ni maandalizi ya kuwaandaa katika maisha, kimaadili na kadhalika. Kuendelea kuwaacha vijana kuzagaa bila maandalizi ya Taifa; ni hatua ya kutokuliandaa Taifa la baadae kwa masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi ambao wanatumika kwenye Vikosi vya Umoja wa Mataifa kulinda Amani *(Peace Keeper),* kama tulivyowapeleka Dafur, ningependa Mheshimiwa Waziri aeleze utaratibu wa malipo yao uko vipi? Wapinganaji hawa ni muhimu sana, kwani pamoja na mambo yote, bado watasababisha nchi yetu kupata vifaa vya kisasa vya kivita, mara baada ya kukamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nitoe rai kwa Waziri juu ya kuwa na mipango ya kulitumia JKT kwa shughuli ya kilimo katika maeneo mbalimbali yenye rutuba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, wapiganaji wanaposhiriki katika shughuli za kuleta amani katika nchi mbalimbali ni marupurupu gani ambayo wanapewa zaidi ya mshahara wa kawaida? Marupurupu haya hulipwa kwa utaratibu gani na kasi ipi?

Marupurupu wanayolipwa zaidi ya mshahara ni Mission Service Allowance, kulingana na MoU kati ya Jamhuri ya Muungano wa UN. Posho ya Wataalamu *(Specialist Allowance).* Viwango MSA, kwa mfano, katika kikundi kilichopo Lebanon ni $ 1,028.00 kwa mwezi.

Utaratibu unaotumika kuwalipa ni kupokea fedha toka UN DPKO. Maafisa wa Askari hulipwa wakiwa katika eneo la ulinzi wa amani na wengine kwa maombi yao, hulipiwa Tanzania kupitia akaunti zao.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na JKT, Naibu Waziri, Mkuu wa JWTZ, Makamanda na Wapiganaji wetu. JWTZ ni Jeshi la Ukombozi wa Bara la Afrika. Watanzania wanayo fahari na wajivunia jeshi lao.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na JWTZ, kulinda mipaka ya nchi yetu, ndiyo chimbuko la amani tunayojivunia Watanzania wote. Mungu ibariki JWTZ.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Rorya, naomba sasa nichangie kwa kutoa ushauri, kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kama ifuatavyo:-

Mipaka ya nchi yetu na nchi jirani ya Kenya iko wazi, hususan mipaka katika Wilaya ya Rorya na Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Waziri, alishuhudia hali hiyo alipotembelea Kata ya Bukwe, kutokana na wizi wa mifugo uliofanywa na majambazi kutoka nchi jirani, kwa kushirikiana na wakala wao.

Kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2009, ng’ombe wapatao 2,500 wametoroshwa kwa kutumia silaha za kivita na wananchi wapatao 40 wamepoteza maisha yao kwa kuuawa.

Mheshimiwa Spika, haya yanapotokea, majambazi hao hutoa taarifa mapema na wanapokuja kuchukua mifugo, hupiga bunduki kuwatisha wananchi ambao hawana silaha.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu limefanya kazi ya kulinda mipaka yetu kwa uzalendo wa hali ya juu na nidhamu ya kuigwa. Kwa kuwa mwaka jana, Mheshimiwa

Waziri alipotembelea Wilaya ya Rorya, Kata ya Bukuru, aliwaahidi wananchi kuwa serikali ihakikishe kuwa mipaka yetu na Kenya, ulinzi unaimarishwa. Nashauri serikali itoe tamko rasmi, kupitia Wizara ya Ulinzi, kuhusu ulinzi wa mipaka ya Wilaya ya Rorya na Wilaya ya Tarime haraka iwezekanavyo ili wananchi waweze kuishi kwa amani na kufanya shughuli za maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa mipaka ya Wilaya ya Tarime na Rorya, ulikuwa unafanywa na Kikosi cha JWTZ katika Kambi ya JWTZ Nyondoto. Nashauri Kambi hii sasa ifufuliwe ili kuokoa ng'ombe wanaotoroshwa kwenda Kenya. Tunahitaji wapiganaji wetu kulinda mipaka yetu, wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake. Naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na kuingia dosari kwa usalama na amani katika nchi mbalimbali kama vile DRC, Somalia, Uganda, Ethiopia na kadhalika, kumepelekea kutolewa maamuzi ya kuunda Jeshi la kulinda Amani ili kuhakikisha raia wa nchi hizo wanaishi kwa usalama na amani.

Lakini ni dhahiri kwamba, *operations* za kulinda amani ni za hatari, ambazo wakati mwingine wanajeshi wanaotumikia *operations* hizo, huweza kujeruhiwa au kupoteza maisha kwa kuwa wanajeshi wetu nao pia wanashiriki katika *operations* hizo; na ili kuwaweka wanajeshi wetu katika hali ya utayari, ni vyema kuwawekea mazingira mazuri kama ambavyo wanajeshi wanaotoka nchi nyingine wanaandaliwa.

Mheshimwia Spika, umefika wakati sasa wanajeshi wetu wanaoshiriki katika *operations* za kulinda amani na usalama katika nchi ambazo zina fujo, wawekewe bima za maisha

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wanajeshi ambao walilitumikia jeshi letu kwa muda mrefu na baadaye kustaafu, lakini hadi hii leo mafao yao hawajalipwa. Mimi binafsi, nimejaribu kufuatilia mafao ya baadhi yao, lakini hadi hii leo sijafanikiwa. Aidha, kuna baadhi ya wanajeshi ambao kwa bahati mbaya, wanafariki wakiwa kazini, inachukua muda mrefu na usumbufu mkubwa kwa wanafamilia kulipwa mafao yao, ikiwemo mirathi. Jambo hili limekuwa linalalamikiwa sana na wanafamilia, lakini bado dosari hii imeshamiri. Ni vyema basi, Mheshimiwa Waziri akalipatia ufumbuzi tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwaenzi Mashujaa wetu hasa walioshiriki katika Vita vya Ukombozi wa Afrika, Vita vya Uganda, limekuwa linapigiwa kelele sana, lakini haionekani kwamba, kuna juhudi na mikakati ya kuwaenzi mashujaa hao. Bahati mbaya, wanajeshi hawa wengi wao wamestaafu na baadhi yao wameshafariki dunia. Suala la Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, limeiletea sifa sana nchi yetu.

Sasa ni vyema basi, sifa hii isiishie kwa nchi pekee bali ni busara kwa wale walioshiriki katika vita hivyo nao wakapewa stahili ya heshima hiyo, kwa kuandaa mikakati ya kuwaenzi kama mashujaa walioiletea sifa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atueleze ameandaa mikakati gani kuwaenzi wapiganaji wetu hao na kadhalika kuwapatia mafao yao yote?

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Wapiganaji, walioandaa hotuba hii nzuri, yenye kuonesha mwelekeo wa kazi za Wizara hii. Baada ya hayo, nachangia mambo yafuatayo:-

Nimefurahishwa na mpango wa Jeshi kuwapeleka vijana kwenye mafunzo ya VETA, ambayo ni muhimu kwani inawasaidia kupata taaluma ya kujiajiri wenyewe na kuweza kujitegemea. Naomba idadi iongezwe.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana kwa Serikali kurudisha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria, kwani mpango huu utawezesha vijana kujifunza mambo mengi, ambayo tayari mmeyaorodhesha. Mimi naomba serikali isisitize somo la uzalendo ili kuwawezesha wanapofanya kazi waelewe wako kazini, kwa kuwajibika kwa wananchi na sio kwa kujinufaisha wao tu.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali ijitahidi kuweka fungu la fedha maalum, kwa ajili ya mafunzo ya mgambo. Mafunzo haya yanasaidia mpango wa Ulinzi Jamii na yanasaidia kupunguza ujambazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nawapa pole Wananchi wa Mbagala, ila naliomba Jeshi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vyombo vyake vya kijeshi ili visilete madhara kama ilivyotokea Mbagala.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijenge nyumba za kutosha ili wanajeshi wakae kambini, badala ya kuishi na wananchi ambayo inawapunguzia heshima. Vile vile naomba serikali iwakopeshe fedha za kujenga nyumba zao binafsi. Baadhi yao hujisahau kujijengea nyumba zao kutokana na kukosa muda au kujisahau.

Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Kwanza kabisa, ninapenda kuwapongeza Wanajeshi wote na Wizara, kwa kufanya kazi vizuri, kwani siku hizi matukio ya ujambazi yamepungua. Hongera sana.

Kuna tatizo la Askari wa K.A.R waliopo katika Wilaya ya Ruangwa; hadi leo hawajapata haki zao baada ya vita. Tunaomba Wizara ishughulikie suala hili, kwani linasumbua sana na ni kero kubwa sana. Ninadhani wapo pia katika Wilaya nyingine. Unaweza kukuta habari zao ukichunguza zaidi.

Ni kero kubwa sana huko Ruangwa; juu ya Askari hao wa K.A.R., ambao wanadai *pension* yao. Ahsante.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Nawapongeza sana Wanajeshi wetu, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Jeshi la Kujenga Taifa lianze kuchukua vijana wengi haraka ili kukuza Umoja wa Kitaifa na kujenga nidhamu kwa vijana wetu, hasa wanaomaliza shule na mafunzo mbalimbali.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi (Mb), Mheshimiwa Dkt. Nchimbi (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi, pamoja na Watendaji wote, walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, ninapenda kutamka rasmi kuwa, ninaunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ninawaombea Mungu awape nguvu, afya, maisha marefu na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuikumbusha serikali kuwa, wanajeshi wengi wanalalamika kuwa, haki zao nyingi hawapati, mfano, posho za safari, fedha za likizo, fedha za matibabu na kadhalika. Ninaomba serikali itambue uzito mkubwa wa kazi wanazofanya wanajeshi; hivyo ni vyema walipwe kila wanachostahili kupata, hata mifano tunayo serikali ikitaka.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi majambazi wamekuwa wakionekana na mavazi ya jeshi la Wananchi wa Tanzania. Ninaomba serikali, iimarishe ulinzi wa mavazi ya jeshi letu ili yasiendelee kutumika vibaya, kwani inadhalilisha jeshi letu majambazi kutumia mavazi hayo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema utaratibu mzuri utumike kuchagua wanajeshi wetu, pale inatokea kuwa kuna nchi inahitaji msaada wa kuimarisha ulinzi na amani kuliko ilivyo sasa, wengi hujirudiarudia wengine huwa na manung’uniko, kwani wanaona uteuzi sio mzuri kuna kujuana.

Mheshimiwa Spika, vile vile ninapenda kuishauri serikali kuwa, marupurupu ya wanajeshi hawa wanaokwenda kufanya kazi huko nje ya nchi; ni vyema ijulikane malipo yao ya ziada ni kiasi gani na hushughulikiwa kwa utaratibu gani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenda kufanya kazi kwenye nchi ambazo zinavuruga vijana wetu, huwa wanahatarisha maisha yao sana; hivyo, ninaishauri serikali iwawekee Bima ya Maisha yao, kwani wako ambao hupata ajali huko na serikali huwa inashindwa kuwahudumia hadi kufa kwao.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, askari wa jeshi wanaokaa uraiani, hupatiwa fedha ndogo sana za kulipia kodi ya nyumba wanazoishi huko uraiani. Hii inatokana na kupata kwa viwango vya kodi za nyumba, sambamba na hali halisi ya maisha. Ninaomba Waziri ambaye ni mwanangu, atoe maelezo kwenye majumuisho yake.

Mheshimiwa Spika, vile vile bado kuna kero ya mishahara kuwa midogo sana, haiendi na hali halisi ya maisha, kwani vitu vingi vimepanda bei sana. Ninaiomba sana serikali, mishahara ya wanajeshi itazamwe upya ili iende sambamba na hali ya maisha na kupanda kwa mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri serikali kuwa, utaratibu uliopo sasa wa wanajeshi kupata chakula kazini sio mzuri, kwani chakula chenyewe sio kizuri. Hivyo, bora wanajeshi wapewe fedha wajitegemee, kuliko kula chakula wasichokihitaji. Naomba Waziri anijibu tafadhali.

Mheshimiwa Spika, niipongeze serikali kwa kurudisha utaratibu wa zamani, vijana wanaomaliza Kidato cha Sita kujiunga na mafunzo ya JKT. Pamoja na pongezi hizi, ninaomba kutoa angalizo kwa serikali kuwa ni vyema ikaweka utaratibu wa kuwapa posho kidogo, kwani lazima wanazo kero mbalimbali za kujikimu pindi wakiwa kwenye mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la utata wa kupata pensheni Wanajeshi mara wanapostaafu. Bado kuna utaratibu mbaya, ambao huchelewesha sana malipo ya pensheni kwa wanajeshi waliokufa kabla ya kupata pensheni zao. Naomba serikali ijiwekee utaratibu mzuri zaidi, kwa wastaafu wa jeshi sasa.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa serikali, pamoja na Wizara ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Taifa, kwa ajali iliyotokea ya mabovu kulipuka huko mbagala. Waswahili husema “Kufanya kosa sio kosa bali kurudia kosa.” Ninaomba serikali ichunguze chanzo cha mabomu ili tatizo hili lisijirudie, sio zuri, limeonesha uzembe mkubwa kwa jeshi letu na limeleta athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuomba, wanawake wakumbukwe kwenye kupandishwa vyeo ndani ya Jeshi hili, pamoja na kuwaandalia maisha ya uzeeni askari wote.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Mkuu wa Majeshi, kwa kuandaa bajeti na hotuba hii na kusomwa leo.

Mchango wangu uko katika eneo moja kuu, ambalo ni usalama wa wananchi na mali zao, maeneo mbalimbali hapa nchini kama vile Bukombe, Chato, Geita, Kilondo, Biharamulo, Ngara na kadhalika.

Mheshimwia Spika, Wananchi wetu wanaishi kwa wasiwasi kutokana na tishio la ujambazi, unaofanywa maeneo hayo.

Kazi kubwa ya Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao. Misukosuko ya kivita ni kazi ya JWTZ.

Maeneo niliyoyataja ni sawa na maeneo ya Kivita; kwa nini JWTZ wasiende kulinda maeneo korofi ambayo tunahisi waasi toka nchi jirani ndio wanafanya uharifu huo?

Kwa nini nchi jirani kwa kutambua uharibifu huo wao wameweka Askari wa Jeshi la Wananchi kulinda maeneo yote korofi mfano, Rwanda, Burundi na kadhalika?

Nashauri maeneo yafuatayo wawepo JWTZ walinde au wafanye msako ili kuondoa/kusafisha waharifu wote. Maeneo hayo ni Kelezia – Runzewe; Runzewe – Bwanga; Runzewe – Nyakanazi; Nyakanazi – Kibondo; na Nyakanazi – Rusahunga.

Mheshimiwa Spika, kama tumeona ni vyema kupeleka majeshi yetu kulinda amani Anjwani (Comoro), Darfur na kadhalika, ni jambo jema. Kwa nini maeneo niliyoyataja tusiende kulinda amani? Sio vizuri kusafisha nyumba yetu kwanza kabla ya kusafisha ya jirani?

Mheshimiwa Spika, huu ni muda muafaka wa Serikali kutenga fedha kwa JWTZ za kufanya *operation* katika maeneo niliyoyataja na mengine. Hata hivyo, nimemwandikia barua Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi, kumwomba rasmi, wapeleke JWTZ kulinda eneo la Kelezia (Ushirombo) – Runzewe na Runzewe – Bwanga.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Bukombe wengi wanapoteza maisha yao kwenye maeneo hayo ya msitu. Hii ni kwa sababu, nadhani waasi toka nchi jirani wamejificha humo.
Hata tarehe 27 Juni, 2009, askari wa Jeshi la Polisi ameuawa na majambazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa maeneo yafuatayo: Ataruhusu JWTZ waende kulinda maeneo ya hatari kwa usalama wa Wana-Bukombe ya Kelezia (Ushirimbo) – Runzewe – Bwanga ili Watanzania wasiendelee kuuawa au serikali inaona ni vyema Wana-Bukombe na maeneo mengine tuishi kwa shida?

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii japo kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni moja kati ya Wizara muhimu katika nchi yoyote hapa duniani. Wizara hii ili iweze kutekeleza wajibu

wake wa kulinda wananchi na mipaka ya nchi, ni lazima ipatiwe mahitaji yake yote, pamoja na ukata wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ndugu zetu wanajeshi ili kazi yao ya ulinzi iimarike na ilete ufanisi, ni lazima suala zima la vitendea kazi litiliwe maanani sana. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, atueleze hali ya vitendea kazi jeshini ikoje na anao mpango gani wa kuhakikisha kwamba jeshi linapata vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni, nchi ilipata maafa makubwa baada ya kulipuka mabomu pale Mbagala – Dar es Salaam. Watu zaidi ya 20 walipoteza maisha, majumba mengi yalibomoka na hasara kubwa ilipatikana pale. Tulisikia kwamba, serikali inaandaa taarifa ya tukio lile; je, ni lini serikali itaitoa taarifa hiyo ili iwe bayana kwa Watanzania wote tujue chanzo chake na hatua nyingine ambazo zimechukuliwa kuhusiana na tukio lile?

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua kuwa, kila Wizara inao wastaafu na hata Wafanyakazi waliofariki wakiwa bado ni Wafanyakazi wa Wizara husika. Kwa nini Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inawasumbua wastaafu wake kwa kuwapatia mfao yao? Kwa nini nenda rudi, lete hiki, mara kile, hayaishi ndani ya Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, mstaafu anayeishi Pemba, ambaye hali yake kiuchumi ni duni, kuambiwa kuwa afuatilie mafao yake Dar es Salaam ni usumbufu mkubwa sana. Mtu yule Dar es Salaam hana pa kuishi, hana jamaa, hana pesa za kukaa *guest house*; sasa afanye nini?

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, nilileta malalamiko ya mpiga kura wangu kwa Naibu Waziri, yaani tangu miaka minne nyuma mpaka nikakata tamaa, mara lete hiki mara kile, pamoja na kukamilisha yote niliyotakiwa, hapana mafanikio yoyote yaliyofikiwa. Sasa ni vyema Mheshimiwa Waziri, atueleze hivi utaratibu huu utaendelea hadi lini?

Kwa nini usiwekwe utaratibu kwa wastaafu wanaoishi Pemba kumaliziwa uhakiki na kupatiwa mafao yao kule kule Pemba bila usumbufu wa kutakiwa kuja Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri wa muda mrefu kwa Wizara hii kuboresha hali ya makazi ya askari kwa ujumla wao. Ni vyema Mheshimiwa Waziri atueleze; je, sasa hali ikoje ya makazi kwa askari wa kawaida na maafisa ndani ya jeshi?

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaonesha upotevu mkubwa wa pesa za walipa kodi, ambazo hazikutumiwa kama ilivyotakiwa. Pesa karibu TSh. Bilioni 1.8 hivi, ikajumuisha malipo ambayo hayakulipwa, lakini hakuna marejesho ya pesa hizo kwenda Hazina. Je, Mheshimiwa Waziri atatueleza nini kuhusu upotevu huu wa pesa za wavuja jasho na atachukua juhudi gani ili tatizo hili lisijirudie tena kwa miaka ijayo? Ahsante sana.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi (Mb) - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi - Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanazozifanya hasa katika suala la ulinzi wa nchi yetu.

Katika ukurasa wa 8, aya ya 15 ya Hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, amezungumzia sana suala la kuharibiwa kwa alama za mipaka *(Beacons).* Suala hili si dogo hata kidogo na tusilichukulie mzaha. Linaonekana dogo kwa sababu Tanzania sasa hivi kuna amani na nchi jirani zake; ikitokea vita suala la mipaka halitakuwa dogo. Kama jirani atatokea mtawala dhalimu au mkorofi, tutapata tabu sana. Mfano mzuri ni Kisiwa cha Migingo, kinachogombewa na nchi jirani zetu, naiomba serikali iliangalie suala hili kwa mapana na marefu kwa ajili ya siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa kukosekana kwa alama za mipaka, ndio maana ujenzi holela unaendelea mipakani na ndio chanzo cha uingizaji silaha za moto; uhamiaji haramu na kadhalika. Kutokana na hayo, aliye Mtanzania na asiye Mtanzania, kwa maeneo ya mipakani ni tata na bila vitambulisho vya uraia, hali hiyo itaendelea kuwa tata zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kwa kuimarisha huduma ya tiba na kinga kwa Wanajeshi na familia zao; vijana wa JKT na kadhalika.

Kwa kuwa Wabunge wanatumia hospitali za binafsi kwa ajili ya matibabu yao na familia zao; na pia Hospitali za Serikali; naiomba Serikali ifikirie kuwaruhusu Wabunge kuhudumiwa na Hospitali/Vituo Tiba vya Jeshi, pale ambapo vituo/hospitali hizo zipo. Naomba ombi hili lifikiriwe kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kufufua mafunzo ya JKT kwa vijana wa Kitanzania. Vijana wanaomaliza JKT, wanapomaliza mafunzo watumike katika masuala ya ulinzi kama vile mgambo na kadhalika, kuliko kuwaacha wanarandaranda mitaani. Vijana hao wakiachwa hivyo, wanaweza kujiingiza katika matendo maovu. Kama hakuna ajira ya kuwapatia, wapewe nyenzo za kuwawezesha kujitegemea warudipo uraiani; wazalishe mali na kazi za ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, napongeza kazi nzuri inayofanywa na SUMA JKT; Ujenzi wa nyumba bora, fenicha na kadhalika. Mafanikio ya SUMA JKT, yaonekane pia katika Kambi nyingine, kwa mfano, Kiwanda cha Kutengeneza Dawa cha TANZANSINO.

Mheshimiwa Spika, kama tatizo ni mtaji kwa kiwanda hiki, naiomba serikali ikiwezeshe kiwanda kuwa na mtaji wa kutosha, pamoja na wataalamu, kwani mahitaji ya dawa ndani ya nchi ni makubwa sana na serikali inaweza kupunguza uingizaji dawa kutoka nje kutokana na dawa za TANZANSINO.

Mheshimiwa Spika, mwisho, serikali iangalie uwezekano wa kujenga Makambi ya Jeshi mbali na makazi ya wananchi, kuepukana na matatizo kama ya Mbagala.

Wananchi wanapojenga makazi karibu na Makambi ya Jeshi, serikali isinyamaze na kutokuchukua hatua za kuzuia ujenzi wa makazi. Makambi ya Jeshi yana mambo ya siri ya kivita, ambayo siyo vizuri yakajengwa karibu na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuitumikia vizuri na kwa ujasiri mkubwa, Wizara hii nyeti. Mwenyezi Mungu, amuwezeshe zaidi yeye na Naibu wake, pamoja na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza zaidi kwenye vyuo vya mafunzo ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Monduli ni Chuo ambacho kinatoa mafunzo kwa Watanzania na pia kutoka nje ya Tanzania, lakini Watanzania wana malalamiko mengi kwamba, ukienda mafunzo Phase I, Phase2 na kwa bahati mbaya ukafeli katika Phase 3 kwamba, huwezi kupandishwa cheo na badala yake, lazima urudi tena chuoni ukasome tena Phases zote tatu, badala ya kurudia ile moja tu ambayo hukufanya vizuri. Hii kwanza ni kuwapotezea muda, lakini pia tunawavunja moyo na hii inafanyika kwa Watanzania tu na kwa wanachuo wote. Je, huu sio ubaguzi unaoonesha kuwapa hadhi na heshima wageni kuliko Watanzania wenyewe?

Lalamiko la pili ni kwamba, kunapotolewa vifaa vyuoni, basi wanachuo wa kigeni ndio wanaopewa vifaa vizuri ama vipya; kulikoni mbona Watanzania wanadharauliwa wakati sadaka huanza nyumbani?

Mheshimiwa Waziri, kama madai haya ni ya kweli, naomba yashughulikiwe na yarekebishwe haraka sana na kama hayajaonekana, naomba yafanyiwe uchunguzi wa kina ili kama yapo basi yakomeshwe. Naomba askari wetu hawa, wapandishwe vyeo kwa mujibu wa uwezo walionao.

Mheshimiwa Spika, pia naomba sana viongozi wa jeshi letu, wasikubali kutumiwa vibaya kule, kupelekewa vijana wanaojiunga na jeshi kwa jina kwamba, ni Wazanzibari am Wapemba, kumbe ni vijana kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa na RPC, wanatumia sana nafasi zao vibaya, kwa kuwanyima fursa na haki zao wengine ambao hawana mahusiano na walio madarakani.

La mwisho, naomba tuwaangalie kwa ukaribu sana, wastaafu wa jeshi pamoja na wahanga/waathirika wa vita, ambao ni walemavu. Tukiwatunza hawa, tutakuwa tumelijengea heshima kubwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ya Wizara yake.

Naipongeza serikali kwa kufungua JKT. Ufufuaji huo, ungezingatia pamoja na maeneo mengine, Wilaya za mpakani kama Ngorongoro na Longido. Wilaya hizi zina eneo refu na nchi jirani ya Kenya katika Wilaya za Narok na Kajiado pia zipo njia nyingi za panya, zinazotumiwa na waharifu wa Kisomali; wezi wa mifugo, wauzaji wa dawa za kulevya, wapelelezi wa masuala ya usalama, wawindaji haramu wa wanyamapori, majangiri na kadhalika. Kwa kuanzisha JKT mipakani (kama Tarime), nchi jirani wataogopa kama ilivyokuwa Uganda wakati wa Vita vya Amini.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yoyote, haiwezi kuimarika bila ya kuwa na ulinzi mzuri na walinzi wenyewe kujituma; kwanza, cha kusikitisha ni tatizo kubwa la sehemu ya kuishi inayowakabili wanajeshi wetu. Wengi wa wanajeshi wanaishi uraiani, kiasi cha kuchangia katika kupokea kwa maadili yao.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi kama walinzi wa nchi yetu, walipaswa kuishi katika Kambi, kwa vile kule wana mambo yao, ambayo raia wa kawaida hapaswi kuyafahamu. Wanajeshi wanaishi uraiani, wakiwa na vifaa mbalimbali vya jeshi; matokeo yake kuna baadhi ya wezi au majambazi, wanaungana na wanajeshi hawa, kiasi cha majambazi/wezi hao kupata mavazi ya kijeshi *(Combat)* na wengine hata silaha ambazo wanazitumia katika kufanya ujambazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, alieleze Bunge hili ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wale Wanajeshi wa Kambi ya Pande Wilaya ya Tanga, ambao walipigana na kuwajeruhi hadi kulazwa hospitali. Kitendo cha wanajeshi kuchukua sheria mikononi mwao, kimekithiri sana au hayo ndiyo baadhi ya mafunzo wanayopata wakiwa chuoni kuwa wawe tu wanawaadhibu raia bila ya kuwafikisha katika vyombo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile serikali inatarajia kuanzisha/kurudisha JKT, hili nalipongeza sana kwa kuwa hii itasaidia kujenga ukakamavu kwa wale wote ambao watajiunga na jeshi hili kama ilivyokuwa hapo awali, wale wote waliopitia JKT walikuwa wakakamavu na nchi ilijivunia jeshi letu hili.

Mwisho, namalizia kwa kusema kuwa, serikali iwaangalie sana wanajeshi wetu, kwa kujitahidi kuwajengea makambi yao maalumu ili kuepuka kuongezeka kwa uhalifu uraiani na pia kuwasaidia katika kupambana na ugumu wa maisha, kwa vile pesa wanazopewa kama posho ya nyumba *(House Allowance)*, haitoshelezi kutokana na upandaji wa kodi kwa wenye nyumba mara kwa mara.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi (Mb), kwa Hotuba nzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu linastahili sifa kwa kazi nzuri lililowahi kuifanya katika Ukombozi wa Afrika. Nawapongeza sana, kwa moyo wao wa kujitoa muhanga. Pamoja na historia hiyo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, linaheshimika sana kwa

umakini wake, kwa nidhamu yake na kwa uwezo wake. Naomba wazidi kuongezewa nguvu.

Mheshimiwa Spika, jeshi letu limeshiriki katika nyanja mbalimbali *(various fronts)*, kama vile majanga na maafa. Jeshi letu limetumika wakati wa El-Nino, wakati wa uokozi MV Bukoba ilipozama, 1996; ajali ya Treni Dodoma; na ajali ya Meli Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nikianza kutaja ushiriki wa jeshi letu *Locally and Internationally*, muda hautatosha. Itoshe kutambua kazi nzuri wanayofanya chini ya Amiri Jeshi Mkuu, CDF na Makamanda wote wahusika.

Jeshi letu limehakikisha usalama wa nchi dhidi ya uvamizi kutoka nje ya nchi, mipaka ni salama kabisa.

Mheshimiwa Spika, ndani ya nchi yetu, kuna tishio kubwa la amani ya wananchi/raia kwa ujumla, kutokana na ujambazi. Leo hii hatuna uhuru wa kusafiri usiku maeneo mengi, kwa sababu ya ujambazi (utekaji nyara). Tumekuwa kama vile tunajiridhisha kwamba, kwa sababu ya ongezeko la watu, basi ni halali kuwa na uhalifu mwingi zaidi na kwamba, tuna Polisi wachache.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1983, hali ya ujambazi na uhalifu ilizidi, kiasi kwamba iliwashinda polisi. Leo hii nina hakika, polisi waliopo hawawezi kudhibiti hali ya uhalifu na kuweza kurejesha utulivu. Naishawishi serikali iwatumie *(outsource)*, Wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi, kuleta haki ya amani na nidhamu kwa kila raia kama ilivyofanyika ilipotumika JKT mwaka 1983.

Mheshimiwa Spika, naomba suala la amani ya raia, pamoja na kuwa liko chini ya Polisi, tusione aibu kuazima nguvu ya Jeshi ili kupata amani iliyo kamili, tubaki na kazi ya kujenga uchumi. Naomba Waziri anapojibu hoja za Wabunge, atolee maelezo hili.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuiomba serikali, ihakikishe inaboresha maslahi ya majeshi yetu ya ulinzi. Ufanisi wa jeshi, pamoja na nidhamu yake, lazima uambatane na maslahi stahiki ya jeshi na wanajeshi na yanafahamika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu wake, pamoja na Viongozi wote wa Wizara hii.

Kwa namna ya pekee, niwashukuru kwa ajira ambazo zimetolewa kwa ajili ya vijana hususan kutoka mkoani kwangu.

Mara ya mwisho niliuliza swali juu ya umuhimu wa kurudisha vijana JKT, mkaahidi kuwa mpo mbioni katika mchakato huo na kweli mmekamilisha zoezi hilo.

Mheshimwia Spika, naomba nisisitize tu umuhimu wa kuwa na maandalizi mazuri katika Makambi hayo. Nakumbuka nilipokuwa Mlale JKT, hali ya mabafu na vyoo, ilikuwa ni mbaya sana; hivyo ni vyema vyoo hivyo au mabafu vifanyiwe marekebisho.

Jeshi isiwe ni sehemu ya kuwakandamiza au kuwaumiza vijana, bali iwe na sura ya kisasa kwa maana kwamba, sio tu lazima iwe ni kwa ajili ya kilimo, bali tuangalie fursa zote. Mfano, hivi karibuni kumeibuka teknolojia nyingi ikiwemo ICT, mafunzo ya *entrepreneurship* na kadhalika. Hivyo basi; ni vyema kuhakikisha kuwa JKT ya sasa inakuwa na tija zaidi kulingana na maisha ya sasa.

Maofisa watakaohusika kuwakuza vijana hao, lazima wawe na nidhamu, kwani sasa hivi kuna suala la UKIMWI ambalo ni tatizo.

Poleni sana kwa maafa yaliyotokea Mbagala. Ni vyema pia hatua za ku-*check* maghala yetu zifanyike mara kwa mara, kwani yawezekana itasaidia kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na ushirikiano wake na uongozi wa kijeshi katika Wizara yake.

Ninawapongeza wananchi wote kwa ujumla, licha ya kuwepo Wanajeshi wachache wasiokuwa na sifa hii ya kuonesha ushirikiano na uelewano mzuri na wananchi raia. Hili ni jambo jema, pasipokuwa na maelewano mazuri kati ya makundi haya, pamoja na kuwa kikundi kimoja kinaumia zaidi, lakini huwa hayupo aliye na amani rohoni kwa asilimia mia moja. Amani ni faraja kwa awaye yoyote katika makundi hayo mawili.

Nawapongeza wanajeshi wote, kwa kudumisha amani ya nchi yetu. Ninawapongeza sana kwa uhodari wanaouonesha, kila waendapo nje ya nchi kikazi. Ni sifa kwao na kwa nchi yetu. Hii nayo inachangia katika kudumisha amani kati yetu na majirani zetu. Bila heshima hiyo, siyo ajabu kuonewa mipakani. Utaratibu na ustaarabu waviendeleze.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza serikali, kwa kukubali kurejesha JKT. Ni jambo jema sana, kwa matumaini yangu na wananchi wengi, JKT italeta na kuimarisha utaifa wetu, uvumilivu kwa upande wa vijana wetu na upendo kati ya vijana wa sehemu mbalimbali katika nchi yetu. Ninayo maombi yafuatayo:-

Maadili yaimarishwe, unyanyasaji wa kijinsia usiruhusiwe. JKT mwanzoni ilianza kuharibu sifa zake kutokana na unyanyasaji wa kijinsia. Hatua kali sana, zichukuliwe kwa watakaojitokeza kunyanyasa wasichana.

Kwa kuwa ndiyo tunarejesha jeshi, ninashauri maandalizi yakamilike kabisa, kabla kikundi cha kwanza cha vijana hakijaenda kuripoti. Vijana hawa wakikuta maisha na utaratibu umeandaliwa vyema, watawavuta na wengine watakaofuata, watakuja kwa roho nyeupe; si vyema tukaanza na picha mbaya/chafu. Ni vyema wakaelewa kuwa, hapo ni mahali pa mafunzo ya kijeshi; si mahali pa burudani au pa mateso, mithili ya mateso kwa waadhibiwa.

Vijana wanaomaliza mafunzo ya JKT kwa kujitolea, waandaliwe taratibu nzuri za ajira; si vyema sana jeshi likakaa na vijana hawa kwa miaka miwili au zaidi, kana kwamba hawana faida yoyote, hata baada ya kuwa JKT kwa kipindi kirefu. Mafunzo ya JKT yaandaliwe vizuri kuweza kuingia katika soko la ajira kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Wapo wanajeshi walioshiriki Vita vya Uganda na Msumbiji, ambao bado wanadai mafao na hawajui lini na kwa namna gani watapata mafao yao hayo. Serikali ni vyema ikawa na uhakika na uwezo wa wananchi wazalendo na walifanya kazi nzuri ya kizalendo, yenye kuiletea sifa na heshima nchi yetu. Walipwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba vigezo vya kujiunga na JKT viwe sawa na vya kujiunga na JWTZ. Majeshi haya ni mtu na mdogo wake, mwisho wa siku kazi zao zinafanana sana. Kipo kigezo cha nafasi ndani ya nyayo za miguuni. Kujiunga na JKT hiyo siyo sifa; kujiunga na JWTZ ndio sifa. Watu wengi wanashindwa kuelewa; je, inakuwaje kijana aliyefanikiwa kujiunga na JKT akatumikia jeshi hili bila wasiwasi kwa miaka kadhaa halafu kijana huyo akazuiwa kujiunga na JWTZ kwa kuwa nyayo zake za miguuni hazina nafasi? Ninashauri, kama ni sifa muhimu basi iwe kwa majeshi yote; JKT na JWTZ. Aidha, ninaomba kufahamishwa watakaokuwa wanajiunga kwa mujibu wa sheria; je, sifa hiyo itahitajika?

Mheshimiwa Spika, hotuba ni nzuri, mipango ni mizuri, kama pesa/fedha haitoshi, JKT isianzishwe isubiri.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR**: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, pamoja na Viongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuongoza vizuri. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi mbali na kulinda nchi na mipaka yake, bali pia linashiriki kutoa misaada katika maafa na majanga mbalimbali, kama vile ya moto, kuporomoka kwa majengo, na kadhalika. Hivyo, wanapaswa kuangaliwa vizuri kimaslahi, kimakazi na kupatiwa vitendea kazi vilivyo bora.

Mheshimiwa Spika, Jeshi kulingana na kazi zao, wanapaswa kupata mlo ulio bora kila siku. Elfu tano za saa za chakula ni kidogo mno, kiasi kwamba, hazitoshelezi mahitaji yao. Hivyo; ni vyema wapewe kati ya shilingi elfu nane hadi elfu kumi kwa siku kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kima cha wastaafu wa jeshi ni vyema kiangaliwe upya, badala ya hali ilivyo sasa. Pia wapatiwe mafao yao mapema iwezekanavyo ili isiwe ni sababu ya kufanya wajiingize katika matendo ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi limetolewa katika shughuli za kisiasa, lakini kwa bahati mbaya, kuna wakati limetumiwa kuwa-*harass* wananchi wakati wa uchaguzi, hasa kule Zanzibar na zaidi kwa Wafuasi wa Chama cha CUF. Hali hii inawakosesha baadhi ya wananchi, kutumia haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Mheshimiwa Spika, nafasi za ajira katika Jeshi la Ulinzi, zitolewe kwa wananchi (vijana) wa Bara na Visiwani (Zanzibar) na wasitoke Wananchi wa Tanzania Bara kuja kuchukua nafasi za Zanzibar. Hali hii imewanyima nafasi vijana kutoka Zanzibar, kuingia katika Jeshi letu la Ulinzi, jambo ambalo halileti sura nzuri katika Jamhuri yetu ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jeshi la Ulinzi linaonesha nidhamu kubwa katika utendaji wa kazi zao, lakini makazi yao hayaridhishi. Kwa kuwafanya waendelee kuishi kwa nidhamu, wanapaswa wapatiwe makazi bora ili nidhamu yao isiishie kazini tu, bali hata wanapokuwa katika makazi yao, pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi, lipatiwe vitendea kazi vilivyo bora, ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri ili yakitokea majanga au maafa yoyote, waweze kufika maeneo ya matukio kwa haraka sana. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, natumaini mmekuwa na mapumziko mazuri ya mchana au mikutano. Sasa tunaendelea. Orodha yangu ya wachangiaji imekwishakamilika na nirejee tu niliyokwisha kuwatangazia kwamba, sasa kwa mpangilio kuanzia Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, watatoa majumuisho, kujaribu kutoa mwanga kwa yale ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeulizia.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ataanza kwa dakika 20 na hatimaye mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwa dakika 25. Sasa namwita Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kuchangia hoja yake, aliyoiwasilisha leo asubuhi, kwa kuanza na kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi kwanza, kukushukuru kwa dhati wewe mwenyewe binafsi, Naibu wako na Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vile vile, kumshukuru kwa dhati Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi kubwa anayofanya ya kuongoza Wizara yetu. Vile vile kwa uwezo wake wa hali ya juu na uchapa kazi, ambao unatufanya sisi wasaidizi wake, kufanya kazi kwa kufuata mfano wake, ambao ni bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kuishukuru kwa dhati, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa jinsi inavyoongoza vizuri shughuli za Wizara yetu. Nitumie nafasi hii vile vile, kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Watumishi wote wa Wizara hii, wakiwemo wanajeshi na raia, pamoja na JKT na Jeshi la Wananchi, kwa kutoa ushirikiano mkubwa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nimshukuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Generali Mwamunyange, kwa kazi kubwa anayofanya na kwa ushirikiano mkubwa sana anaofanya kwa Viongozi wa Kiraia. Namshukuru yeye binafsi, *Chief of Staff*, Maafisa wote wa Jeshi na Askari, kwa kazi hiyo nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vile vile, kumshukuru sana mke wangu Jane na watoto wangu, ndugu, jamaa na marafiki zangu, kwa ushirikiano wanaonipa katika majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, nitumie nafasi hii, kuwashukuru sana Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Kambi zote, kwa ushirikiano ambao wameipa Wizara hii, kwa mwaka huu mzima wa fedha unaomalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa. Nianze kujibu baadhi ya hoja za Kambi ya Upinzani. Hoja mojawapo iliyotoka Kambi ya Upinzani, iliitaka Wizara kuanzia sasa, kuona uwezekano wa kuanza kutoa vyeo moja kwa moja, kwa askari wote wanaofuzu mafunzo ya kupata vyeo kule kule mafunzoni kabla hawajarudi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, mafunzo wanayopata askari wetu si kigezo pekee cha kupata cheo, ni sehemu tu ya vigezo vya kupata vyeo. Kwa hiyo, wakimaliza mafunzo, wanaangaliwa sasa kama wanakidhi

vigezo vile vingine ndipo wanapata cheo. Utaratibu huu haupishani sana na utaratibu wa nafasi nyingine za Bunge lako, kwa mfano ili uwe Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lazima ufike umri wa miaka 21. Sasa kila raia mwenye miaka 21, akijitangaza kwamba kawa Mbunge, itakuwa tabu kidogo, lakini ni sehemu ya vigezo, sio sifa kamili ya kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili iliyotolewa na Kambi ya Upinzani ni kuhusu maduka ya Jeshi, pamoja na kupunguziwa kodi kuwa na bei za juu. Naomba nikubaliane na Kambi ya Upinzani kwamba, habari hii ni ya kweli. Halmashauri ya Majeshi ya Ulinzi, imeshakutana na ikalitambua tatizo hilo na imeshatoa maelekezo ya mikataba kuangaliwa upya, lakini vile vile kusimamia kwa karibu, kuhakikisha tatizo hili linaondolewa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani vile vile, ilitoa hoja ya kuona uwezekano wa Kampuni yetu ya Nyumbu kuimarishwa ili iweze kutengeneza magari ya kisasa, lakini yanayokidhi mazingira ya nchi yetu. Naomba kusema, ushauri huu ni mzuri. Kwa sasa Nyumbu inafanya uchunguzi wa magari 26 katika sehemu mbalimbali nchini, kwenye makambi yake, kuona kama yanafaa. Pia tumechukua uamuzi wa kuwa *assembly line,* kwa maana kwamba, tuanze kujenga uzoefu wa kuunganisha kabla hatujawa na uwezo kamili wa kutengeneza vitu sisi wenyewe. Kwa hiyo, ushauri wa Upinzani ni mzuri na tunaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vile vile, kuongelea ushauri wa Kambi ya Upinzani kuhusu Mtandao wa Kipekee wa Mawasilino (ITN). Naomba niseme kwamba, wazo lao pia ni zuri. Mtandao huu uliundwa maalum, kumsaidia Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kuweza kufanya mawasiliano na Vikosi vyote nchini, kwa uhakika na kwa usalama. Nalithibitishia Bunge lako kwamba; ni kweli mtambo huu una nguvu za ziada na hivyo unaweza kutumika kwa matumizi mengine ya kiserikali. Kwa kutambua hivyo, Serikali imetoa ruhusa mtambo huu utumike kwa mawasiliano ya kiserikali, yanayoitwa *E-Government* na utaratibu huu unasimamiwa na Wizara ya Utumishi na unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nijibu hoja ya Upinzani inayohusiana na Watumishi wa Umma, kuondolewa katika salary slip mwaka 2004. Kwanza, habari yenyewe ni kweli kwamba, waliondolewa. Naomba nilithibitishie Bunge lako kwamba, Wizara ya Fedha, inalifanyia kazi jambo hili, kuhakikisha wanaopata usumbufu huo hawapati tena.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vile vile, kujibu hoja iliyotolewa na Kambi ya Upinzani, ambayo inaongelea askari walioathirika na tatizo la umri, ambalo limerekebishwa kutokana na sheria ya pensheni ya askari wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kwamba, kutokana na usikivu wa Serikali, baada ya kutambua kwamba tatizo hili lipo, Wizara ya Ulinzi kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi, tulikaa tukakubaliana kwamba, tatizo hili linatakiwa litatuliwe; tukapitisha kwenye Halmashauri ya Majeshi ya Ulinzi, uamuzi ukafanywa wa kutatua tatizo hilo na

baada ya kufanya uamuzi huo, taarifa hiyo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais, ambaye faili hilo halikukaa kwake hata mwezi mmoja, akawa amesaini kuonesha ambavyo naye alilipa uzito. Kwa hiyo, Maafisa ambao walikuwa wameathirika, wanaotakiwa kulipwa kutokana na jambo hili ni Maafisa 91, askari 140; jumla yao ni 231. Tatizo lao kama nilivyoeleza, kwa kuwa sisi ndio tulioliona; ni wazi tuna dhamira ya kulimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vile vile, kujibu hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, ambao kwa pamoja walitaka eneo la Jeshi la Kisakasaka lipimwe pamoja na kupima maeneo mengine ya Jeshi nchi nzima. Naomba nikubaliane nao kwamba; ni kweli tuna maeneo mengi sana ya Jeshi letu, ambayo hayajapimwa na uamuzi wa kuyapima umekwishafanyika. Kinachofanyika sasa ni kufanya upimaji huo, kulingana na fedha inavyopatikana, lakini ni moja ya mambo ya vipaumbele vikubwa katika Jeshi letu na katika Wizara ya Ulinzi. Naomba niwahakikishie kwamba, jambo hili tunalifanya kwa dhamira ya dhati na tutalimaliza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujibu hoja ya Mheshimiwa Ali Ameir na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, naomba sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa Mariam Faki, ambaye aliongelea umuhimu wa Serikali kuongeza idadi ya vijana wanaosoma VETA, umuhimu wa kuimarisha uzalendo katika JKT na kuhakikisha mafunzo ya uzalendo yanasisitizwa zaidi, vile vile umuhimu wa kuongeza fungu la Mgambo ambalo kwa sasa lipo lakini dogo. Naomba niseme, Serikali inakubaliana na ushauri huu mzuri na tutaufanyia kazi kadiri bajeti ya nchi yetu itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Jeshi ya Kanda ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kaboyonga kwamba, ujenzi huu umepangwa kuanza katika mwaka huu wa fedha, kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ujerumani. Kwa hiyo, Wizara yetu kwa upande wake, itatimiza wajibu wake kikamilifu, kuona kwamba sisi hatuwi wakwamishaji wa zoezi hili ili likamilike kwa haraka na wananchi na askari walio katika maeneo yale, waanze kupata huduma hiyo haraka itakavyowezekana, mara hospitali hiyo itakapokamilika kujengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Anthony Diallo, ambaye alikuwa na matatizo makubwa mawili: Tatizo lake la kwanza, alisema askari waliwafanyia fujo raia walioko katika Jimbo lake na kuwahamisha katika eneo.

Mheshimiwa Spika, tumelifanyia uchunguzi wa kutosha jambo hili na majibu yake ni kama ifuatavyo: Askari wa Jeshi letu walioko Mwanza, waligundua ongezeko la wananchi kujenga katika eneo la Jeshi, ambapo ongezeko hilo la ujenzi katia eneo hilo, umekuwepo kwa muda mrefu. Kwa kuzingatia umuhimu wa wananchi nao kupata makazi, hawakuchukua hatua kwa wakati unaostahili. Siku za karibuni yalitokea maendeleo mapya, ambapo wananchi walianza kujenga maeneo ambayo yako karibu na maghala, ambayo yanahifadhi mabomu. Ujenzi huo ukiwa katika hatua za awali kabisa,

Jeshi letu lilichukua hatua ya kuzuia usiendelee. Kwa hiyo, kwa maana ya Jeshi letu, Jeshi letu lilichukua hatua ya kuokoa raia wasipate madhara yanayoweza kutokea siku za usoni.

Kwa hiyo, nilidhani ilikuwa ni wakati muafaka wa kulipongeza Jeshi letu, kwa kuchukua hatua hiyo ya haraka ya kuokoa raia hao na madhara ambayo yangeweza kupatikana, maana wajibu mkubwa wa Jeshi letu sio kuokoa watu walioumia tu, lakini ni kuhakikisha watu wetu hawapati madhara. Kwa hiyo, wajibu wao walitimiza kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nijibu hoja ya Mheshimiwa Anthony Diallo, kuhusu uwezekano wa Hospitali ya Jeshi pale Mwanza kuwa Hospitali Teule ya Wilaya. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Diallo, kwa kulifuatilia sana jambo hili. Naomba nimhakikishie kwamba, kutokana na ufuatiliaji wake, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limekubali kwamba, Hospitali hiyo inaweza kutumika kama Hospitali ya Wilaya. Vile vile Waziri wa Ulinzi, amekubali kwamba, inaweza kutumika kama Hospitali ya Wilaya. Kwa maana hiyo basi, tunwaomba Madiwani wa Jimbo la Ilemela, watimize wajibu wao wa kukaa na kupitisha Azimio la kuomba Jambo hili. Wafuate taratibu zinazohusika na kuhakikisha mchakato huo unakwenda na wawe na hakika kwamba, maombi yao yatakapofika kwenye meza ya Mkuu wa Majeshi na Waziri wa Ulinzi, yatapitishwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijibu hoja ya Mheshimiwa Tatu Ntimizi, ambaye aliongelea tatizo la askari wetu kujichukulia sheria mkononi. Kwanza, naomba niseme kwamba, askari wanaojihusisha na tabia ya kuchukua sheria mkononi ni wachache sana katika Jeshi letu. Wanajeshi wetu walio wengi, wana nidhamu ya hali ya juu na wamethibitisha hivyo kwa vitendo. Naomba niwahakikishie kwamba, Wizara pamoja na Makao Makuu ya Jeshi na Viongozi wote wa Jeshi, wanakerwa sana na tabia ya askari wachache wanaochukua sheria mikononi. Mara zote, Jeshi la Wananchi limekuwa likichukua hatua kali dhidi ya askari wote, ambao wanafanya vitendo vya utovu wa nidhamu na kujichukulia sheria mkononi.

Kwa bahati mbaya tu kwamba, hatua za kijeshi zinazochukuliwa na Jeshi la Wananchi huwa hazitolewi kwa matumizi ya Umma. Kwa hiyo, hawawatangazii wananchi kila inapotokea kwamba, askari kadhaa wamefukuzwa kazi, wangapi wamefanywa hivi na kadhalika. Nataka niwahakikishie kwamba, askari wengi wenye tabia hii wamefukuzwa kazi na wengine kuchukuliwa hatua nyingine za kinidhamu ili tabia hii ikomeshwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumechukua utaratibu mpya wa kuajiri Askari wa Jeshi la Wananchi, kwa kuanza kuchukua sasa vijana wanaopitia JKT na JKU. Nia hasa ya uamuzi huu, kwanza ni kuhakikisha kwamba, vijana hawa wameangaliwa tabia zao kwa makini kule kabla hawajachukuliwa. Kwa hiyo ni vijana tu wale ambao wako katika kiwango cha juu kabisa cha nidhamu na ubora, ndio wanaochukuliwa. Pili; inasaidia kupunguza malalamiko kwenye baadhi ya maeneo ya Jamhuri yetu, ambayo nayo yanakwenda vizuri toka uamuzi huu umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili vile vile, Jeshi letu limejenga ushirikiano wa karibu sana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama. Tunashirikiana kwa karibu sana na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama. Nataka niwahakikishie kwamba, tutaendelea kushirikiana navyo. Jeshi letu, Mkuu wa Majeshi na Mkuu wa Jeshi la Polisi, wanafanya kazi kwa karibu sana na ndio maana mambo ya nchi yetu mengi yanayohusu ulinzi na usalama, yanakwenda vizuri. Tunaomba Viongozi wetu hawa wa Majeshi, waendelee kufanya kazi kwa karibu na kwa ushirikiano wa hali ya juu na askari wote waige mfano mzuri unaofanywa na viongozi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vile vile, kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, ambaye alikuwa ameomba askari wa kule kwenye Jimbo, lake wapatiwe basi. Kwa sasa kwenye eneo lile, wanalo basi moja aina ya TATA, ambalo linaweza kuchukua abiria 65. Naomba nitumie nafasi hii, kumpongeza sana sana Mheshimiwa Ruth Msafiri, ambaye mara zote, mwaka huu peke yake amesimama karibu mara tatu, kutetea maslahi ya askari katika eneo lake na maeneo mengine ya nchi yetu. Tunaomba tumhakikishie, hali itakaporuhusu, tunaweza tukalifanya jambo hili kwa kuwaongezea zaidi usafiri askari wetu walioko kwenye eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nijibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, ambaye kwa uchungu na mara nyingi ameeleza sana kuhusu kukithiri kwa majambazi katika eneo lake. Ameomba Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, litumike katika kuhakikisha kwamba, hali ile inawekwa vizuri. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Luhahula kwamba, kwa kuwa vyombo hivi vya ulinzi na usalama, vinafanya kazi pamoja; pamoja na kwamba tunatambua kwamba kazi ya msako wa majambazi ni kazi ya Jeshi la Polisi, mara Jeshi la Polisi litakapotoa nia ya kushirikiana na Jeshi letu kwenye eneo hilo, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, liko tayari wakati wowote, kutoa ushirikiano wa hali ya juu kuhakikisha kwamba, majambazi hao wanadhibitiwa.

Vile vile kwa mujibu wa taratibu, Mkuu wa Mkoa anaweza kumwandikia Waziri wa Ulinzi, kumweleza umuhimu wa kuingilia kati kama jambo ni la dharura sana na anaamini kwa dhati kwamba, Jeshi la Wananchi ndilo linaloweza kuokoa jambo hilo. Mheshimiwa Luhahula, awe na hakika kwamba, Serikali inatambua matatizo yaliyoko kule na ipo tayari kushirikiana na wananchi wa kule, kuona kwamba nao wanaishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maswali yaliyoulizwa ni mengi sana; na kwa vyovyote vile hatutaweza kuyajibu yote; nitumie nafasi kuwashukuru wote ambao wameuliza maswali na mengine ataendelea kuyajibu Mheshimiwa Waziri. Kwa kumalizia, niwashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja kwa mara nyingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Huu ni mfano mzuri wa namna ya kujibu maswali, kwa sababu ukiulizwa jina lako nani, unataja jina, sio kutaja hali ya hewa na mambo mengine. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Nchimbi, kwa mfano mzuri sana huo.

Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Namhakikishia tu, muda atakaotumia kutamka majina ya Waheshimiwa Wabunge, hautahesabiwa katika dakika zake zile 25. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu. Kama ilivyo kawaida, nitaanza na kuwatambua waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza idadi yao ni kumi kama ifuatavyo: Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Saleh Ali Farah, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi - Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi idadi yao ni 51 kama ifuatavyo: Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshikiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mwadini Abbass Jecha, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki na Mheshimiwa Damas Nakei.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Nuru Bafadhali, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda, Mheshimiwa Margreth Sitta, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis na Mheshimiwa Elietta Switi, ambaye alikuwa wa mwisho katika kuchangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutushauri ipasavyo chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Masilingi. Aidha, napenda niwapongeze na kuwashukuru Kambi ya Upinzani vile vile kwa hotuba yao nzuri, ambayo itachangia katika utekelezaji wa bajeti yetu. Napenda niwapongeze Wabunge wote, ambao kwa kiwango kikubwa, wametoa pongezi nyingi kwa Jeshi letu na wamechangia na nina hakika michango yao itaweza kutusaidia katika utekelezaji wa bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana na upendo waliouonesha Waheshimiwa Wabunge, karibu wote waliochangia pamoja nawe Mheshimiwa Spika, kwa Jeshi letu la Ulinzi na JKT. Michango mingi imesikika ikitetea maslahi ya wanajeshi na kwa hiyo, nataka niwahakikishieni tu na sisi kama Wizara, tuko pamoja kuhakikisha kwamba, maslahi hayo yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ninasoma bajeti yangu asubuhi, sikupata muda wa kuwashukuru wote, lakini napenda tu niwashukuru Naibu Waziri wangu, kwa kunisaidia kwa kazi hii tunayoifanya, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ulinzi. Aidha, napenda nimshukuru Mkuu wa Majeshi, Mnadhimu Mkuu, Makamanda na Wapiganaji wote, kwa mchango mzuri wanaotoa na kwa ushirikiano wanaotupa pale Wizara ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si rahisi kuzijibu hoja zote zilizotolewa kwa muda tuliokuwa nao, kwa hiyo, nitajaribu kujibu baadhi tu ya hoja zilizotolewa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutaziandika, tutazitoa kwa maandishi na kuwafikishia hoja zao kila Mbunge aliyechangia.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na eneo ambalo limechangiwa na wengi; suala zima la maslahi kwa Wanajeshi wetu. Serikali imekuwa ikiongeza mishahara kwa Wafanyakazi wake wote wa Umma, pamoja na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na kila mara panapokuwa na ongezeko, basi na mishahara ya Wanajeshi vile vile huwa inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, tumeweza kufanikiwa kuongeza *ration allowance* kutoka 2500/= hadi kufikia 5000/=. Wabunge wengi waliochangia, wamesema kwamba, bado fedha hizo ni kidogo na sisi tunakiri hilo. Serikali imeweza kutufikisha hapo na imeonesha nia ya kuweza kuziongeza hizi mwaka hadi mwaka, pindi bajeti ikiruhusu ili tufike pale ambapo ingekuwa kiwango cha kutosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, vile vile mwaka huu wa fedha, Serikali imeweza kuongeza *allowance* inayotolewa kwa ajili ya makazi, kwa ajili ya nyumba za Wanajeshi. *Allowance* hii ambayo inaitwa *Ngome Allowance*, ilikuwa ikitolewa kwa vima vya mishahara ya mwaka 1994; kwa maana hiyo, watu walikuwa wanapata kiwango kidogo sana, lakini hatimaye Serikali imekubali kubadilisha, wataanza kupata *Ngome Allowance* hii kwa vima vya mishahara vya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni nalo limejadiliwa sana. Tuseme tu kwamba, kwa sasa Serikali imeweza kuongeza kutoka fedha zilizokuwa zikitolewa mpaka kima cha chini cha pensheni sasa kufikishwa 50,000/=. Ni kweli kima bado ni kidogo kama wengi walivyosema, lakini Serikali itakuwa ikiongeza kila mara na hii si kwa Wanajeshi tu, ni wastaafu wote wa Utumishi wa Umma ili hatimaye tuweze kuhakikisha kwamba, kima kinachopatikana kinatosheleza mahitaji. Ni kweli kwamba, bado ni kidogo na mifano mingi iliyotolewa hapa kwamba, pengine ingekuwa busara zaidi kiendane na kima cha chini cha mshahara. Suala hilo linapokelewa na endapo uwezo utaruhusu, basi jambo hio litaweza kufanikishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi mengine ya wastaafu, niseme kwamba, wastaafu wa Jeshi wako wengi na wamekuwa wakipata maslahi yafuatayo: Kwanza, kuna pensheni ya kawaida ambayo wanaipata. Kulikuwa kuna michango mingi, iliyokuwa inawazungumzia wale walioumia katika Vita vya Kagera, hao pamoja na pensheni yao ya kawaida, wanapata *disability allowance*, vile vile kwa kiwango cha ulemavu walichopata. Aidha, wale waliopoteza maisha wakati wanalitumikia Jeshi, wanapata *death gratuity* na familia zao wanapata ile inayoitwa *survivors benefits*, kwa maana ya mjane na watoto. Watoto huwa wanahudumiwa mpaka wanapofika miaka 18 na mjane anahudumiwa kwa kipindi chote cha maisha yake au kama ataolewa, basi hapo ndipo inaposimamishwa *benefit* hiyo. Kwa hiyo, suala hili pengine nieleze tu kwamba, pensheni hizi zimekuwa zikitolewa, tatizo kubwa zaidi ni kima chenyewe kwamba, ni kidogo mno, kiasi cha kwamba yale manufaa yanakuwa hayapatikani inavyotakiwa.

Tunalitazama suala hili na tutaendelea kushauriana ili hatimaye tuweze kuongeza vima hivi ili hawa wajane, pamoja na watoto wa wale wanaofariki katika Utumishi wa Jeshi, waweze kuendelea kupata vima ambavyo vitatosheleza kwa mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la Wanajeshi waliopigana Vita ya Pili vya Dunia, wale Askari wa KAR. Ni kweli kwamba, walikuwa wanapata msaada kutoka Uingereza, lakini msaada ule ulisitishwa baada ya taratibu za kuugawa kuonekana kwamba hazifai. Baada ya hapo, Wizara yangu ilikabidhiwa jukumu la kuhakikisha kwamba, tunawatambua wahusika wote ili hatimaye waweze kupatiwa fedha hizo. Tumefanya kazi ya kuwataka Wakuu wa Wilaya, waorodheshe walete Wizarani. Kazi hiyo imefanyika, lakini kwa bahati mbaya sana, majina yaliyokuja yalikuwa mengi mno, kiasi cha kwamba, tukalazimika kuitafuta *register* ya hawa waliopigana Vita ya Pili ya Dunia, ambayo iko Nairobi na London na hatimaye tumeiapata.

Maamuzi ni kwamba, sasa tutoe kwenye magazeti, wale wote ambao wataona majina yao kwenye *register* hiyo, waweze kujiorodhesha, tujue waliobaki ambao bado wako hai ndio wenye stahili hii ili waweze kupata fedha hizo. Binafsi, nimezungumza na Balozi wa Uingereza, pamoja na Mwambata Jeshi wao hapa, wamesema wao wako tayari kuisaidai Serikali, kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kutoka kwenye hicho chama cha hiari ili fedha hizi ziwafikie walengwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limechukua muda mrefu, lakini nataka kuwahakikishieni kwamba, tutalifanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo ili wanajeshi hawa wastaafu, waweze kupata fedha zao.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la milipuko iliyotokea Mabagala. Yamezungumzwa mengi, napenda nirudie kutoa pole kwa wale wote walioathika, kwa namna moja au nyingine katika mlipuko huo. Napenda nichukue fursa hii, kuwapongeza Wanajeshi wetu, waliojitoa mhanga katika kuhakikisha wanadhibiti madhara yaliyotokea pale.

Mheshimiwa Spika, wakati milipuko ile inatokea, watu walikuwa wanakimbia kutoka kwenye eneo lile, lakini Wanajeshi wetu walifanya kazi ya kuingia katika eneo, kwenda kudhibiti madhara yasiwe makubwa sana. Napenda nichukue fursa hii, kuwapongeza wote waliofanya kazi hiyo na wametusaidia sana; vinginevyo, madhara yale yangekuwa makubwa kuliko ambavyo yametokea.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Tume. Ziliundwa tume mbili; moja ni Tume ya Serikali ya kubaini uharibifu uliotokea, ambayo imeshafikisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sisi kama Wizara ya Ulinzi, tulitaka Baraza la Uchunguzi la kutafuta chanzo cha ajali na kutoa mapendekezo ili ajali hizo zisiweze kutokea tena. Napenda kusema kwamba, Ripoti hiyo nimeipokea na taratibu zitafanywa ili iweze kupita katika mlolongo wa kisheria unaotakiwa na hatimaye tutatoa taarifa kwa umma. Kwa hiyo, napenda niwatoe wasiwasi kwamba, hili suala halitafichwa fichwa; suala hili litafanyiwa kazi na taarifa ya chanzo cha ajali ile itatolewa. Vilevile tutaweza kuyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Baraza la Uchunguzi ili kuzuia ajali kama zile kutotokea tena katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mapendekezo yaliyokuwemo katika taarifa hiyo, tutayaweka bayana. Pamoja na mambo mengine, yanataka kuwe na *buffer zone,* hayo maeneo ambayo yana umbali kati ya Kambi za Jeshi na Wananchi wanapoishi, maghala yenye sifa zinazotakiwa, mafunzo kwa wanao-*handle* mabomu yale na silaha kama hizo, pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara. Kwa hivyo, haya yote yalikuwa yakifanyika, lakini kama nilivyosema, tutatoa taarifa rasmi ya matatizo haya yaliyotokea kupitia taarifa ya Baraza lile.

Mheshimiwa Spika, moja tu la kusema ni kwamba, kweli sheria za makazi zilikiukwa na kwamba, watu walikuwa wanakaribia sana Kambi za Jeshi na matokeo yake ndiyo haya yaliyotokea sasa. Suala hili tupo tayari kuliweka sawa, pamoja na kwamba, gharama zake zitakuwa kubwa, lakini tutashauri ili hatimaye tuweze kutekeleza ushauri uliotolewa na Baraza.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi walizungumzia mazingira ya kazi. Mazingira ya kazi ya Jeshi tunakiri kwamba, kwa kiwango kikubwa, bado hayajawa kama tunavyotaka hususan makazi, ofisi na vitendea kazi kwa ujumla. Serikali inaendelea na utaratibu wake wa kuhakikisha kwamba, tunashirikiana na Mashirika ya Hifadhi za Jamii, hususan NSSF, pamoja na watu wengine watakaokuwa tayari kuikopesha Serikali katika kujenga makazi bora. Tupo katika mazungumzo; ni matumaini

yetu kwamba, hilo litawezekana kama ilivyowezekana mwaka jana, lakini miaka iliyopita ilikuwa kwa kiwango kidogo cha nyumba 242 tu. Sasa tuna lengo la kuhakikisha kwamba, makazi bora yanapatikana karibu nchi nzima katika makambi yetu ili hatimaye Wanajeshi hawa warudi kuishi makambini badala ya uraiani.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, itafanyika kwa ofisi na vitendea kazi; na vitendea kazi hivi kama Wabunge walivyozungumza hapa, ni kweli kwamba, Serikali iko mbioni ili kuweza kuhakikisha kwamba, Jeshi letu kama Ilani ya Uchaguzi inavyosema, liwe Jeshi dogo la kisasa, lenye wataalam waliobobea na vitendea kazi bora. Kwa hiyo, Komandi zote za *land forces*, pamoja na ile ya *navy*, zipate vitendea kazi hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika suala la JKT. Kama ilivyoamuliwa katika Ilani ya Uchaguzi, itarejeshwa ili vijana waingie kwa mujibu wa sheria. Namshukuru Mheshimiwa Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, kwa tahadhari alizozitoa na sisi tunayaona haya kwamba, kwa kuwa sasa idadi ya wanafunzi ni kubwa sana, Waziri wa Elimu alikuwa anatuambia sasa hivi wanaomaliza kidato cha Sita wanafikia zaidi ya elfu hamsini, kuwachukua kwa wakati mmoja haitakuwa jambo rahisi.

Kwa hiyo, Serikali itajipanga vyema kuweza kuyafufua makambi haya ili hatimaye tuweze kuwachukua vijana hawa. Vilevile tutatayarisha wakufunzi wa kutosha, kuweza kutoa mafunzo yanayotakiwa. Lengo ni kufundisha vijana kuwa wakakamavu, wawe na *study* za ulinzi, pamoja na uzalendo na nidhamu inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, JKT itakuwa mstari wa mbele, kuimarisha kilimo kama wengi walivyochangia na vilevile, tutaweza kuendeleza juhudi zote ambazo zilikuwa zikifanyika hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kwamba, ni sababu zipi za msingi ambazo zilisababisha Serikali kusitisha mafunzo ya JKT huko nyuma. Jibu ni kwamba, yalisitishwa kwa sababu tu hali ya uchumi haikuruhusu wakati huo, pamoja na ushauri uliotolewa na IMF. Baada ya Serikali kurejesha shughuli za JKT 2001, imejipanga upya ili kuhakikisha maadili na malezi ya vijana yanasisitizwa na kuimarishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni hatua zilizochukuliwa: Kwanza, JKT imeanzisha Chuo cha Uongozi pale Ruvu kwa ajili ya kuandaa viongozi wa kuwalea vijana. Katika chuo hiki, viongozi huchujwa ili kuwapata wale walio bora na wenye maadili ya kulea vijana. Aidha, kulikuwa kuna hoja ya wasiwasi wa baadhi ya Wabunge juu ya unyanyasaji wa kijinsia, endapo JKT kwa Mujibu wa Sheria itarudishwa; na hapa tunasema kwamba, umeanzishwa utaratibu wa vijana kuwa na Serikali yao, ambapo watakuwa wanajiongoza wao wenyewe huku wakiwa chini ya malezi ya Viongozi wa JKT. Utaratibu huu utasaidia kubaini maovu ambayo yanatendeka na watatoa taarifa kunakohusika ili hatua ziweze kuchukuliwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, niingie katika hoja ya mabadiliko ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa; kwamba, ni kwa nini basi mpaka sasa hivi pamoja na kwamba, tulisema itakamilika mwezi wa Tisa mwaka jana, sheria hii haijafanyiwa mabadiliko?

Tunachosema ni kwamba, ile Kamati iliyoundwa kuipitia, imemaliza kazi yake na taarifa itawasilishwa kwa *Defence Forces Committee* hivi karibuni ili tuipitie na kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuchelewa ilikuwa ni kwamba, muda mwingi tuliutumia kutaka ushauri na kuwashirikisha wadau ili nao waweze kutoa mawazo yao juu ya namna bora ya kurekebisha Sheria ya Mwaka 1966. Niseme tu kwamba, baadhi ya marekebisho yameanza kufanyiwa kazi. Kwa mfano, kuongeza umri wa kustaafu, tayari hili limeshapitishwa. Kama mnalifahamu, tumelitolea taarifa. Maombi ya kukokotoa pensheni kwa wale waliotumikia zaidi ya miaka 36, pia tumeshapeleka Hazina na kwa sababu umri wa kustaafu umeshaongezwa, hatuna wasiwasi kwamba, suala hili sasa litakuwa ni historia, kwa maana kwamba, hawatakuwa wanalipwa miaka 36 tu.

Katika hatua nyingine, Sera ya Ulinzi wa Taifa inakaribia sasa kukamilika. Tumeitaka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, watoe maoni yao juu ya Sera hii na tutakapopata tu maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tayari tutakuwa tumekamilisha Sera ya Ulinzi wa Taifa, ambayo sasa itaendana vyema na Sheria ya Ulinzi wa Taifa na kuweza kutekelezeka kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda kuwa mchache, naomba nieleze tu kwamba, kulikuwa kuna hoja ya suala zima la mapigano yanayotokea katika maeneo ya Tarime na kule Rorya. Kwanza, nimshukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba, suala hili analishughulikia ipasavyo. Amekuwa akienda kule, amekuwa akijaribu kuwakutanisha Wazee wa makabila haya kwa ajili ya kuzungumza nao, amekuwa akitushauri sisi ambao tuko katika vyombo hivi vya Ulinzi na Usalama, namna bora ya kuweza kulishughulikia suala hili.

Sasa niseme tu kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, suala hili litashughulikiwa kwa kadiri itakavyoonekana inafaa, lakini maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele:-

Kwanza, tutahakikisha kwamba, taratibu zinafanywa ili wale Wazee wa makabila yanayohusika, waweze kukutanishwa na kupatanishwa ili wao watusaidie katika kupunguza matatizo haya yanayotokea kule.

Jeshi la Ulinzi la Wananchi, litaanzisha *detach* kule ili iweze kuwa rahisi kufanya doria za mara kwa mara katika maeneo yale. Kama ilivyosemwa, JKT wako tayari kuanzisha Kambi maeneo yale, kwa maana ya kujihusisha na Kilimo, lakini wakati huo huo, watakuwa tayari kutoa ulinzi katika maeneo hayo. Nimepewa taarifa kwamba, wenzetu wa Polisi, wameongeza nguvu katika eneo lile na hatimaye Serikali itashauriwa kufanya utaratibu wa kuweka *access roads* ili doria ziweze kuwa rahisi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Kwa hiyo, suala la mapigano katika maeneo hayo, litashughulikiwa kama nilivyosema, pamoja na jitihada nyingine za Serikali zitakazoonekana zinafaa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja aliyoitoa Mheshimiwa Elisa Mollel, nayo ni mgogoro uliopo baina ya Wananchi na Jeshi, katika eneo la *Tanganyika Packers* pale Arumeru.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mollel, kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba, suala hili linapatiwa ufumbuzi. Mimi binafsi ameniona, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amemwona na tumeweza kulizungumza suala hili. Wizara ya Ulinzi, pamoja na Jeshi la Wananchi, tumefikia muafaka ambao nadhani ni mzuri na tumeshauri kwa Waziri Mkuu, kwamba, tuchukue njia hiyo kulimaliza tatizo hilo.

Muafaka ambao tunauzungumzia sisi ni kwamba, kwa kuwa Jeshi ni la Wananchi na liko pale; na wananchi walio wengi tayari wako pale wamejenga, basi sasa tutenganishe ile sehemu ambayo Wananchi wamejenga waachiwe waendelee kuishi pale na ile sehemu nyingine ambayo Jeshi lipo, basi Jeshi liendelee kuchukua ile nafasi na kufanya shughuli zake za ulinzi. Kwa hiyo, kwa mtazamo wangu, naona hii ni njia bora zaidi ya kusuluhisha mgogoro huu na kama tutakubaliana kwenye maamuzi haya, basi nadhani tatizo hili litakuwa limefikia mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kueleza eneo moja, nalo ni hoja iliyotolewa ya marupurupu kwa ajili ya wale wanaokwenda kulinda amani nje ya nchi. Hoja ilikuwa, Wapiganaji wanaposhiriki katika shughuli za kuleta amani katika nchi mbalimbali ni marupurupu gani ambayo wanapewa zaidi ya mishahara ya kawaida; na marupurupu hayo hulipwa kwa utaratibu gani na kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, jibu ni kwamba, marupurupu yanayolipwa zaidi ya mshahara ni yafuatayo: Kwanza, kuna *Mission Services Allowance*, kulingana na *Memorundum of Understanding* kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Mataifa.

Pili, kuna *pocket money*, inayotolewa. Tatu, kuna fedha za likizo, yaani *leave allowance*. Vilevile utaratibu unaotumika katika kutoa fedha hizo ni kupokea fedha kutoka UN, ndipo hufikishwa kwa wahusika na Maafisa hulipwa wakiwa katika eneo la ulinzi wa amani na wengine kwa maombi yao, hulipwa Tanzania, kupitia akaunti zao, endapo wanapenda malipo hayo yatolewe hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali ni kwamba, hoja bado ninazo nyingi hapa na bila shaka, sitaweza kuzijibu zote. Nimejaribu kujibu kwa maeneo makubwa yaliyochangiwa na wengi ili niweze kuwafikia wengi, lakini kama nilivyosema awali, tutaendelea kuyaandika yote, hoja moja baada ya nyingine na kuwafikishia Waheshimiwa Wabunge ili hatimaye waweze kupata majibu yaliyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, nawe pia nadhani ndiyo maana unamsaidia Naibu Waziri, majibu yako ni ya moja kwa moja; yanalenga hoja; nadhani sote tumefahamu shughuli za Jeshi letu.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mbele yetu ni ya kukubali kupitisha Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2009/1010. Hoja imeungwa mkono, lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 100 na 101, itabidi Katibu atupeleke kwenye utaratibu unaofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 38 - Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

Kif. 1001 – *Defence Forces Headquarters'*
*Command … ... .... .... ... ... .... .... Shs. 291,365,991,700*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho kilichotajwa, naomba nipate ufafanuzi. Kwa kuwa kila tarehe Mosi Septemba ya kila mwaka, huwa kunafanyika sherehe za mashujaa wetu; na kwa kuwa sherehe hizo kila mwaka naona zikifanyikia Dar es Salaam, ambayo nadhani siyo Makao Makuu ya nchi, yanaweza kufanyika pia katika mikoa mingine; je, Mheshimiwa Waziri, utakubaliana nami kwamba kwa mwaka unaofuata ikiwezekana sherehe hizo pia zifanyike katika Mji wa Songea kwa kuwa Mji huo una historia kubwa ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ingawa hukusema, bado hatujafika kwenye Fungu 57, ambako ndiko tunaukuta Mshahara wa Waziri. Usithubutu kuushika Mshahara wa Jenerali, utaleta balaa hapa wewe. (*Kicheko*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, sina haja ya kushika Mshahara wa Jenerali hata kidogo. Programu Ten, Subvote 1001 na Subvote 221700, ambayo inazungumzia *Food Supplies and Services.*

**MWENYEKITI:** Sawa endelea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula ni muhimu sana katika Jeshi na wote ambao tumepitia *National Service* tunajua hilo. Eeh! lakini kwa *numbers* kidogo hapa zinanipa shida labda nielezwe kwamba, chakula kimeongezeka. Kulikuwa na shilingi bilioni 35 mwaka 2007/08, shilingi bilioni 24 mwaka 2008/09 na mwaka huu shilingi bilioni 81.6; sasa hii nina hakika Bunge lako Tukufu linahitajai

maelezo kama Wanajeshi sasa watanenepa sana; au watapata chakula cha kutosha; au ni msingi gani pamekuwa na nyongeza ya namna hii?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Cheyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kwamba, mwaka huu tuna nyongeza katika hizi fedha za chakula, kwa maana ya *ration allowances.* Huko nyuma, walikuwa wanapata shilingi 2,500 kwa siku, mwaka jana waliendelea kupata shilingi 2,500, lakini zikaongezwa katikati hapo kwa *extra budgetary measures* na sasa hivi ndiyo tumekubaliana kwamba, watapewa shilingi 5,000. Kwa hiyo, hii nyongeza unayoina hapa ni kutokana na nyongeza hiyo ya *ration allowances. (Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 – *Land Forces Command* … Shs. 11,722, 788,100

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 – Air *Forces Command* … .... ..... Shs. 6,379, 899,600

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1009 – *Navy Command* … ..... .... Shs. 3,238, 525, 600

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Subvote 230900 - *Routine Maintenance and Repair of Naval Operations Including Sea.* Katika mchango wangu, ambao nimempelekea Mheshimiwa Waziri, ingawa hakutamka kwamba, na mimi nimechangia kwa maandishi. Nilionesha kusikitika kwangu, jinsi ambavyo kuna uchakavu mwingi sana *including* wa meli katika Kikosi au Kitengo hiki cha *Navy;* na nikiangalia fedha iliyoko na yale ambayo tuliyaona pale, nashangaa kama kweli milioni 727 hizi zitakidhi katika kuliweka Jeshi letu vizuri zaidi kwa upande wa *Navy;* ukizingatia kwamba, hali halisi katika Bahari yetu Kuu, kuna maharamia na nini na ulinzi unahitaji kuimarishwa? Kwa hali kama hii; kweli hizi fedha zitatosha kusaidia kutatua matatizo ambayo yako kwenye *Navy*? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analolizungumzia Mheshimiwa John Cheyo ni kuhusu *Routine Maintenance and Repair of Naval Operations.* Fedha zilizokuwepo hapo, ndiyo hizo

zinazozungumzia masuala ya *repair* na *maintenance* na zana tulizokuwa nazo kwamba, zinahitajika kama shilingi milioni 700.

Kama Mheshimiwa Cheyo, anazungumzia ununuzi wa vyombo vipya, niseme tu kwamba; fedha zilizopatikana katika bajeti ya mwaka huu ni hizi kwa ajili ya *repair* ya vyombo vya *Navy*. Kama nilivyokuwa nazungumza siku za nyuma ni kwamba, hili suala la uharamia lina njia nyingi za kupambana nalo. Sisi wenyewe kama Jeshi la Tanzania, uwezo wetu kwa sasa ni kufanya doria katika *territorial waters*, zile *High Seas*. Tuna ushirikiano na nchi nyingine, zikiwemo za *SADC*, pamoja na nchi za Mataifa makubwa, ambazo wana *Naval Ships* zao katika maeneo ya Ghuba ya Aden.

Pia ni kweli kwamba, tunahitaji fedha zaidi, lakini zipo taratibu zinazopangwa kwa ajili hiyo, hatimaye tuweze kupata mikopo nafuu ya kuweza kupata zana bora zaidi za kufanya shughuli hii.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service Force* … ... Shs. 69,077,870,000

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Katika kifungu hiki cha mwanzo.

**MWENYEKITI:** Unacheka au unakohoa? *(Kicheko*)

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Nakohoa. Programu ya *National Serivice,* kifungu 210100. Naomba kuulizia kwamba, kwa sababu *National Service …*

**MWENYEKITI**: Umesema kifungu gani?

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Kile cha 210100.

**MWENYEKITI:** Hicho ni mishahara.

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Huwezi kuchukua mshahara wa Jenerali wa JKT, hawajibiki kwetu, huwa tunachukua mishahara ya wale wanaowajibika kwetu.

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Mwenyekiti, basi nitauliza baadae.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and General* … ... Shs. 11,638,192,400

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nitumie Subvote 1001.

**MWENYEKITI:** Nimekwishakielewa, mkisimama hapo ni Mshahara wa Waziri. Haya endelea.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ngerengere linatunza heshima kubwa sana kwa nchi hii. Mimi ndiyo njia yangu ya kwenda nyumbani kwangu, lakini ukipita pale kila wakati unasikitika; Wanajeshi wale na Maafisa wako njiani, wanangoja Mabasi, wapo pale wanatimuliwa mavumbi. Sasa ningependa kufahamu, kama Serikali ina mpango wowote wa kuwapatia basi la usafiri angalau la kuwapeleka mpaka mwisho Ubena?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwenegoha, kama ifuatavyo:-

Jeshi limenunua magari mapya zaidi ya 600 na kitu; kuna ambayo yalishawasili na yalishasambazwa katika makambi mbalimbali, kuna ambayo yanategemewa kufika muda wowote. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba, endapo yatafika hayo ambayo yanasubiriwa, basi na Kikosi hiki cha Ngerengere, kitaweza kupata usafiri wa kudumu. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwa kutumia kifungu hiki, nihusishe swali langu ili nisipoteze muda. Nadhani Mheshimiwa Waziri, alikuwa amesikia kuhusiana na umuhimu wa maadhimisho ya tarehe Mosi Septemba, ambayo yanawaheshimu Mashujaa wetu, yasifanyike Dar es Salaam peke yake na badala yake yaweze kuwa yanazunguka hata kwenye mikoa mingine, tukianzia na Mkoa wa Ruvuma, ambapo Mji wa Songea unakumbukwa kwa mashujaa wa Majimaji.

Je, Mheshimiwa Waziri, mwaka unaofuata unaweza ukahamishia shughuli hizo zifanyike Songea? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Meshimiwa Eng. Stella Manyanya, kama ifuatavyo:-

Sherehe hizi zinaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini suala lake kwa kweli ni ushauri ambao unazungumzika. Kwa mfano, tu Sherehe za Mashujaa kwa mwaka huu, ninaambiwa kwamba, zitafanyika katika Kambi ya Kaboya, Mkoani Kagera. Kwa hiyo,

sioni kwa nini katika siku za usoni zisiweze kufanyika kule Songea? Kwa hiyo, tutafikisha mawazo haya kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili iweze kuwa hivyo.

**MWENYEKITI:** Na kwa mzunguko hata Milambo Barracks. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika kifungu hiki cha 210100, ambacho ninaomba Waziri anifahamishe, kwa sababu JKT na Jeshi vinasaidia kujenga *skills* za vijana; kwa nini kusiwe na Kambi ya JKT na ya Wanamaji katika Wilaya ya Ukerewe?

**MWENYEKITI:** Dah! Mheshimiwa Waziri! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mongella, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu JKT; Makambi ya JKT yako mengi nchini na ipo dhamira ya kuanzisha katika kila Wilaya kwa siku za baadae, uwezo wa kifedha ukiruhusu. Hivi sasa wamekuwa wakitafuta maeneo muafaka, kwa ajili ya aidha, kuanzisha mapya na vilevile kufufua yale ya zamani kwa kazi hii ya kuchukua vijana kwa Mujibu wa Sheria.

Kwa hiyo, kwa ombi lake Mheshimiwa Mongella la JKT kule Ukerewe; nadhani ni zuri tu, endapo uwezo utapatikana wakati huo wa kuanzisha kila Wilaya, basi na Ukerewe nayo itaweza kupata Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Wanamaji, niseme tu kwamba, hii *Command* ya *Navy* ina maeneo yake maalum, ambayo sasa hivi wanafanyia kazi zao. Nadhani eneo analolizungumzia Mheshimiwa ni ulinzi unaofanywa na vikosi vilivyoko karibu na Ziwa Victoria. Kwa hiyo, sidhani kama kwa sasa kuna haja ya kuanzisha Kambi ya *Navy* huko.

**MWENYEKITI:** Ushauri tu Mheshimiwa Waziri, hata kama mnataka kuweka JKT Ukerewe, msithubutu Kisiwa cha Ukala. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho, ninaomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri au maelezo. Mwaka jana niliwahi kusema ndani ya Bunge hili kwamba, kuna Watanzania wengi; askari, pamoja na raia, ambao walipigana Vita vya Kagera mwaka 1978/79; wengine wengi waliumia na wengine walipata ulemavu wa kudumu. Niliwahi pia kusema kwamba, nina mtu mmoja kule Mbeya, ambaye alishiriki katika vita hiyo na alipata ulemavu, anaitwa Ndugu Saidoni Mzumbwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu bwana tangu amekwenda nyumbani, hajapata msaada wowote na Serikali. Nilipouliza mwaka jana na wewe ulisaidia ukasema hivi; Serikali ingekuja na utaratibu wa kuwaorodhesha wale wote walioumia na kupata madhara ili ione namna ya kuwasaidia vizuri zaidi. Mpaka leo, hatujapata maelezo ya

Serikali, wanachukua hatua gani katika kuwasaidia Watanzania hawa, ambao waliiletea nchi yetu sifa, lakini baada ya kumaliza vita na wengi wakapata madhara wameachwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa maelezo gani?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Zipo Kanuni za Jeshi zinazohusiana na malipo ya wastaafu na malipo ya walioumia wakiwa kazini. Ndiyo kama nilivyokuwa nazungumza wakati nahitimisha hoja yangu ni kwamba, hawa askari waliopigana Vita vya Kagera, wanachokipata sasa hivi ni pensheni zao na wale walioumia wanapata hiyo *disability allowance*, ambayo imekuwa ikitolewa kwa viwango mbalimbali, kutegemea na kiwango cha ulemavu.

Sasa nataka tu nimwombe Mheshimiwa Zambi, huyu anayemzungumzia kwa sababu ni *specific case,* hapati pensheni au hiyo *disability allowance;* basi naomba aniletee jina lake na nitahakikisha kwamba hiyo stahili yake anaipata.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Hotuba yetu ya Upinzani, tulitaka kupata ufafanuzi juu ya posho ya chakula, inayoitwa *ration allowance* kwamba, kuna baadhi ya Majeshi wanapewa fedha zao taslimu, shilingi laki moja na nusu; lakini wengine hawapewi fedha hizo, wanakula kwa zabuni na hata chakula ambacho wanapata hawa wengine, hakitimii shilingi 5,000 kwa siku. Kwa nini utaratibu huu usiwekwe tu kwa wote kwamba kila mmoja apewe shilingi laki moja na nusu *cash* kuliko kula kwa zabuni? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Hii posho ya *ration allowance*, kwa kawaida inatolewa kwa wazabuni ili askari waweze kupata chakula na ndipo ilipokuwa utaratibu wa kupata milo mitatu kwa siku, kwa fedha ambayo ilionekana ndogo sana na sasa hivi ndiyo hiyo imefikia kiwango cha shilingi 5,000.

Wanaopata fedha taslimu ni wale ambao wanajitegemea, kwa maana kwamba, wana makazi yao nje ya Makambi. Vile vile Makao Makuu ya Jeshi, yalianzisha utaratibu wa kuangalia kama unaweza ukawa bora kuwapatia fedha hizi taslimu kwa pale Makao Makuu. Kilichoonekana ni kwamba, baadhi yao hawali tena na kwa hiyo ni kinyume na utaratibu, kwa sababu tunataka Wanajeshi hawa wakati wote wawe sawasawa kwa kazi. Kwa hiyo, kutokana na uzoefu huo, huenda hata utaratibu huo wa kwanza kwa wale walioanzishiwa kupewa fedha, itabidi warudi nyuma waanze kuwalipa wazabuni ili wawe wanakula na muda wote wawe tayari kwa kazi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimechangia kwa maandishi, kufuatia ombi langu la mwaka jana kuhusu kuanzishwa kwa Kambi ya

JKT pale Kirurumo Ukimbu. *Corridor* hii ya kutoka Itigi mpaka Mbeya, takriban kilomita 500. Sababu mojawapo, pamoja na shughuli za JKT na JWTZ, ambazo ni nzuri, lakini tuliomba pia kwa sababu ya tatizo la ujambazi na ujangili, maeneo hayo ambapo kuna mapori makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulielezwa kwamba, tufuate utaratibu wa Kanuni za Jeshi kwamba, ipitie kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoani. Tulifanya hivyo, nilitarajia labda ningepata majibu mwaka huu kwamba, *status* ya ombi hilo ikoje. Kwa hiyo, ningeliomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Lwanji, swali lake kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema, dhamira ya kuanzisha Makambi haya ipo. Tunataka yawe mengi, kwa sababu tunataka kuanza kuwarejesha vijana hawa, ambao ni wengi kama nilivyosema. Tatizo kubwa ni uwezo wa kuweza kuyaanzisha maeneo yote yanayohitajika kwa wakati mmoja haupo. Ndiyo maana sasa hivi kipaumbele kimewekwa katika kuyafufua yale ambayo tayari yapo, miundombinu ipo kwa gharama nafuu zaidi. Ombi lako Mheshimiwa Lwanji tunalipokea na ikitokea fursa, tutaweza kufanya hivyo ambavyo Mkoa wako unaomba.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja, ambaye hakutaja jina lake; ameniandikia kwamba; kuhusiana na Ukala, Wana-Ukala wamenisikia, nitachukuliwa na mamba kule Mtera. Kwa hiyo, jamani mimi sipiti tena barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa kupitia Mtera na sababu ni hizo. *(Makofi/Kicheko)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*… … Shs.216,930,200
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … Shs.480,364,600
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* … … Shs. 79,942,400
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*… Shs. 46,776,100
Kif. 1006 - *Legal Services Unit* … … Shs. 50,475,900
Kif. 1007- *Information, Education and Communication* .... … … Shs. 22,700,000
Kif. 1008 - *Military Tender Board Unit*… … Shs. 84,835,000
Kif. 1009 - *Independent Telecommunication Network* … … … … Shs. 21,200,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Industries, Construction and Agriculture* Shs. 393,113,400

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi katika hii Programu 20 - *Productive Services, Subvote 2001.* Ninaangalia *Industries Construction and Agriculture*, lakini sioni *item* yoyote ambayo ina-*address* suala hili la *agriculture*. Nilitaka nizungumzie JKT Itende, kuhusu ukulima wa kahawa lakini sioni hapa. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Tumeshapita Fungu la JKT.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Military Reserch and Development*… Shs. 359,700,000

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 38 – Wizara ya Ulinzi**

Kif. 1001 – *Defence Forces Headquarters' Command* …. .... .... .... .... .... ..... ..... Shs.20,000,000,000

**MHE JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vote 1001, Subvote 5492, haikutengewa fedha, lakini sehemu hii inahusika na UKIMWI. Sasa nataka maelezo kidogo tu kwamba, UKIMWI uko kila mahali *including* Jeshini; nimeona kama vile hizi fedha zilikuwa zaidi zinategemea kutoka *World Bank;* je, kuna mahali pengine popote ambapo Mheshimiwa Waziri ame-*provide* kwa sababu ya Programu ya UKIMWI kwa ajili ya kusaidia vijana wetu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa John Cheyo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Programu hii ambayo ilikuwa inafadhiliwa na Benki ya Dunia sasa imekamilika, fedha hizo hazitakuwepo kwa mwaka huu. Tumejaribu kuweka katika maeneo mbalimbali katika bajeti yetu ya kawaida, ikiwemo kwenye sehemu ya *Medical Supplies,* baadhi ya fedha kwa ajili ya kuwasaidia wale ambao wanatumia dawa na katika Utawala kule kwa mafunzo na kadhalika. Kwa hiyo, tumeliangalia hilo na tumeweza kuweka kiasi kidogo cha fedha, kwa ajili ya kuendeleza shughuli ambazo zilikuwa zinafanyika na fungu hili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service Force*… ... ... Shs.13,500,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and General* … ... ...... Shs. 00
Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … .... Shs. 230,000.000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2001 – *Industries, Construction and Agriculture…* .... ..... .... .... .... ..... .... Shs.14,431,518,000

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwamba uliniona, sasa nimepaona mahali penyewe hasa pa kuzungumzia.

Nilikuwa naomba ufafanuzi kwamba, katika kifungu 2001, nilitaka kujua kwa upande wa kilimo kama JKT Itende nao wapo katika programu ya kuboresha kahawa yao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mpesya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Mheshimiwa Mpesya, yuko katika kifungu ambacho sio sahihi kwa swali lake. Sasa hivi hapa tuko katika *Development Vote* ya Wizara na hii ni Idara katika Wizara na madhumuni ya Idara hii ni kuangalia hayo masuala yaliyotajwa hapo, lakini siyo sehemu ya JKT. JKT wana *Development.*

*S*ijui kama nimeeleweka Mheshimiwa Mwenyekiti?

**MWENYEKITI:** Nadhani umsaidie tu, kama una habari zozote kwa sababu amehangaika sana. Je, kuna mambo ya kilimo maana yake mmetaja hapa *Industries, Construction and Agriculture,* hata kama ni kwa maana ya sera na kadhalika; kutokea Makao Makuu mna-*support* hizo kwenye Makambi yoyote na hususan Itende?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba, Idara hii ambayo iko chini ya Wizara, madhumuni yake ni kusaidia viwanda, kilimo, pamoja na *construction* ambazo zinafanywa na JKT.

**MWENYEKITI:** JKT Itende inaweza ikabahatika?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Nitashauriana na Uongozi wa JKT, kuona tunaweza kusaidiaje hilo.

**MWENYEKITI:** Naona mambo ni mazuri tu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Military Research and Development* ... .... Shs. 00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, kabla sijatoa taarifa, naomba niwataje baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ambao walichangia katika hoja yangu, lakini kwa bahati mbaya sikuwataja. Naomba nimtambue Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua hao, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu, liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza awali, hoja iliyoko mbele yetu hapa ni ya Bunge kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2009/2010.

Hoja imetolewa na Mheshimiwa Waziri mtoa hoja na imeungwa mkono, sasa wajibu wangu ni kuwahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja imepitishwa kwa heshima zote za Kijeshi na kwa hiyo, nafurahi kutangaza kwamba, Bunge letu limepitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2009/2010. Sasa wajibu wangu ni kuwatakia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Jeshi letu, kuanzia Jenerali mwenyewe mpaka Makamanda, Maafisa Wapiganaji, pamoja na Vikosi vya JKT kwamba, tunawatazamia mtafanya kazi vyema; na wakati wote, nadhani Serikali inapopata nafuu zaidi, itaendelea kutazama jinsi ambavyo mtaongezewa ili kuzidi kuienzi kazi yenu nzuri.

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika – Taarifa.

Asubuhi wakati Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akisoma hotuba yake; ukurasa wa nne kwenye hotuba yake, alimtaja aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Nyaulawa kama Marehemu Julius Nyaulawa.

Mheshimiwa Spika, nashawishika kusimama kuweka kumbukumbu sahihi, kwa sababu nilikuwa jirani sana na Marehemu Nyaulawa kuwa, majina yake kamili ni Richard Saidi Nyaulawa na wala hakuwa Julius Nyaulawa. Nataka kufanya hivyo, kwa sababu ya kumbukumbu.

Ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana kutukumbusha hilo, mara nyingine haya yanatokea katika uchapaji, jina la kwanza likakosewa. Nadhani ni kwa bahati mbaya tu. Ahsante kutukumbusha hilo.

Kwa hiyo, sina matangazo yoyote, naliahirisha Bunge huku nikiwatakia Sikukuu njema ya kesho (Saba Saba).

Naliahirisha Bunge hadi Siku ya Jumatano tarehe 08 Julai, 2009, tutakapozungumzia Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi humu Bungeni saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.19 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 08 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*